# Nipashe

Ijumaa Agosti 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580004

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




Spika Ndugai aona fursa mkutano mabunge ya CPA

UKURASA 3


Umeme Stieglers: Mlango wa kufikia dira ya maendeleo — Ukurasa 19

Lindi, Mtwara 'kucheele' waamka kulima ufuta — Ukurasa 18

BUFE

Ijumaa Agosti 23, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Onyo la Marekani laiogopesha Ugiriki kuisaidia meli ya Iran — Ukurasa 15

Michikichi yapewa kupaumbele, TARI Kahinga uwanja mpya wa maboresho

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

TANZANIA inatumia mabilioni ya fedha kila mwaka takribani bilioni 600 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje kwa vile kiwango cha bidhaa hiyo kinachozalishwa nchini hakikidhi mahitaji ya walaji.

Kwa kiasi kikubwa mafuta yanayozalishwa yanatokana na michikichi ambayo pamoja na kuchakatwa mafuta ya kula kama mawese kuna mengine yanayotumiwa viwandani au mafuta ya mise ambayo hupatikana hapa nchini japo kwa kiwango kidogo.

Chikichiki ndilo zao linalotoa mafuta mengi kwenye yale yanapandwa ukilinganisha na mazao mengine kama alizeti, ufuta, pamba, karanga na soya, wanasema wataalaamu wa kilimo.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI Habari katika picha — Ukurasa 17

Mradi unaowanasua waliokwama baada ya shule hadi ujasiriamali Ukurasa 20

UKURASA 13

# Polisi alivyobwia 'unga' miaka 17

• **Asimulia** alivyokodisha sare za jeshi kwa majambazi, alivyofahamika kwa jina la 'Jesus'... *Endelea uk.4*



Aliyekuwa Askari Polisi, Ambani Famili, ambaye kwa sasa ni Mratibu wa Mafunzo wa Asasi isiyo ya kiserikali ya Mefada, akifafanua jambo alipofanya mazungumzo na gazeti hili, Kinondoni, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JOHN BADI**

## YALIYOMO


UKURASA WA 7

**SABABU MKOA KUKAA GIZANI SIKU TATU HIZI**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) limetoa ufafanuzi kuhusu katizo la umeme lililotokea...

UKURASA WA 21

**MBARONI TUHUMA MENO YA TEMBO 13**

JESHI la Polisi linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kukutwa na vipande 13 vya meno ya...

UKURASA WA 26

**MAGUFULI ATETA NA MABALOZI 43 IKULU**

MABALOZI wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani wamempongeza Rais...


## Tamko la uchaguzi wa mitaa rasmi leo

UKURASA 2

## Tahadhari maambukizo VVU

• **Utafiti** mpya wabainisha watu 10 nchini hupata virusi kila saa... *Endelea ukurasa 2*


MICHEZO SIMBA HII UKIUMIA UMEPOTEZA NAMBA UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

# Tahadhari kasi maambukizo mapya VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) imesema maambukizo mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) yako juu na kwamba utafiti mpya umebaini kwamba kila saa moja watu 10 wanaambukizwa maradhi hayo.

Kutokana na utafiti huo, tume imetoa tahadhari kwa wananchi kuchukua hatua za kujikinga ili kujilinda na maambukio mapya.

Akizungumza jana katika semina ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ukimwi, Dawa za Kulevya na Kifua Kikuu na ile inayoshughulikia sheria ndogo, Mkurugenzi Mtendaji wa Tacaids, Dk. Leonard Maboko, alisema katika utafiti uliofanywa mwaka 2016/17 kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilionyesha kiwango hicho cha maambukizo.

Alisema kuanzia Januari hadi Desemba, walikadiria maambukizi mapya kila mwaka ni watu 72,000, hivyo ni vyema watu wakachukua tahadhari kujiepusha na hali hiyo na pia kujitokeza kupima ili kujua afya zao.

"Hivyo kwa mwezi ni watu 6,000, kwa siku ni watu zaidi ya mia mbili na kwa saa ni watu 10 kila siku wanapata maambukizo mapya ya virusi vya Ukimwi," alisema.

**Hakuna uhaba wa kondomu**

Kuhusu madai kwamba kuna uhaba wa kondomu, Dk. Maboko alisema hakuna tatizo hilo kwa kuwa tayari wameshapokea kondomu milioni 30.

"Ni kweli kulikuwa na upungufu wa bidhaa hasa mkoa wa Njombe katika kipindi cha kuelekea mwisho wa mwaka jana na hali hii ilitokana na michakato ya namna ya uagizaji kwa wanaotengeneza," alisema.

Alibainisha mpaka sasa kondomu zimeshafika nchini kwa idadi hiyo na ziko Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

"Kondomu ambazo zilipotea ni zile zinazotolewa bure ambazo zinawekwa katika mikusanyiko ya jamii kama vituo vya afya, vyuoni na mahali pengine, lakini hivi sasa kondomu hizi zimeshaanza kusambazwa kwenye vituo vya MSD kanda, hivyo wadau waagize ili zifike kwa walengwa," alisema.

Akizungumzia kuhusu 90-90-90, Dk. Maboko alisema kama nchi imefanya vizuri katika 90 ya pili ya walioambukiza kuanza kutumia dawa ambayo lengo ni kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2030, lakini kwa sasa ipo kwa asilimia 94.

"90 ya kwanza ni ifikapo mwaka 2030 Watanzania wawe wamejua hali zao, 90 ya pili ni waliojua hali zao wawe wameanza kutumia dawa ya kufubaza virusi na 90 ya tatu ni wanaotumia dawa wawe wamefubaza virusi hivyo. Hapa kwenye 90 ya pili tumefanya vizuri na tumevuka lengo," alisema.

Dk. Maboko alisema 90 ya kwanza bado nchi iko kwenye asilimia 61 hali iliyosababisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuamua kuwa balozi wa kuhamasisha wanaume kujitokeza kupima kwa kuwa wapimaji wengi walikuwa wanawake na 90 ya tatu imefikia asilimia 87 kwa sasa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ukimwi, oscar Mukasa, alishauri kuwapo kwa vyanzo vingine vya fedha ili nchi ipambane na Ukimwi badala ya kutegemea nchi wahisani ambao wanakusudia kupunguza misaada kwa asilimia 23 kuanzia Oktoba, mwaka huu.

Alisema kama nchi ni muhimu sasa kukaangalia vyanzo vingine vya mapato ili kuweza kusimama wenyewe.

"Ni wakati sasa wa kuisukuma serikali tupate tozo maalum kwa ajili ya kuweka kwenye mfuko wa kupambana na Ukimwi. Uwapo mfuko wa uwekezaji utakaoleta pamoja sekta binafsi ikiongozwa na sekta ya umma kwenye kutafuta njia mbadala ya kupata fedha," alisema Mukasa.



Rais John Magufuli akizungumza katika kikao na mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**.

# Kipenga uchaguzi wa S/Mitaa kupulizwa leo

**Na Enock Charles**

TAREHE rasmi ya kufanyika kwa uchaguzi wa serikali za mitaa, itajulikana leo, baada ya serikali kuahidi kutoa tamko.

Serikali iliwahi kutamka kuwa uchaguzi huo utafanyika Oktoba, lakini haikuwahi kuweka wazi tarehe rasmi.

Vyama vya siasa na wadau wamekuwa wakilalamikia ukimya wa serikali kutotoa tamko kuhusiana na uchaguzi huo husasan tarehe na kanuni za uchaguzi huo.

Tangazo hilo linatarajiwa kutolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi), Selemani Jafo, atakapokutana na wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa na wadau wengine jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Tamisemi, mkutano wa Waziri Jafo na viongozi hao utafanyika jijini Dodoma leo kwa lengo la kutoa tangazo la uchaguzi huo na maelekezo mengine mbalimbali.

"Lengo la mkutano huo ni kutoa tangazo la uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 na maelekezo mbalimbali kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa kawaida uchaguzi huo hufanyika mwaka mmoja kabla ya uchaguzi mkuu, lakini kutotangazwa kwa tarehe na kanuni za uchaguzi huo, kumeibua wasiwasi kwa vyama vya siasa.

Wadau wa uchaguzi ikiwamo vyama vya siasa wametoa malalamiko wakidai kuchelewa kutangazwa kwa kanuni kunaweza kuathiri maandalizi kuelekea uchaguzi huo, kwa kuwa kuzifahamu kanuni hizo ni moja ya maandalizi muhimu katika uchaguzi huo.

Akizungumza na gazeti hili mapema wiki hii, Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alidai kuchelewa kutangazwa kwa kanuni hizo kunaathiri mchakato wa vyama kufanya maandalizi ya mafunzo kwa mawakala na wagombea wao katika uchaguzi huo.

"Kuchelewa kutangazwa kwa kanuni itakayotumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa kunaathiri maandalizi yetu kwa sababu huwezi kuandaa wagombea kwa mfano, bila kujua kanuni zinasemaje kuhusu sifa za wagombea wanaotakiwa, maana kubadilika kwa kanuni kunaweza kupelekea kubadilika kwa aina ya mgombea," alisema Shaibu.

Uchaguzi huo unatarajiwa kutumia Sh. bilioni 82, na kinachosubiriwa na wadau wa uchaguzi husasan vyama vya siasa, ni kutangazwa kwa tarehe na kanuni zitakazotumika kusimamia uchaguzi huo.

Taarifa ya Tamisemi imetolewa siku chache baada ya Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mwita Waitara, kuwataka Watanzania kuwa na subira kuhusu uchaguzi huo, huku akisema suala hilo aachiwe Rais.

# RC Moro aiagiza Nida kuongeza vituo

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Steven Kebwe, ameiagiza Ofisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) mkoa, kuongeza vituo vya kutoa huduma hiyo katika wilaya zote ili kuwasaidia wananchi hasa waishio vijijini kupata huduma hiyo kiurahisi na kukamilisha katika muda mwafaka.

Dk. Kebwe alisema hayo jana wakati alipotembelea ofisi hizo kufuatia malalamiko yaliyotolewa na wananchi kuhusu kuchelewa kupata namba na vitambulisho jambo linaloleta athari za usajili wa laini za simu kwa jamii.

Alisema, licha ya kazi hiyo kuendelea, lakini bado miezi minne pekee kusitishwa kwa usajili wa laini za simu kwa alama za vidole mwezi Desemba mwaka huu, huku watu wengi wakiwa bado hawajapata.

Aliitaka jamii kuwa na mwamko wa kuitumia nafasi iliyopo ya kwenda kupata huduma hiyo kwa wakati kwa kuwa kuchelewa kunaweza kuleta usumbufu baadaye.

Rajabu Ally, mkazi wa Manispaa ya Morogoro alisema, upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa bado ni changamoto kutokana na vigezo au vielelezo na masharti vilivyowekwa ikiwamo mtu kutakiwa kuwa na cheti cha kuzaliwa au cheti cha shule hali inayowalazimu kufuatilia kwa kipindi kirefu bila ya mafanikio.

John Msekwa, mkazi wa Tungi alisema, serikali za mitaa zinatakiwa kuchukua nafasi yake kwa kuwatambua wakazi wa maeneo husika ili iwe rahisi kwao kupata vitambulisho bila kutegemea masharti yaliyopo.

"Nina miaka ya kuzaliwa zaidi ya 70 hapa, cheti nakipata wapi kwa sasa na nina mwezi wa sita natafuta kitambulisho, kitambulisho changu cha kupigia kura kimeharibika sana, kila ninapokwenda wanagoma kunisajilia laini, sasa serikali ya mtaa ikisimama kwa hilo wengi tutapata vitambulisho," alisema.

Ofisa Usajili wa vitambulisho NIDA mkoani hapa, James Malimo alisema, kuchelewa kwa upatikanaji wa vitambuliso hivyo kwa baadhi ya wananchi kunatokana na wengi kushindwa kutimiza masharti yaliyowekwa na kwamba yapo maombi mbalimbali yamekwama kutokana na changamoto za wananchi kushindwa kuwasilisha vielelezo zaidi.

Aliwaasa wananchi kuhakikisha wanakamilisha masharti hayo ya vielelezo vya msingi na wanavipata kwa wakati ili kukamilisha usajili na maombi yao yafanyiwe kazi kwa kuwa hawatamsajili mtu bila kuwa na vielelezo ili kuepuka kuwasajili wasio Watanzania.

# Mahakama yakataa kupokea nyaraka kesi ya kina Aveva

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeshindwa kuendelea kusikiliza ushahidi wa kesi ya kughushi na kutakatisha Dola za Marekani 300,000 inayowakabili Rais wa Klabu ya Simba, Evance Aveva na mwenzake baada ya utetezi kupinga nyaraka za punguzo la tozo la kodi zisipokelewe.

Wakili wa utetezi Nehemia Nkoko, alitoa pingamizi hilo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kwamba nyaraka za msamaha wa tozo ya kodi inazodaiwa za kughushiwa zisipokelewe kama kielelezo.

Awali, shahidi wa Jamhuri Mchunguzi Mkuu kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Frank Mkilanya, alidai kuwa katika uchunguzi wake alibaini barua kutoka Simba kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya kuomba msamaha wa tozo ya Dola za Marekani 40,000 badala ya kiwango halisi cha Dola za Marekani 109,000

Mkilanya, alidai nyasi bandia zilinunuliwa kwa wakala anayeitwa Hamisi na zilitoka katika Kampuni ya Nina iliyopo China.

Alidai kuwa wakati wa uchunguzi alimhoji mshtakiwa Hans Poppe, ambaye alidai Hamisi alifariki na akampa hati ya kusafirishia mwili ambayo aliomba kuitoa kama kielelezo.

Wakili wa Serikali, Leonard Swai, aliomba kutoa kielelezo hicho, lakini Wakili Nkoko, alipinga kwa madai kwamba si nakala halisi na kinachothibitisha kifo ni cheti cha kifo.

Akitoa uamuzi Hakimu

INAENDELEA UK.8



Mfanyabiashara Hariri Mohamedi Hariri na mkewe, Muna Saidi, wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, wakikabiliwa na kesi ya kusafirisha gramu 214.11 za dawa za kulevya aina ya heroine. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ndugai anusa fursa mkutano CPA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema ujio wa Mkutano wa 50 wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola kanda ya Afrika (CPA) ambao utakuwa na washiriki takribani 400, utatoa fursa nyingi kwa Tanzania ikiwamo kutoa kibali cha uwekezaji wa hoteli ya nyota tano jijini Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ndugai alisema mkutano huo utafanyika Zanzibar kuanzia Agosti 31, hadi Septemba 5, mwaka huu na utafunguliwa Septemba 2, na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

INAENDELEA UK.8

# Mawakili kesi ya Mbowe chupuchupu kukamatwa

**Na Hellen Mwango**

HAKIMU Mkazi Mkuu, Thomas Simba, jana nusura awaamuru askari polisi kuwakamata mawakili wa pande zote mbili katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, baada ya kudaiwa kwamba shahidi anasoma ushahidi wake.

Kadhalika, hakimu aliwaamuru askari polisi waliokuwa ndani ya ukumbi namba moja kukaa tayari kwamba anaweza kutoa amri ya kukamatwa mawakili kutokana na utovu wa nidhamu.

Saa 6:12 adhuhuri, ukumbi namba moja wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Simba, ilianza kusikiliza kesi hiyo.

Shahidi wa saba, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Victoria Wihenge (30), alipanda kizimbani kutoa ushahidi lakini wakati akiendelea na ushahidi wake, mawakili wa utetezi, Hekima Mwasipu na Nikson Matata, walinyanyuka kwenda kwenye kizimba cha shahidi huyo.

Mawakili hao walikwenda kizimbani hapo kwa madai kwamba shahidi ananukuu pembeni kwa siri wakati akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon.

Hata hivyo, Wankyo alililalamikia mahakama kwamba mawakili Mwasipu na Matata wanamtishia shahidi kizimbani.

Wakati hayo yakiendelea, Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alikuwa akilumbana na Wakili Matata hali iliyozua mzozo, huku wakijibishana bila kufuata utaratibu wa kisheria.

INAENDELEA UK.8




# Simulizi polisi aliyebwia 'unga' kwa miaka 17

**Na Romana Mallya**



AMBANI Famili anasimulia namna alivyojiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kwa miaka 17 kulikosababisha afungwe jela na kufukuzwa kazi katika Jeshi la Polisi lililokuwa limemwajiri.

Jumanne Julai 23, mwaka huu, Nipashe ilizungumza na askari polisi huyo wa zamani ofisini kwake Kinondoni jijini Dar es Salaam anakohudumia watu walioathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya, maarufu unga.

Famili **(pichani)** anaeleza kuwa kutokana na tamaa ya kupata mafanikio kimaisha kwa haraka ya kimaisha, alijikuta akitumbukia kwenye kadhia hiyo iliyompeleka jela kutumikia kifungo.

Anasimulia kuwa alianza kutumia dawa za kulevya akiwa na umri wa miaka 22 na aliendelea na hali hiyo kwa miaka 17 na alifikia hatua ya kujidunga sindano.

"Nilikuwa nalipwa mshahara halali serikalini kupitia cheo cha konstebo wa polisi, lakini nikaoona kwamba ili nitoke kwa haraka kimaisha, niiingie kwenye utumiaji wa dawa za kulevya huku nikifanya 'dili' mbalimbali za kuniingizia fedha.

"Niliamini dawa za kulevya zingeniwezesha kupata mali za haraka haraka na tamaa hiyo ilinijia baada ya kuona wale waliokuwa wakitumia, walikuwa wanafanya dili nyingi haramu na kupata fedha nyingi.

"Niliamini kwa kutumia dawa za kulevya, nitaonekana mjanja wa mjini na niliamini rahisi ya kujipatia fedha za haraka," Famili anasema.

Anabainisha kuwa kabla ya kutiwa mbaroni na vyombo vya dola kutokana na kujihusisha na dawa za kulevya na matukio ya kihalifu, alilitumikia Jeshi la Polisi kwa miaka sita.

"Nilihitimu mafunzo ya upolisi mwaka 1991, nilipangwa kazi kituo changu cha kwanza cha kazi nakumbuka kilikuwa Kilwa Road, baadaye nilihamishiwa vituo tofauti tofauti na mwishowe nilipelekwa Kituo cha Polisi Msimbazi kule Kariakoo.

"Nikiwa Msimbazi, ndipo nilianza kutumia dawa za kulevya, kipindi hicho maeneo ya Kariakoo yalikuwa yameathiriwa sana kwa kuwa na watu wengi wanaotumia dawa za kulevya na vitendo vya kihalifu.

"Wakati huo nilikuwa ninakaa Kiwalani (wilayani Ilala). Nilianza kidogo kidogo kujifunza na maeneo ambayo nilikuwa nikienda kwa ajili ya kutumia dawa za kulevya ni vijiwe vilivyokuwapo wakati huo katika mitaa ya Livingstone, Sikukuu na Fire.

"Nilipoingia na kujiunga na watu wanaotumia dawa za kulevya, yale niliyokuwa nawaza ya kupata fedha kwa haraka, niliona matunda yake. Kwa kweli, nilifanikiwa kukutana na wauzaji wenyewe na kwa sababu walijua mimi ni polisi, walishirikiana nami na tulipata fedha nyingi kwa njia zisizo halali na wauzaji wakawa marafiki zangu.

"Ilifikia hatua nikawa najihusisha na matukio ya ujambazi, nikawa nakodisha sare za jeshi kwa majambazi, wakifanikiwa kupata fedha, tunagawana. Nakumbuka tabia hii nilianza kuifanya mwaka 1996.

"Hata hivyo fedha walizonipatia ziliishia kwenye starehe tu, nilikuwa napata Sh. 200,000 hadi 400,000 kulingana na tukio walilolifanya, na kwa mwezi wanaweza kufanya matukio mawili au matatu au kusiwe na tukio kabisa," anasema.

## SAFARI YA GEREZANI

Famili anasema mwaka 1997, alijikuta anafungwa jela baada ya kukodisha sare na silaha zake kwa majambazi ambao walikamatwa na Jeshi la Polisi wakati wakifanya uhalifu jijini Dar es Salaam.

"Baada ya kubanwa na kupigwa sana, wale majambazi walinitaja, na wakati wanakamatwa sikuwa na taarifa zozote mpaka nilipofuatwa na askari wenzangu ambao walinikamata na kunipeleka Kituo Kikuu cha Polisi kwa ajili ya gwaride la utambuzi maana tayari nilikuwa nimeshatajwa.

"Kipindi hicho kituo changu cha kazi kilikuwa Kituo cha Polisi Oysterbay. Mbaya zaidi, wale majambazi walipobanwa zaidi, walitaja hadi eneo ninalofanya kazi, na wakati wa gwaride la utambuzi, (majambazi) wote waliohusika kwenye tukio lile walinitaja, nikashtakiwa kijeshi na kuunganishwa nao," anasema.

## APOTEZA MAMA

Famili anaendelea kueleza kuwa kitendo cha kukamatwa, kufukuzwa kazi na kuunganishwa kwenye kesi ya ujambazi kwa kosa la kushirikiana na wahalifu, kilisababisha mama yake mzazi kupata mshtuko uliosababish kufariki dunia.

"Mama yangu alipopata taarifa kuhusu tukio nililolifanya, presha ilipanda na baadaye alifariki dunia wakati mimi tayari nikiwa gerezani. Nakumbuka ilikuwa siku ya nne tangu niingie gerezani ndipo nikapata taarifa mama yangu amefariki dunia.

"Tulihukumiwa kutumikia kifungo cha mwaka mmoja na miezi sita jela kila mmoja. Baada ya kuingia gerezani, sikuweza tena kuendelea na utumiaji wa dawa za kulevya hadi nilipomaliza kifungo changu.

"Nilipata mateso makali, mwili ulikuwa unauma lakini sikuwa na jinsi, niliendelea hivyo hadi nilipomaliza kifungo, baada ya kutoka, sikuweza kuvumilia maumivu yale, niliendelea kutumia unga hadi mwaka 2011," anasema.

## MAISHA BILA UNGA

Famili anasema kutokana na kukosa kazi ya kufanya, maisha yake mtaani yalibadilika, hivyo kuandamwa na msongo wa mawazo wa kukosa ajira na njia pekee ya kuukabili aliona ni kuendelea kutumia dawa za kulevya.

"Wakati mwingine nilikosa fedha za kununua dawa, hivyo nikawa ninapata madhara, wakati mwingine ninaharisha sana, maumivu makali sana ya mwili, lakini sikuwahi kumwibia mtu.

"Kijiwe changu kilichonipa umaarufu Kinondoni na maeneo mengine ya karibu kilikuwa makaburi ya Manyanya. Kwa kweli, nilibadilika, nywele zangu zikawa ndefu na kwa sababu nilikuwa sizichani, zikajisokota nikawa rasta, nikaota ndevu, mwonekano mpya wa sura ukawafanya watu wanibatize jina la Yesu, wakawa wananiita Jesus. Kinondoni yote nikajulikana kama Jesus," anasema.

## AOKOTA MAKOPO

Famili anasema kuwa kutokana na ugumu wa maisha mtaani, aliamua kujihusisha na uokotaji wa chupa za maji zilizotumika na vyuma chakavu ili apate fedha za kununua unga.

"Nilifikia hatua ya kujidunga sindano, hivyo ilikuwa siwezi kupita siku bila kujidunga, ili nipate fedha, niliamua kuokota chupa za maji zilizotumika na vyuma chakavu na kwenda kuuza.

"Ile biashara ya chupa na vyuma chakavu ilinifanya niwe maarufu zaidi kwa sababu nilikuwa natembea kwa miguu kutoka Kinondoni Manyanya hadi Magomeni kutafuta chupa asubuhi na jioni.

"Kila asubuhi nikiamka nikishatumia dawa zangu, safari ya kuokota chupa ilianza na ikifika jioni narudia tena, hayo ndiyo yalikuwa maisha yangu.

"Tofauti na wala unga wenzangu waliojihusisha na vitendo vya wizi, mimi pamoja na hali ngumu ya kifedha, sikuwahi kumpora mtu kitu chake au kuiba mali ya mtu maeneo yote niliyopita," anasema.

## MAISHA BILA DAWA

Famili anasema mwaka 2011, akiwa na wenzake kijiweni kwao makaburi ya Manyanya, walitembelewa na maofisa kutoka taasisi za kupambana na dawa za kulevya ambao waliwapa elimu kuhusu athari za matumizi ya dawa hizo.

Anasema walielezwa kuwa uwezekano wa kupata magonjwa hatari kama vile homa ya ini na kuambukizwa Virusi vya Ukimwi (VVU).

"Hiyo taasisi ilitufikia mara kwa mara kijiweni pale kutoa elimu na kutugawia vifaa mbalimbali ambavyo tunavitumia kujidunga mfano sindano, pamba, maji ya kuchanganyia, lengo lao lilikuwa tusiambukizane magonjwa," anasema.

"Taasisi hiyo ilikuwa ikitutembelea kila baada ya siku tatu na walipokuwa wakirudi, walitaka mrejesho kama vifaa walivyopatia, tumevitumia ipasavyo.

"Baada ya elimu hiyo, niliamua kubailika ndipo walipotaka nitafute mdhamini ambaye ni ndugu wa karibu na baada ya kumpata, nilianza kutumia Methadone (dawa wanazopewa waathirika wa matumizi ya unga) kuanzia mwaka 2011 hadi mwaka 2014 nilipomaliza dozi.

"Wakati naendelea na dozi ya Methadone, mwili wangu ulirudi kwenye hali ya kawaida, nikapata mke ambaye kwa sasa tuna watoto.

"Baada ya kumaliza dozi, nilikutana na Mefada (asasi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na utoaji wa elimu kuhusu athari zitokanazo na dawa za kulevya, Ukimwi na homa ya ini) na waliniajiri hadi leo," anasema.

Famili sasa ni Mratibu wa Mafunzo wa Mefada na anabainisha kuwa katika huduma zao, tangu mwaka 2015, wameweza kufikia watumiaji wa dawa za kulevya 7,489 (wanaume 6,960 na wanawake 529) jijini kuwapa elimu.

Famili anasema maeneo yaliyoathirika zaidi kwa matumizi ya dawa za kulevya jijini ni Msasani, Tegeta, Bunju, Kigamboni na Magomeni Kagera.

## HALI ILIVYO KITAIFA

Taarifa iliyotolewa Juni 25, mwaka huu na Ofisi ya Waziri Mkuu, ilibainisha kuwa mwaka 2015 nchi ilikuwa na waathirika wa dawa za kulevya waliokuwa wakitibiwa kwenye vituo vya tiba 2,400 na kwamba hadi kufikia mwaka jana, kulikuwa na wagonjwa 7,000.

Ilielezwa pia katika taarifa hiyo kuwa maambukizo ya Ukimwi kwa waraibu wa dawa za kulevya wanaojidunga yamepungua kutoka asilimia 35 mwaka 2015 hadi asilimia 18.5 mwaka 2018.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yazindua mpango kazi uendelezaji miji

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imezindua rasmi Mpango Kazi wa Uendelezaji Miji Tanzania ili kuhakikisha nchi inakuwa na miji iliyopangwa na makazi yenye huduma zote za kijamii.

Huo ni utekelezaji wa mpango wa pili wa taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/17-2020/21.

Mpango huo umezinduliwa jijini Dodoma na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mpango kazi huo, Waziri Jafo alisema serikali imejidhatiti kuandaa mipango miji madhubuti ambayo imezingatiwa katika miongozo ya kuandaa mipango ya taifa.

“Serikali inazindua rasmi mpango huo ili kuleta mpangilio mzuri wa miji wenye manufaa kwa taifa na kufanya ukuaji wa miji kuwa mchakato wenye manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa nchi,” alisema Waziri Jafo.

Pia alisema, mpango huo umejikita katika maeneo manne ambayo ni matumizi ya lugha ya mpango kazi, suala la utawala na kanuni, mkakati wa fedha pamoja na kuchunguza njia za kukuza uchumi zitakazochochea ukuaji wake katika viwango vya juu.

Alisema maeneo hayo manne ni muhimu kufanya ukuaji wa miji kuwa mchakato wenye manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa kuwa unatoa mapendekezo ya msingi kwa wakati ambayo ni muhimu kwa upangaji wa maendeleo ya miji nchini.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema ukuaji wa miji ni suala pana ambalo linahitaji wadau wengi kuunganisha juhudi ili kuhakikisha ukuaji wa miji inayosimamiwa kikamilifu.

Dk. Mabula alisema, wizara yake iko tayari kutoa ushirikiano katika kuleta pamoja jitihada za kila taasisi ili kuepuka jambo moja kufanywa na wadau zaidi ya mmoja, lengo likiwa kufanikisha malengo ya nchi iliyojiwekea.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Adolph Ndunguru, alisema mpango huo utasaidia kutatua changamoto za upangaji miji kwa maendeleo ya uchumi na taifa kwa ujumla.

Vilevile Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa kiuchumi na Kijamii, Dk. Tausi Kida, alisema mpango huo utasaidia katika uandaaji wa mipango ya kitaifa ya uendelezaji miji pamoja na sera uliotokana na utafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii uliofanywa kwa kufuata kanuni za kisayansi za ufanyaji tafiti.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akiwa ameanguka baada ya kugongwa na bodaboda (mbele), katika eneo la Kawe, juzi. **PICHA MIRAJI MSALA**

# Hasunga ataka mikakati kuboresha kahawa

**Na Mathias Canal,** SONGWE

SERIKALI imewataka wakulima nchini kupitia vyama vya ushirika kuweka mkakati wa kununua na kutumia mitambo ya kuchakata kahawa ili kuongeza na kuwa na mwendelezo wa ubora na hatimaye kupata bei nzuri sokoni.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa minada ya kahawa kanda ya Mbeya-Songwe.

Pia alizitaka halmashauri kupitia vyanzo vya mapato kuendelea kuwekeza katika uendelezaji wa zao hilo ikiwamo uzalishaji wa miche, ununuzi wa CPU na kuwawezesha wakulima na maofisa ugani kupata mafunzo ya kilimo bora ikiwamo kuwapatia vitendea kazi.

Alisema ili kulinda ubora wa kahawa, matumizi ya mitambo ya kisasa ya kuchakata kahawa (CPU) hayawezi kuepukika.

Kwa mujibu wa Hasunga, nchini kuna takribani mitambo 481 ambayo bado ni michache kulinganisha na kahawa inayozalishwa.

“Nawasihi wadau wote muone umuhimu wa uwapo wa mitambo hii kwa kuwa ili upate kahawa nyingi zenye sifa za ubora unaofanana ni lazima kuwapo na matumizi makubwa ya CPU tena kwa kuzingatia hatua zote za uchakataji wa kahawa,” alisema.

Hasunga aliongeza kuwa lengo la serikali ni kuona kahawa zote zinaandaliwa katika mitambo ya kisasa ili zipate bei nzuri katika masoko pamoja na kuimarisha tija katika uzalishaji.


SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

TANESCO

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KATIZO LA UMEME MKOA WA KAGERA**

Agosti 22, 2019

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linatoa ufafanuzi juu ya katizo la umeme lililotokea Mkoani Kagera kwa siku tatu kuanzia Agosti 19 hadi 21, 2019.

**CHANZO CHA HITILAFU**

Mti wa Caristus kuangukia nguzo za umeme mkubwa (tower no. 77 na 78) nchini Uganda na kukata waya katika njia ya Umeme inayotoka Masaka kuelekea Kagera Tanzania.

**UTATUZI**

Wataalamu na mafundi walifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha huduma ya umeme imerejea, ambapo viongozi waandamizi kutoka Tanzania kutoka Wizara ya Nishati wakiongozwa na Naibu Kamishina, TANESCO wakiongozwa na Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usafirishaji Umeme na walikwenda Masaka nchini Uganda kuhakikisha kazi hiyo inayofanywa na mafundi wa Uganda inakamilika na huduma ya umeme kurejea.

**HISTORIA YA MKOA WA KAGERA KUUNGANISHWA NA NJIA YA UMEME KUTOKA UGANDA**

Miaka ya zamani vyanzo vikuu vya kufua umeme vilikuwa ni Nyumba ya Mungu - Kilimanjaro, Hale - Tanga, Mtera – Dodoma na Kidatu – Morogoro, umeme uliozalishwa katika vyanzo hivyo ulisafirishwa kwenda maeneo mbalimbali ya nchi kupitia miradi kadha ya usafirishaji umeme.

Hata hivyo, hadi kufikia miaka ya 1990 baadhi ya maeneo ya nchi yalikuwa bado hayajaunganishwa na mfumo gridi ya Taifa hii ni kutokana na umbali kuwa mkubwa kutoka kwenye vyanzo vya ufuaji umeme ambapo miradi ya usafirishaji kutokana na umbali huo inakuwa ni ya gharama sana.

Kutokana na kuwa mahitaji ja umeme yalikuwa tayari ni makubwa katika maeneo ambayo hata hayajafikiwa na gridi ya Taifa ililazimu kufanya miradi mbadala kwa ajili ya kufikisha umeme wa uhakika ikibidi kutoka nchi jirani kwa ajili ya Mikoa iliyo mbali na pia pembezoni mwa nchi ikiwemo Mkoa wa Kagera.

Mwaka 1992, Mkoa wa Kagera uliungwa kwenye gridi ya Taifa ya Uganda kupitia njia ya umeme na hivyo njia kuu ya umeme msongo wa 132 kV kutoka Masaka Uganda kwenda Kyaka Tanzania kujengwa.

Mradi huu ulifanywa kwa ushirika baina ya Tanzania na Uganda ambapo kila nchi ilipata ufadhili kutekeleza mradi katika upande wake.

Jitihada za sasa ni kuhakikisha Mikoa yote ya nchi inaungwa katika gridi ya Taifa ya Tanzania, ambapo ni Mikoa minne tu imesalia ikiwemo Kagera, Kigoma, Katavi na Rukwa ambapo miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa kufanikisha hilo.

Baada ya mradi wa Rusumo kukamilika itakuwa hatua mojawapo ya kuunganisha Mkoa wa Kagera na gridi ya Taifa kupitia kituo cha Kyaka, tayari Wilaya za Muleba , Ngara na Biharamulo zikizopo katika Mkoa wa Kagera zimeshaunganishwa na gridi ya Taifa ya Tanzania miaka ya hivi karibuni, jitihada zinaendelea kuhakikisha Mkoa wote wa Kagera unapata umeme kupitia gridi ya Taifa ya Tanzania.

**Kwa mawasiliano**
**kituo cha miito ya simu 2194400 na 0768 985100**
**Facebook https://www.facebook.com/tanescoyetultd/**
**IMETOLEWA NA: OFISI YA UHUSIANO**
**TANESCO MAKAO MAKUU**

215385802

## MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# *Wananchi tahadhari Ukimwi bado tishio*

**TUME** ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) imewataka wananchi kuchukua tahadhari ya maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kutokana na watu 10 kwa saa kila siku kupata maambukizi hayo.

Akizungumza jana katika semina ya Kamati ya kudumu ya Bunge inayoshughulikia Ukimwi, dawa za kulevya na kifua kikuu na kamati ya bunge inayoshughulikia sheria ndogo, Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema katika utafiti uliofanywa mwaka 2016/17 kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilionyesha kiwango hicho cha maambukizi kwa saa.

Alisema kuanzia Januari hadi Desemba walikadiria maambukizi mapya kila mwaka ni watu 72,000, hivyo ni vyema wakachukua tahadhari kujiepusha na hali hiyo na pia kujitokeza kupima ili kujua afya zao.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kwa mwezi ni watu 6,000, kwa siku ni watu zaidi ya 200 na kwa saa ni watu 10 kila siku wanapata maambukizi mapya ya virusi.

Takwimu hizi zinabainisha kuwa hali ya maambukizi ya VVU inatisha, hivyo kinachotakiwa ni kwa jamii kushtuka na kuchukua hatua zaidi za kuepusha tishio hilo kuwa janga zaidi kwa jamii yetu.

Ikumbukwe kwamba mwarobaini dhidi ya maambukizi mapya ya virusi ni kuchukua tahadhari wakati wote, na tahadhari dhidi ya VVU ambavyo husababisha ugonjwa hatari wa Ukimwi inajulikana.

Tunasema hivyo kwa kuwa kila uchao serikali, wadau na wataalamu wa afya wamekuwa wakitoa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali kama semina, mikutano, warsha, makongamano, mijadala pamoja na vyombo vya habari.

Tahadhari ni kuacha vitendo vya zinaa, kutumia mipira wakati wa kufanya tendo la ndoa, kupina afya mara kwa mara ili kuepuka kuambukizana, kwa kutaja baadhi.

Hata hivyo, tunachokiona sisi kuwa kichocheo cha maambukizi mapya ya virusi ni jamii kukaidi ushauri huo utolewao kila uchao wa kuchukua tahadhari wakati wote.

Hili linathibitishwa na kutolewa takwimu zinazoonyesha kupungua kwa maambukizi, lakini baada ya muda fulani maambukizi kuongezeka.

Ushauri wetu kwa jamii ni kuwa ifike mahali ibadilike kwa kuacha uzembe na ukaidi pale inapopewa ushauri na wataalamu wa afya kuhusiana na hatua za kuchukua kuepusha maambukizi mapya ya VVU.

Ukweli huo inatokana na kila mmoja kuwa ameshagusswa na janga la Ukimwi kwa kupoteza ndugu, jamaa, rafiki au jirani.

Tunapaswa kukumbuka kila wakati kuwa hadi sasa Ukimwi hauna tiba wala kinga, hivyo njia pekee ni kijiepusha na maambukizi mapya.

Kujiepisha na maambukizi mapya ni kitu kinachowezekana ikiwa kila mmoja katika nafasi yake atatambua kuwa Ukimwi ni janga la taifa, hivyo kuchukua tahadhari kwa ajili ya kuzuia maambukizi.


Ndiyo maana serikali imekuwa ikitumia rasilimali na kuda kuhakikisha maambukizi ya VVU yanapungua kwa kiwango kikubwa kama si kuisha kabisa, kwa lengo la kuhakikisha kuwa taifa linabaki na rasilimali watu kwa ajili ya kukuza uchumi na maendeleo yake.

Ni matumaini yetu kuwa kila mmoja atatafakari takwimu hizi mpya za TACAIDS ambazo zinatisha, hivyo kuchukua hatua za kujiepusha dhidi ya maambukizi mapya ya VVU.

Kimsingi, kuelezwa kuwa watu 10 kwa saa kila siku wanapata maambukizi hayo, ni jambo ambalo kwa mtu mwenye akili timamu hushtuka na kujitafakari kuhusu hatima ya maisha yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# *Usafi uko wapi kwa wachuuzi hawa?*



Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya vijana na wanawake katika maeneo mbalimbali wanajishughulisha na uchuuzi kama kuuza mitumba, vyakula, vyombo, dawa mbalimbali zikiwamo za mbu ikiwa ni ajira ya kuwapatia kipato.

Hata hivyo, moja ya changamoto inayowasumbua ni baadhi yao kutozingatia usafi wa mazingira kwenye maeneo wanayofanyia biashara na kuhatarisha afya zao.

Kwa mfano jijini Dar es Salaam, wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao wanajisaidia haja ndogo kwenye chupa za plastiki na kuzicha kwenye sehemu zao za biashara.

Wengine wamekuwa wakizitupa kwenye mitaro pembeni ya barabara na viwanjani hali inayoonyesha kwamba wanahitaji kuelimishwa ili kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira kuliko kujiendea kienyeji.

Siku za nyuma wapo waliokuwa waliojisaidia haja kubwa katika mifuko ya plastiki na kuitupa mitaroni, lakini kwa sasa hilo halipo baada ya serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo iliyokuwa ikichangia uchafuzi wa mazingira.

Uchafuzi huo wa mazingira ndiyo uliomwibua Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuwataka wafanyabiashara hao kuzingatia usafi kwenye maeneo yao ya biashara.

Makonda alifikia hatua hiyo na kuweka askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na mgambo, kuwakamata wachafuzi wa mazingira jijini Dar es Salaam ili liendelee kuwa na mandhari safi.

Mjadala huu unatambua kwamba suala la uchafu ni tabia ambayo inakuwa na si rahisi kuiondoa bila kutumia sheria na shinikizo haidhibitiki, lakini wafanyabiashara wakielimishwa na kuzingatia, wanaweza kubadilika na kuzingatia usafi.

Kwa sasa mbali na kujisaidia katika chupa za plastiki, wengine wanapanga bidhaa kwenye mitaro au kuchimba kingo za barabara na kuweka vibanda kwa ajili ya kuweka bidhaa hizo.

Hapo uwezekano ni kwamba kuna uchafuzi na uharibifu wa mazingira, katika hali hiyo wapo wanaofanya hivyo wakijua kuwa ni kosa na wengine hwafahamu uenda hawajui, lakini jambo la msingi ni kuwaelimisha ili waachane na tabia hiyo.

Wakielimishwa wanaweza kufuata na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu kama zilivyoelekeza, ikiwamo kuhakikisha katika maeneo kunakuwa na usafi kwa muda wote ili kulinda afya zao na za wateja.

Wafanyabiashara wadogo kuanzia kwa machinga na mamalishe au babalishe, wana umuhimu wao kwa mahitaji ya watu ya kila siku maeneo ya mijini, lakini ni vyema wazingatie sheria.

Ni kweli baadhi ya maeneo waliotengewa kufanyia biashara, hayana huduma za msingi zikiwamo za maji, vyoo na nyingine nyingi, ndio maana wengine wamekuwa wakivamia hata sehemu zisizo rasmi kwa shughuli zao.

Lakini, ni muhimu wakazingatia usafi na utunzaji wa mazingira kwa kuepuka kujisaidia katika chupa na kutupa haja ndogo ovyo au kufanya uharibifu wowote wa mazingira.

Wakati ambao juhudi zimekuwa zikifanyika za kutafuta maeneo rasmi ya biashara na kuyaboresha, wafanyabiashara nao hawana budi kuzingatia usafi kwa kuepuka kujisaidia na kutupa taka ovyo.

Vilevile ni muhimu mamlaka husika hasa halmashauri kuharakisha ujenzi wa masoko ya wamachinga ili waweze kufanya shughuli zao kwenye maeneo rasmi yenye huduma zote muhimu.

Hatua hiyo inaweza kupunguza mtindo wa kujisaidia haja ndogo katika chupa au kutupa taka ovyo, kwa vile kwenye masoko kutakuwa na huduma zote za vyoo na vizimba vya kuwekea taka.

Mbali na utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wakiwamo mama lishe na baba lishe, njia nyingine ya kupunguza changamoto ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira unaofanywa kwenye maeneo ya biashara.

Ikumbukwe kwamba uchafuzi wa mazingira unaweza kuchangia hata magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu iwapo wahusika hawatazingatia umuhimu wa usafi.

Kwa mfano mtu anajisaidia haja kubwa kwenye mfuko wa plastiki kisha anautupa mtaroni au sehemu yoyote, huo ni uchafuzi wa mazingira ambao mwisho wake ni kusababisha magonjwa ya mlipuko.

Mifuko ya plastiki kwa sasa haipo tena, haijulikani wale waliokuwa na mtindo wa kujisaidia katika mfuko hiyo wanatumia mifuko wana ipo mbadala, lakini jambo la msingi ni kuachana na tabia hiyo.

# Sababu umeme kukatika Kagera

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) limetoa ufafanuzi kuhusu katizo la umeme lililotokea mkoani Kagera kwa muda wa siku tatu mfululizo kuwa lilitokana na hitilafu.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa jana na ofisi ya uhusiano Tanesco, tatizo hilo lilitokea baada ya mti wa caristus kuangukia nguzo za umeme mkubwa (tower no. 77 na 78) nchini Uganda na kukata waya katika njia ya umeme inayotoka Masaka kuelekea Kagera.

Vile vile, tangazo hilo lilifafanua kuwa wataalamu na mafundi walifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha huduma ya umeme imerejea.

"Viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Nishati wakiongozwa na Naibu Kamishna, Tanesco na Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usafirishaji Umeme, walikwenda Masaka nchini Uganda kuhakikisha kazi hiyo inafanywa na mafundi wa nchi hiyo ili huduma irejee," lilisema.

Tangazo hilo lilifafanua kuwa miaka ya nyuma vyanzo vikuu vya kufua umeme vilikuwa ni nyumba ya Mungu-Kilimanjaro, Hale-Tanga, Mtera-Dodoma na Kidatu-Morogoro.

"Umeme uliozalishwa katika vyanzo hivyo ulisafirishwa kwenda maeneo mbalimbali ya nchi kupitia miradi kadhaa ya usafirishaji umeme," tangazo lilifafanua.

Mwaka 1990 baadhi ya maeneo ya nchi yalikuwa bado hayajaunganishwa na mfumo wa gridi ya taifa.

"Hii ni kutokana na umbali kuwa mkubwa kutoka kwenye vyanzo vya ufuaji umeme ambapo miradi ya usafirishaji kutokana na umbali huo inakuwa ni ya gharama.

"Kutokana na kuwa mahitaji ya umeme yalikuwa tayari ni makubwa katika maeneo ambayo hata hayajafikiwa na gridi ya taifa ililazimu kufanya miradi mbadala kwa ajili ya kufikisha umeme wa uhakika ikibidi kutoka nchi jirani kwa ajili ya mikoa iliyo mbali na pia pembezoni mwa nchi ikiwamo Mkoa wa Kagera."

Mwaka 1992, Mkoa wa Kagera uliungwa kwenye gridi ya taifa ya Uganda kupitia njia ya umeme na hivyo njia kuu ya umeme msongo wa 132 kV kutoka Masaka Uganda kwenda Kyaka Tanzania kujengwa.

"Mradi huu ulifanywa kwa ushirika baina ya Tanzania na Uganda na kila nchi ilipata ufadhili kutekeleza mradi katika upande wake.

"Jitihada za sasa ni kuhakikisha mikoa yote ya nchi inaungwa katika gridi ya taifa ya Tanzania."

# Mwanafunzi darasa la 4 akutwa amejinyonga

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWANAFUNZI wa darasa la nne Shule ya Msingi Olsunyai, Elibariki Lekine (12), jijini hapa amekutwa amekufa baada ya kudaiwa kujinyonga kwa kutumia kamba ya katani.

Akithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11:28 jioni katika eneo la mtaa wa FFU, Kata ya Murieti.

Alisema mwili huo ulikutwa kwenye nyumba ambayo ujenzi wake ulikuwa unaendelea, inayomilikiwa na Emmanuel Thomas.

"Mwili wa marehemu ulikutwa umening'inia huku umefungwa kamba ya katani iliyokuwa imefungwa kwenye mbao ya jukwaa lililokuwa linatumika na mafundi ujenzi kwa ajili ya kusimamia," alisema.

Kamanda Shana alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea ili kubaini chanzo cha tukio hilo na mwili wa marehemu umehifadhiwa chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Mkoa ya Mount Meru kwa ajjili ya uchunguzi zaidi.

## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

## TAARIFA KWA UMMA

21 Agosti, 2019

## UWEPO KWENYE SOKO WA DAWA BANDIA YA KAPSULI YENYE JINA 'COLD CAP'

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.
2. TMDA inapenda kuutangazia umma kwamba kupitia mifumo yake ya ukaguzi na ufuatiliaji wa bidhaa katika soko imebaini uwepo wa dawa bandia ya kapsuli yenye jina Cold cap inayoonesha kwenye lebo yake kuwa inatengenezwa nchini India.
3. Dawa hii bandia inatofautiana kwa kiasi kikubwa na dawa halisi aina ya Coldcap inayotengenezwa na kiwanda cha Regal Pharmaceuticals Ltd kilichopo Nairobi nchini Kenya, na ambayo imesajiliwa hapa nchini.
4. Maelezo ya namna ya kutambua dawa bandia hii aina ya Cold cap ni kama inavyoelezwa katika Jedwali hapo chini.

| Na. Maelezo ya dawa bandia aina ya Cold cap | Dawa halisi ya Coldcap iliyosajiliwa |
|---|---|
| **4.1 Muonekano wa kifungashio (box).**<br>i. Muonekeano wa rangi ya bluu iliopauka ambayo imezungukwa na mstari wa rangi nyeupe iliyoitenganisha rangi ya zambarau.<br>ii. Kuna mchoro wa kapsuli ambayo upande mmoja wa capsule hiyo una rangi nyekundu na upande mwingine una madoa doa mekundu. Kapsuli hiyo haina herufi wala maandishi yoyote.<br>iii. Neno 'Cold cap' halijaunganika, ni maneno mawili.<br>iv. Imeandikwa nchi tu ilipotengenezewa, haina jina la mtengenezaji.<br> | i. Muonekeano wake ni wa rangi ya pinki iliyopauka ambayo imezungukwa na rangi ya bluu.<br>ii. Kuna mchoro wa kapsuli ya rangi ya pinki ambayo juu yake ina herufi R iliyondani ya duara na chini ya herufi hiyo kuna maneno yaliyoandikwa kwa rangi nyekundu COLDCAP ORIGINAL.<br>iii. Neno 'Coldcap' limeunganika kama neno moja.<br>iv. Imetengenezwa na kiwanda cha Regal Pharmaceuticals Ltd, Nairobi<br> |
| **4.2 Muonekano wa kapsuli:-**<br>i. Upande mmoja wa kapsuli una rangi ya pinki na upande mwingine hauna rangi.<br>ii. Kapsuli inaonesha dawa iliyo ndani ambayo ni chembechembe za duara za rangi ya njano, nyeupe na pinki.<br> | i. Kapsuli yote ina rangi ya pinki.<br>ii. Kapsuli haionesi dawa iliyo ndani. Hata hivyo dawa ndani ya kapsuli ni unga mweupe.<br> |

5. Kwa taarifa hii wananchi wote ambao wamenunua dawa hizi kutoka kwenye maduka ya dawa wanashauriwa warudishe waliponunua.
6. Wauzaji wa jumla wote ambao wana dawa aina ya Cold cap yenye muonekano wa Cold cap bandia kama ilivyofafanuliwa hapo juu kwenye stoo au maghala yao wanaelekezwa kuacha kuzisambaza na wawasiliane na TMDA ili kupewa utaratibu wa wapi pa kuzipeleka.
7. TMDA inatoa rai kwa wananchi wote kuendelea kutoa taarifa ikiwa watabaini kampuni, kikundi, mitandao au mtu yeyote anayejihusisha na utengenezaji, usambazaji au uuzaji wa dawa bandia ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.

**Imetolewa na:**
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**
**S.L.P 1253, Dodoma Au**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam**
**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751**
**Nukushi: +255 22 2450793**
**Simu bila Malipo: 0800110084**

HABARI KITAIFA

# Ndugai anusa fursa mkutano CPA

INATOKA UK 3

Alisema mkutano huo utajumuisha maspika, manaibu spika, wabunge na mabalozi kutoka nchi wanachama, Maspika wa mabara mengine au kanda na kumekuwa na mwitikio mkubwa sana.

"Mpaka sasa Maspika 20 kutoka nchi wanachama wameshathibitisha ushiriki wao pamoja na wabunge kutoka nchi hizo na wafanyakazi, wameonesha nia kubwa ya kushiriki hasa ikizingatiwa unafanyika kwenye mji wa kitalii,"alisema.

Fursa za CPA

Ndugai alisema pamoja na mkutano huo huwa wa kubadilishana uzoefu, lakini pia Tanzania itashawishi kuridhiwa kwa sehemu ya fedha za CPA kuwekeza katika ujenzi wa hoteli ya nyota tano jijini Dodoma ambayo kiwanja kimeshapatikana.

"Tanzania ndio makao makuu ya CPA, kwa kuwa tuna kamfuko ketu ambako nchi wanachama huchangia, kapo kamenona kidogo na sisi Tanzania ndio tunatunza kwa fedha za kigeni, hivyo tutashawishi wenzetu wakubali sehemu fulani ya fedha hizo kuwekeza Dodoma," alisema.

Alifafanua uwekezaji huo ni wakujenga hoteli hiyo ambayo itakuwa ni mali ya CPA na kiwanja kipo kikubwa jirani ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) na michakato mbalimbali imeshafanyika na mkutano huo ndio unatarajiwa kuridhia.

"Hivyo tutashawishi ili fedha hizo zibaki nchini kwetu kwa kuwekeza ili kujenga jiji la Dodoma, tutajenga hoteli ya kisasa kabisa," alisema.

Aliongeza: "Kama mnavyojua wanapokuja mabalozi na viongozi wazito Dodoma tunapata tabu sana jinsi ya kuwa accommodate (kuwahudumia) kuna wakati tulitembelewa na Rais wa Benki ya UDP ilikuwa shida tuliwaza tutamuweka wapi, tulitumia maarifa mengi sana, hivyo kuna haja ya kuwa na hoteli kubwa zenye hadhi hiyo."

Kadhalika, alisema upo utalii wa aina mbalimbali na mkutano huo unatarajiwa kuingizia nchi mapato kwa maana ya fedha za kigeni kutokana na huduma mbalimbali.

"Pia wafanyabiashara ambao ni wamiliki wa hoteli, wauza vyakula, wenye magari ya kukodi taxi na wauzaji wa vitu mbalimbali pia watapata fursa nzuri ya kufanya biashara zao," alisema.

Spika alisema faida nyingine ni kutangaza vivutio vya nchi na kwamba ni heshima kubwa kwa Tanzania na Bunge iliyopewa jukumu la kuratibu mkutano huo.

"Naomba kuwashauri wafanyabiashara na Watanzania kutumia fursa hizi tunazopata za kuaminiwa na mataifa mbalimbali, ni adhimu mataifa mengine wanazililia na hii tumshukuru Rais John Magufuli ambaye ameendelea kuipatia heshima nchi yetu," alisema.

Katibu wa Bunge ambaye pia ni Katibu wa CPA, Stephen Kagaigai, alisema mkutano huo utahudumiwa kwa viwango kama Mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Makao makuu ya chama yapo Tanzania hapa bungeni, tumefanya maandalizi ya kutosha hadi sasa kuwapokea wageni na tunatarajia wageni kati ya 400-500 wataingia kuanzia Agosti 28, mwaka huu," alisema.

# Mawakili kesi ya Mbowe chupuchupu kukamatwa

INATOKA UK 3

"Askari sogeeni hapa karibu yangu naweza kutoa amri wakati wowote muwakamate mawakili hawa wanabishana kienyeji bila kuiheshimu mahakama na kufuata utaratibu wa kisheria," alisema Hakimu Simba kwa jazba, huku askari akiwa amesimama karibu yake kwa ukakamavu.

Nchimbi alidai kuwa kitendo cha mawakili wa utetezi kinasababisha kumtoa shahidi nje ya mwelekeo wa kesi ya Jamhuri.

Hata hivyo, Wakili Mwasipu alisimama kuiomba radhi mahakama na mahakama hiyo ilirídhia.

Shahidi alidai kuwa Januari 30, mwaka jana, Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni aliitisha mkutano wa wadau wa uchaguzi mdogo wa jimbo hilo ikiwamo wa vyama 11 vya siasa.

Alidai kuwa agenda kubwa ya mkutano huo ilikuwa kupanga uapishaji mawakala wa wagombea na utaratibu wa uchaguzi wa Februari 17, 2018.

Alidai kuwa mawakala wa vyama vyote waliapishwa Februari 10, 2018 na kwamba walitambulishwa kwa wasimamizi wa uchaguzi Februari 17,2018 asubuhi kabla upigaji kura haujaanza.

Alidai kuwa kabla ya kuwaapisha mawakala hao, msimamizi wa uchaguzi aliwaandikia barua wadau wote wa uchaguzi huo vikiwamo vyama vya CCK, CUF, ASP, UMD, DP, TLP, Chadema, CCM na Demokrasia Makini kuwasilisha majina ya mawakala siku saba kabla ya uchaguzi.

Februari 16, alidai kuwa walijitokeza Ester Matiko na Suzan Lyimo ofisini kwake kwenda kudai kiapo cha utii badala ya barua ya utambulisho wa mawakala.

Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori.

Upande wa utetezi uliongozwa na Peter Kibatala, Jeremia Mtobesya, Hekima Mwasipu na Fredy Kiwelo.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Awali Koplo Charles akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kuandika taarifa kwenye mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video na ilipofika saa 10 alasiri, alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

Alisema alipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika, baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani alimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali.

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari polisi kunusuru kamera," alidai Koplo Charles.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawakuwapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, Bulaya alishawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Pia ilidaiwa kuwa siku hiyo, katika barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni, Kinondoni, kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa Jeshi la Polisi, Gerald Ngiichi, na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.


TAARIFA KWA UMMA



Frank Tarkisio Kisinini

Mtajwa hapo juu sio mfanyakazi wa Ndumi Finance tangu tarehe 24/06/2019. Pia, **Frank Tarkisio Kisinini** hajawahi kuajiriwa na GGBM Investments (T) Ltd,hivyo kampuni haitajihusisha na chochote atakachokifanya kuanzia tarehe tajwa hapo juu.

21583702


# Mahakama yakataa kupokea nyaraka

INATOKA UK 3

Simba, alikubaliana na hoja za utetezi na kukataa kupokea kielelezo hicho.

Shahidi alidai katika uchunguzi alibaini viongozi wa klabu wa Simba walipeleka TRA nyaraka ikionyesha nyasi walinunua kwa zaidi ya Dola za Marekani 40,000, lakini alipohoji aliambiwa walinunua kwa Dola za Marekani 109,000.

Alidai viongozi hao walipotakiwa kupeleka nyaraka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili wapate msahama wa tozo ya ukaguzi wa mzigo walipeleka nyaraka ya Dola za Marekani zaidi ya 40,000.

Shahidi alidai mzigo huo haukufanyiwa ukaguzi China hivyo walitakiwa kulipa gharama, lakini kutokana na barua waliyoandika walisamehewa.

Alidai aliitaarifu TRA kuhusu nyaraka hizo. Baada ya kudai hayo aliomba kutoa nyaraka hizo kama kielelezo mahakamani, lakini mawakili wa utetezi walipinga wakidai hana mamlaka ya kutoa kielelezo hicho.

Mahakama iliamuru kutoa uamuzi Agosti 28, mwaka huu, kesi iliahirishwa na washtakiwa walirudi rumande.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka la 10 ikiwamo kula njama, kughushi, kuwasilisha nyaraka za kughushi, kutoa maelezo ya uongo na utakatishaji wa fedha.

# Miradi mikubwa iwaongezee ujuzi

Na Beatrice Moses

SERIKALI imeshauriwa kuwekeza katika miradi mikubwa ya ujenzi wa reli ya kisasa na flyover inayotekelezwa nchini kwa kuhakikisha inatumika kuwaongezea ujuzi wahandisi wazawa na wanafunzi wa fani za ujenzi.

Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Wahandisi, Ipyana Moses, alitoa ushauri huo jana alipozungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya kutembelea taasisi ya Dar es Salaam Institute of Technology (DIT), mwishoni mwa wiki. Moses alisema taasisi yao imebaini ushiriki mdogo wa wahandisi wazawa kwenye miradi hiyo, hivyo wamewasiliana na serikali na kuishauri kuona jinsi inavyoweza kubadilisha sera kwenye mikataba ya awali ili kubainisha nafasi za wahandisi Watanzania.

Alisema taasisi yao ina jukumu la kuwaunganisha wahandisi wote nchini wanajifunza na kushauri cha kufanya ili kumudu kwenye soko, pia kutimiza lengo la kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda.

Akizungumzia ziara hiyo alisema ni sehemu ya utaratibu wa kutembelea shule za sekondari kuhamasisha wananafunzi kupenda masomo ya sayansi, pia kutembelea taasisi zinazotoa mafunzo ya sayansi na uhandisi ili kushauri na kuboresha maeneo ambayo wanabaini kuna udhaifu, hatua ambayo inalenga kuhakikisha wanaohitimu masomo hayo wanakuwa bora.

Mhandisi mshauri wa masuala ya ujenzi wa nyumba na barabara, Erasto Machume, alisema wataalam wa ujenzi wa barabara wao tatizo ni vitendea kazi na uzoefu katika baadhi ya miradi, kwa Tanzania Fly Over ya kwanza ni Mfugale.

Mratibu wa ziara hiyo, Dk. John Msuma, alisema hawawezi kuwa na mafanikio bila kuwa na ushirikiano mzuri na wadau, kama taasisi hiyo ambayo tayari ina wahandisi waliopo kwenye soko, hivyo wanatambua zaidi mahitaji yalivyo.

# Shahidi aeleza alivyokimbia vurugu kuhofia usalama wake

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeambiwa na shahidi katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, kwamba kutokana na ghasia na vurugu, alishindwa kuendelea kurekodi picha za video.

Shahidi huyo wa sita wa Jamhuri, Koplo Charles, alidai maneno yaliyozungumzwa na viongozi wa Chadema yalisababisha hamasa na kwamba ilikuwa hatari kwa maisha yake na vitendea kazi ikiwamo kamera.

Koplo Charles alitoa madai hayo juzi katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, wakati akihojiwa na Jamhuri.

Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori, alimhoji shahidi kuhusu majibu aliyoyatoa kwa utetezi kwamba hakuwaona washtakiwa na wafuasi wao wakiwa na silaha.

Shahidi alidai kuwa hakuwaona kwa sababu kazi yake ya kupiga picha iliishia viwanja vya Buibui na kwamba hakuwahi kwenda kwenye maandamano kwa sababu alikimbia na gari la polisi kunusuru usalama wake na kamera.

Aidha, alidai kuwa kuhusu picha na sauti za washtakiwa zilizosikika kwenye video, alikiri ni za washtakiwa hao kwa sababu anawafahamu kabla ya siku ya mkutano huo.

Alidai kuwa jukumu lake siku ya tukio lilikuwa kupiga picha za mkutano wa kufunga kampeni katika viwanja vya Buibui na kwamba hakuna picha iliyohaririwa kwa sababu alikuwa akirekodi kwa awamu tofauti.

Shahidi wa nane, Ofisa Uchaguzi Wilaya ya Kinondoni, Victoria Wihenge (30), alidai kuwa Januari mwaka jana aliitisha mkutano wa wajumbe wakiwamo wadau wa siasa ngazi ya Mwenyekiti na Katibu wa Wilaya.

Hata hivyo, shahidi ataendelea leo kutoa ushahidi wa Jamhuri.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na mawakili wa serikali wakuu, Faraja Nchimbi, Dk. Zainabu Mango, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Jaqline Nyantori.

Upande wa utetezi uliongozwa na Peter Kibatala, Jeremia Mtobesya, Hekima Mwasipu na Fredy Kiwelo.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Awali Koplo Charles akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kuandika taarifa kwenye mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video na ilipofika saa 10 alasiri, alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

Alisema alipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika, baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani alimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali.

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari la polisi kunusuru kamera," alidai Koplo Charles.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawakuwapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko usiyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, Bulaya alishawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu. Pia ilidaiwa kuwa siku hiyo, katika barabara ya Kawawa eneo la Mkwajuni, Kinondoni, kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa Jeshi la Polisi, Gerald Ngiichi, na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui, kwenye mkutano wa hadhara, Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano... watu wanapotea, watu wanauawa, wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome."

Maneno hayo yanadaiwa yalikuwa na mwelekeo wa kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.

Washtakiwa wote waliposomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.



Mchuuzi wa kofia akisaka wateja katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, eneo la Oysterbay, jijini Dar es Salaam jana. Kofia moja inauzwa 5,000/- hadi 15,000/- kulingana na ubora wake. **PICHA: JOHN BADI**.

## Solwa kunufaika majisafi kutoka Ziwa Victoria

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANANCHI wa Jimbo la Solwa, Shinyanga Vijijini, wanatarajia kunufaika na majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria na kuondokana na adha ya kutumia maji yasiyo salama.

Hayo yalibainishwa juzi na Mbunge wa jimbo hilo, Ahmed Salum, wakati akisoma taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM kuanzia mwaka 2016-19, kwenye ziara ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ya kukagua utekelezaji wa Ilani hiyo.

Alisema kwenye jimbo hilo kuna jumla ya vijiji 126 kati ya hivyo 93 vinapata huduma ya majisafi na salama, vikiwamo vilivyopitiwa na mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, huku vijiji vingine vilivyobaki vinatarajiwa mwakani (2020) kutumia majisafi.

"Sasa hivi kuna mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria ambao upo Kata ya Masengwa, una hatua nne hadi kukamilika kwake na ukishakamilika tu mwakani (2020) utanufaisha pia jumla ya vijiji 14 ambavyo vitapitiwa na bomba hilo na hatimaye kuondokana na adha ya matumizi ya maji machafu," alisema Salum.

Pia alisema suala la umeme wa REA awamu ya kwanza, vijiji 35 vimeshawekewa nishati hiyo na awamu ya pili vitawekewa vijiji 50 na hadi kufikia mwakani asilimia 90 ya vijiji vyote jimboni humo vitakuwa na umeme.

Naye Balozi Iddi ambaye pia ni mlezi wa CCM Mkoa wa Shinyanga, aliwatoa wasiwasi wananchi wa jimbo hilo kuwa suala matumizi ya maji machafu jimboni humo litabaki kuwa historia, kwa kuwa serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria.

Alisema uwapo wa maji ya kutosha pamoja na nishati ya umeme katika maeneo mbalimbali nchini, kutaifanya Tanzania kufikia malengo ya sera ya uchumi wa viwanda, kwa kuwa bila ya kuwapo na huduma hizo muhimu sera hiyo haitaweza kufanikiwa.

Katika hatua nyingine Balozi Iddi aliwataka Watanzania katika kuelekea kwenye kipindi cha uchaguzi wasiwachague viongozi wasio na sifa, wapende maendeleo hasa kutoka CCM, ili kuwapo na muunganiko wa uongozi kutoka chama kimoja na kuwatatulia changamoto zao.

# Masasi yafanikisha miradi kwa mfuko wa jimbo

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MBUNGE wa Jimbo la Ndanda, Cecil Mwambe, ameipongeza Halmashauri ya Masasi Vijijini kwa utekelezaji makini wa miradi ya maendeleo kupitia fedha za mfuko wa jimbo kwa kufikisha asilimia 94.92 kwa matumizi ya Sh. milioni 74.66 na kuleta tija kwa wananchi wa jimbo hilo.

Pongezi hizo alizitoa jana katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichoketi katika ukumbi wa halmashauri hiyo na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa.

Mwambe alisema kutokana na watendaji wa halmashauri hiyo kwa kushirikiana na Mkurugenzi wao, Changwa Mkwazu, kusimamia vema fedha zinazotolewa na mfuko huo Jimbo la Ndanda, imeleta tija kwa jamii kama ilivyokusudiwa.

Alisema kuwa kila ulikopelekwa mradi ambao fedha zake zimetokana na fedha za mfuko wa jimbo mradi umetekelezwa kikamilifu na hata thamani ya fedha imeonekana.

Mwambe alisema fedha hizo za mfuko wa jimbo zimesaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa, ofisi za vijiji, zahanati na ujenzi wa soko la Ndanda na kwamba miradi yote hiyo imekamilika kikamilifu na inalingana na thamani ya fedha zilizotumika. "Matokeo haya mazuri ya utekelezaji wa miradi kikamilifu yametokana na uadilifu wa watendaji na mkurugenzi katika halmashauri hiyo, hivyo ushirikiano huo uendelee daima ili miradi inayotekelezwa na fedha za mfuko wa jimbo ilete tija kwa walengwa," alisema Mwambe.

Alisema halmashauri isibweteke na miradi hiyo badala yake ichukue hatua za kukamilisha ujenzi wa zahanati iliyoanza kujengwa ya Nanda na ambayo inajengwa pia kwa fedha za mfuko wa jimbo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, amelipongeza Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kwa kukaa na kupokea na kujadili taarifa za kufunga mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mzee alisema uadilifu unaonyeshwa na watendaji hao wa halmashauri katika kutekeleza miradi ya maendeleo, utasaidia kuifikisha Masasi katika kilele chanya cha maendeleo kwa wananchi wake na kupunguza changamoto zilizopo za huduma za kijamii.

# Tamasha la jinsia kuwakutanisha wanawake 1,500 Dar Septemba

**Na Yasmine Protace**

WANAWAKE zaidi ya 1,500, kutoka Tanzania na nje ya nchi, wanatarajia kushiriki tamasha kubwa la kisasa la 14 lililoandaliwa na TGNP Mtandao, ambalo linatarajia kufanyika mwezi ujao jijini Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa na Ofisa Habari wa TGNP Mtandao, Monica John, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

"Tamasha hilo litaanza Septemba 23 hadi Septemba 27, ambapo washiriki kutoka ndani ya nchi na nje ya nchi, wamethibitisha kushiriki," alisema.

Aliongeza kuwa tamasha hilo litawakutanisha wanawake kutoka mikoa mbalimbali ya nchini na nje ya nchi, ambapo watapaza sauti zao kwa ajili ya masuala ya wanawake.

Alisema tamasha hilo linaimarisha ujenzi wa nguvu za wanawake katika umoja wao na kupaza sauti zao.

Aliongeza kuwa kutokana na umuhimu wa tamasha hilo, watakapokutana watabadilishana mawazo na uzoefu.

"Washiriki wataonyesha maonyesho mbalimbali na watapata fursa kuelekea Tanzania ya viwanda," alisema.

Aliongeza kuwa watatafakari na kupeana taarifa na kupeana taarifa kuhusu maazimio ya mkutano wa nne wa dunia wa wanawake uliofanyika Beijing, China mwaka 1995 pamoja na kuzitambua nyanja mbalimbali.

Aliongeza kuwa baadhi ya mada kuu ni harakati za wanawake zinavyoweza kuleta mabadiliko.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, aliongeza kuwa miaka 25 ya TGNP Mtandao ni ukombozi kwa wanawake.

Alisema kuwa katika tamasha hilo kutakuwa na masuala ya Beijin na kufanya mikakati ya pamoja ili kuona wapi walipo na wanakokwenda.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mwalimu Commercial Bank Plc, Herman Kessy, akifungua mkutano mkuu wa tatu wa mwaka wa benki hiyo, uliofanyika mkoani Mtwara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge laibana benki utata malipo nembo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeagiza Benki ya Posta (TPB) kuwasilisha mikataba ya utengenezaji nembo na ukarabati wa nyumba ilizopanga baada ya kubaini utata katika malipo yake.

Hatua hiyo ya kamati imetokana na kutoridhishwa na majibu yaliyotolewa na uongozi wa benki hiyo, ilipoitwa mbele ya kamati hiyo.

Akitoa maagizo hayo jana wakati wa kupitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alisema majibu yaliyotolewa kuhusu utengenezaji wa nembo bado yana utata kutokana na kubadilishwa mtengenezaji baada ya wa awali kupatiwa fedha.

Alisema mkataba wa kwanza walioingia ulikuwa wa Sh. milioni 247 na baada ya miezi miwili ulifutwa wakidai amechelewa kufanya kazi hiyo na kuingia mkataba wa pili na mtu mwingine wa Sh. milioni 495.75.

"CAG mwenyewe pia amehoji imekuwaje waache mtu wa Sh. milioni 247 wachukue wa Sh. milioni 495, ndiyo maana tumeagiza hiyo mikataba tuipitie tuone kama huyo mtu alikiuka, wamemchukulia hatua gani na kwanini wakachukua wa kiwango kikubwa," alisema.

Kuhusu ukarabati wa nyumba ambazo benki hiyo imezihodhi zilizokuwa zikimilikiwa na Benki ya Twiga na Benki ya Wanawake, Kaboyoka alisema zaidi ya Sh. bilioni 1.7 zimetumika kukarabati nyumba hizo ambazo hazimilikiwi na benki hiyo.

"Matengenezo ya nyumba yametumika zaidi ya Sh. bilioni 1.7 na ndiyo tumewaambia nyumba siyo zenu, mmetumiaje kiasi hicho chote cha fedha wakati ni nyumba za kukodisha?" Kaboyoka alisema.

"Kwa hiyo tujue kodi wanalipa kiasi gani ili wao waweze kutengeneza nyumba hizo na kwanini wakodi nyumba ambazo hazifai?"

Mwenyekiti huyo alisema Benki hiyo inatakiwa kuhakikisha ifikapo Novemba mwaka huu iwe imewasilisha ripoti yenye majibu ya hoja hizo.

Kaboyoka alisema kamati kwa kiasi kikubwa wanaangalia mashirika ya umma yenye hisa kubwa kwa serikali ili yafanye kazi kwa ufanisi.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanafuata sheria ya manunuzi ya umma yaliyowekwa ili yaweze kufanya vizuri hivyo kuongeza mapato kwa serikali.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya TPB, Dk. Edmund Mndolwa, alisema benki hiyo imeamua kuwalipa wanahisa wa Benki ya Wanawake (TWB) mtaji wao wote walioweka kwenye benki hiyo.

Aliwahakikishia wanahisa hao kuwa watalipwa fedha zao zote, akieleza kuwa uamuzi huo ulifanyika Desemba mwaka jana.

# Mwenge kuzindua miradi 39 yenye thamani ya bil.16/-

**Na Tiganya, Vincent**

JUMLA ya miradi 39 yenye thamani ya Sh. bilioni 16.9 inatarajiwa kuzinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru mkoani Tabora.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, Mwenge huo unatarajia kuanza mbio zake Jumatatu na kumaliza mbio zake Septemba 2, mwaka huu.

Alisema Mwenge wa Uhuru utapokelewa mkoani Tabora ukitokea Singida ambapo utakimbizwa katika halmashauri nane za mkoa huo.

Mwanri alisema Mwenge utaanzia Igunga, Nzega Mji, Nzega Wilaya, Uyui, Kaliua, Urambo, Tabora Manispaa na kumalizia mbio zake katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kabla ya kukabidhiwa mkoani Mbeya.

Aliongeza kuwa katika kila halmashauri mkoani Tabora, Mwenge wa Uhuru utaweka mawe ya msingi, kufungua na kuzindua miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali za umma na binafsi.

Mwanri alisema kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru mwaka huu; maji ni haki ya kila mtu tutunze vyanzo vyake na tukumbuke kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema kuwa kauli mbiu inaambatana na ujumbe usemao pima, jitambue, ishi, nipo tayari kutokomeza malaria, wewe je? Kataa rushwa, jenga Tanzania, tujenge maisha yetu, jamii yetu na uhuru wetu bila dawa za kulevya.

Mwanri alisema mbio za Mwenge wa Uhuru zitaambatana na maonyesho ya shughuli mbalimbali za ujasiriamali kutoka katika vikundi mbalimbali vya kiuchumi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Aidha, alisema kutakuwa na maonyesho ya shughuli zinazofanywa na sekta mbalimbali za afya, maji na maelezo ya jinsi ya kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 2019.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema katika kila halmashauri kutafanyika mikesha itayohusisha shughuli za upimaji wa virusi vya Ukimwi, malaria na magonjwa mengine usiku mzima.

Alitoa wito kwa wananchi wote mnaombwa kushiriki kikamilifu kwa kujitokeza maeneo yote Mwenge wa Uhuru utakakopita na kuushangilia kwani ni alama muhimu inayowakilisha Watanzania wote.

# Wamiliki 163 Tanzanite wabanwa TRA

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WAMILIKI 163 wa migodi walioajiri wachimbaji 4,500 wa madini ya Tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wameandikiwa barua na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwataka kuwalipia kodi ya mapato na ya ufundi wachimbaji hao.

Meneja wa TRA mkoani Manyara, John Mwigura, alisema kati ya wamiliki hao 163, ni 31 pekee waliopeleka taarifa za wafanyakazi walio nao na namna wanavyofanya shughuli zao migodini.

"Migodi ya dhahabu kule Geita wanalipa kodi ya ajira kwa wachimbaji wao na tozo ya ufundi, hivyo wachimbaji wa Tanzanite nao wanapaswa kulipa kama wamiliki wa maeneo mengine wanavyofanya," alisema Mwigura.

Alisema kila wakizungumza na wamiliki hao juu ya kuwalipia kodi ya ajira na tozo ya ufundi kwa wafanyakazi wao, wamekuwa wakitoa sababu tatu kwa TRA ambazo wanadai hawastahili kuzilipa.

Kwa mujibu wa meneja huyo, sababu ya kwanza wanadai hawajaajiri kwenye migodi, sababu ya pili wameajiri ila hawalipi mishahara na ya tatu hawajapata madini, hivyo hawawezi kulipa chochote.

Alisema waliwaeleza kuwa wanapaswa kuwapa taarifa za mrejesho wa wanavyofanyia kazi na uzalishaji kila mwezi, lakini hawafanyi, hivyo wanapeleka kwenye ofisi za tume ya madini.

"Kati ya wamiliki hao 163 wa migodi ni wamiliki 31 pekee walioleta taarifa zao za uchimbaji kwa kila mwezi ila baada ya kuona wamiliki wenzao hawaleti nao wakaacha kutuletea ndipo tukaamua kuwapa taarifa wote," alisema Mwigura.

Alisema endapo wamiliki hao wasipolipia kwa hiyari, watawafikisha mahakamani baada ya kukutana nao Mirerani na kuzungumza nao juu ya malipo hayo kuanzia miaka mitatu iliyopita.

"Timu ya TRA mkoani Manyara itakuwa Mirerani kwa muda wa siku tano kuanzia Agosti 19 hadi 23 kwa ajili ya kuzungumza na wamiliki hao wa migodi juu ya kodi ya ajira na tozo ya ufundi," alisema Mwigura.

Alisema wanafanya hayo kupitia sheria ya madini, sheria ya kazi inayowataka wawe na mikataba ya kazi na sheria ya kodi ya mfumo wa kujikadiria kulingana na wafanyakazi walio nao.

"Tumeshakaa vikao vinne tukitoa elimu ya kutosha juu ya hilo ikiwamo mbele ya Mkuu wa Mkoa Alexander Mnyeti, Mkuu wa Wilaya, Zephania Chaula na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya, Yefred Myenzi na mihutasari ipo," alisema Mwigura.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, akizindua mradi wa maji Kijiji cha Endamilay uliowezeshwa na Norwegian Church Aid kwa kusimamiwa na kituo cha Pembe Nne za Utamaduni Haydom (4CCP) jana. **PICHA: GIFT THADEY.**

## Simanjiro kicheko nyongeza ya shule

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WILAYA ya Simanjiro mkoani Manyara iliyokuwa na shule moja pekee ya sekondari ya kidato cha tano na sita, hatimaye imepata nyingine, hivyo kufikisha shule mbili.

Mjumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa Halmashauri, Sendeu Laizer, aliyasema hayo juzi wakati akielezea umaliziaji wa shule hiyo.

Laizer alisema baada ya Shule ya Sekondari Emboreet kuwa ya kidato cha tano na sita hivi sasa Shule ya Sekondari Simanjiro nayo imefikia hatua hiyo hivyo kuwa na shule mbili zenye hadhi hiyo.

"Shule hii ya Simanjiro ipo kwenye Kata ya Orkesumet na itakuwa na mikondo miwili na tunawapongeza wote waliofanikisha shughuli yote hadi kukamilika kwake," alisema.

Diwani wa Ngorika, Albert Msole, alisema hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa itasababisha kiwango cha elimu kwenye eneo hilo kupanda zaidi tofauti na mwanzo.

"Kwa mujibu wa sera ya elimu na ilani ya uchaguzi ya CCM, kila tarafa inapaswa kuwa na shule moja ya sekondari ya kidato cha tano hadi cha sita. Sisi Simanjiro tumepata mbili nadhani tunaendelea vizuri kutekeleza hilo," alisema Msole.

Alisema juhudi zinapaswa kuongezwa ili shule nyingine ikiwamo za Mirerani, Ngorika, Terrat na Naisinyai ziboreshwe na kuwa na hadhi ya kidato cha tano na cha sita.

Mkazi wa Mji Mdogo wa Orkesumet, Julius Lazaro, alisema hivi sasa Simanjiro inazidi kupiga hatua kubwa kwenye suala zima la maendeleo tofauti na hapo awali.

Lazaro alisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli na Mbunge James Ole Millya kwa miaka minne waliokuwa madarakani wamefanya maendeleo makubwa mno.

"Mwaka 2015 kulikuwa hakuna hata kipande cha lami, hakukuwa na hata sekondari ya kidato cha sita, hakukuwa na mahakama ya wilaya na sasa hospitali ya wilaya imejengwa," alisema.

# Wakili aomba kukamilishwa upelelezi kesi OBC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKILI wa utetezi Daudi Haraka, ameomba kukamilishwa kwa upelelezi wa kesi inayomkabili Mkurugenzi wa Kampuni ya Uwindaji ya Oterlo Businness Corporation (OBC), Isack Lesian Mollel (59), na wenzake 10.

Alitoa ombi hilo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Niku Mwakatobe, anayesikiliza kesi mbili za Mollel anayekabiliwa na mashtaka 37 yakiwamo ya kuajiri raia wa kigeni kinyume cha sheria za nchi na uhujumu uchumi.

Haraka alidai kuwa kesi hizo za mashtaka ya uhujumu uchumi hazijawekwa kikomo cha muda wa upelelezi, lakini anaomba upande wa Jamuhuri uharakishe upelelezi ili kuanza kusikilizwa kesi.

Pia kwa upande wa kesi ya Mollel na wenzake 10 waliokutwa wanafanya kazi nchini kinyume cha sheria za kazi, Haraka aliomba upande wa Jamuhuri uache kuja na sababu zingine kwa kuwa tarehe ya kesi hiyo iliyopangwa Septemba 2, mwaka huu, ili isomwe maelezo ya awali.

"Naomba Mheshimiwa Hakimu uwaeleze hawa wenzetu wa Jamuhuri, siku hiyo wasije na sababu zingine tena ili tusikilize maelezo ya awali na ikiwezekana waje na mashahidi ianze kusikilizwa. Tangu upelelezi ukamilike leo (jana) ni mara ya nne wanakuja na sababu na kesi inapigwa tarehe," alidai.

Kabla ya Hakimu Niku kuzungumza, Wakili wa Serikali, Naomi Mollel, akisaidiana na Godluck Peter, aliomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine kwa sababu upelelezi haujakamilika. Katika kesi ya wafanyakazi 10, pia aliomba tarehe nyingine kwa madai kwamba wakili wa kesi hiyo amekwenda kwenye mafunzo Dar es Salaam.

Hakimu Mwakatobe alisema anakubaliana na wakili wa utetezi kuwa kesi hiyo ya wafanyakazi 10 na Mollel, upelelezi wake ulishakamilika siku nyingi, hivyo aliagiza upande wa Jamuhuri kusoma maelezo ya awali Septemba 2 na siku hiyo hiyo waje na mashahidi ianze kusikilizwa.

Kuhusu kesi ya uhujumu uchumi, aliipanga Septemba 4 kwa ajili ya kutajwa na kuamuru mshtakiwa kuendelea kukaa rumande.

Washtakiwa katika kesi ya kufanya kazi nchini kinyume cha sheria inawakabili Mollel ambaye ni mshtakiwa wa kwanza kutokana na kuajiri raia wa kigeni, Darweshi Jumma, Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, Martin Crasta, Imtiaz Feyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali.

Kabla ya kusomewa mashtaka hayo, Mollel alifutiwa kesi namba moja ya mwaka huu, iliyokuwa inamkabili ya kuajiri raia 10 wa kigeni kinyume cha sheria za ajira na kuunganishwa kwenye kesi namba 74 ya mwaka huu, inayowahusu washtakiwa hao waliokamatwa Loliondo kwa tuhuma za kufanya kazi bila vibali.

# Aswekwa lupango kwa kusema uongo

**Na Mary Mosha,** SIHA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza kukamatwa na kuwekwa mahabusu Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbise Construction Limited, Arnold Mwasumbi, kutokana na kutoa maelezo ya uongo juu ya mradi wa maji unaotekelezwa katika kijiji cha Munge, Kata ya Donyomoruwa.

Mradi huo unaotekelezwa kwa fedha za serikali ya Tanzania, utagharimu zaidi ya Sh. milioni 750 hadi kukamilika kwake.

Mbise aliingia matatani jana baada ya Naibu Waziri huyo kufanya ziara ya kushtukiza katika eneo la mradi huo na kujikuta akimdanganya katika taarifa ya maendeleo ya mradi.

Kwa mujibu wa Aweso, amelazimika kumweka ndani mkurugenzi huyo kutokana na kutoa maelezo ya uongo, licha ya mradi huo kutokamilika huku tayari akiwa amelipwa fedha kwa asilimia 100.

"Mkandarasi huyu licha ya kulipwa kwa asilimia 100 bado ametumia muda wa miezi tisa kuchimba mitaro wenye urefu wa kilomita 18. Hatutamwongezea muda na sijaridhishwa na kasi anayoendelea nayo kwani lengo la Rais John Magufuli ni kumtua mama ndoo kichwani. Sisi hatutamvumilia mtu yeyote atakayekwamisha hili.

"OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) mkamateni huyu maana anapotosha umma kwa uongo na pia ananidanganya na mimi. Isitoshe zipo taarifa kuwa kila kiongozi wa serikali akija mnamleta kiongozi wenu tofauti na anatoa maelezo mengine kabisa. Hii inaonyesha mnafanya mambo ya kihuni na mnachelewesha maendeleo kwa wananchi," alisema.

Naibu Waziri alisema wakati umefika wahandisi wa maji nchini kusimamia vyema makandarasi wanaopewa kazi na kwamba hata wao serikali haitawafumbia macho.

Alipohojiwa kuhusu utekelezaji wa mradi huo, Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Siha, Joyce Bahati, alisema kampuni hiyo ilitia saini mkataba wa miezi 10 na hadi sasa imemaliza miezi tisa na kazi imekamilika kwa asilimia 25.

Aidha, akizungumzia udhaifu wa utekelezaji wa mradi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Maji ya Munge, Musa Lamboseli, aliiomba serikali kuangalia namna ya kupata mkandarasi mwingine atakayesaidia kupatikana kwa maji kwa wakati.

"Wakati mnawapa hawa makandarasi kazi hakikisheni tayari walishafanya kazi nyingine na mkaziona kwani wanaharibu malengo ya serikali na kukwamisha maendeleo ya wananchi," alisema.

Mkurugenzi huyo, aliiambia Nipashe kuwa hawana uwezo wa kumaliza mradi huo kwa muda uliopo kwa kuwa wamelazimika kusimama kwa zaidi ya miezi mitatu kwa sababu ya umbali na ugumu wa miamba

# Dawa yaleta matumaini wagonjwa TB

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

NAIBU Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu ya Kibong'oto, Dk. Riziki Kisonga, amesema ujio wa dawa mpya ya kutibu maradhi hayo sugu ni ukombozi mkubwa katika mapambano ya kudhibiti magonjwa hayo nchini Tanzania na duniani kwa ujumla.

Katika mahojiano maalum na Nipashe kuhusu ujio wa dawa mpya ya kutibu ugonjwa huo, Dk. Kisonga alisema Taasisi ya Chakula na Dawa ya Marekani imetoa kibali cha matumizi ya dawa hiyo iitwayo 'Pretomanid' itumike kwa kuchanganya na dawa zingine mbili kutibu kifua kikuu sugu zaidi.

"Dawa moja ambayo imetangazwa inaitwa Pretomanid ambayo baada ya kufanyika utafiti mbalimbali Afrika Kusini na nchi zingine kama 14, imeonyesha mafanikio makubwa ikichanganywa na 'bedaquiline' na 'linezolid' katika kutibu kifua kikuu sugu zaidi," alisema Dk. Kisonga.

Alisema masharti ambayo yametolewa kwenye matumizi ya dawa hiyo ni pamoja na kuhakikisha inatumika tu kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu zaidi, yaani XDR-TB pamoja na wagonjwa wa kifua kikuu sugu, yaani MDR-TB ambao wameshindwa kutumia dawa zingine za awali na wengine ambao wamepata madhara ya dawa za awali za kutibu kifua kikuu sugu.

Aidha, Dk. Kisonga alisema kundi hilo pekee ndilo linaloweza kuingia kwenye kundi la matibabu kwa kutumia dawa hizo ambazo ni mchanganyiko wa dawa tatu za pretomanid, bedaquiline na linezolid.

"Tanzania mpaka sasa tangu tulipoanza kutoa huduma za kifua kikuu sugu, tumepata wagonjwa wawili ambao walikuwa wana kifua kikuu sugu zaidi. Tunashukuru kwamba dawa ambazo tulizichanganya wakati tunawapa tiba hawa wagonjwa, zimewasaidia na walipona na wanaendelea na shughuli zao za kawaida.

"Ukiniuliza, tumetumia muda gani kuwatibu mpaka wakapona wagonjwa wenyewe wanaweza wakashuhudia kwamba tumetumia zaidi ya miezi 24, wengine 36 kusema kwamba huyu mgonjwa amepona kabisa. Lakini ujio wa dawa hizi nafikiri unaweza ukawa ukombozi mkubwa sana katika mapambano ya kudhibiti kifua kikuu na kifua kikuu sugu zaidi Tanzania na nchi zingine duniani kote," alisema.

Dk. Kisonga pia alisema miaka ya 2000 mpaka 2016, wagonjwa wote waliokuwa wanagundulika na kifua kikuu sugu, walikuwa wanakwenda kuanza tiba katika Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu (Kibong'oto).

Lakini kuanzia mwaka 2016, alisema serikali iligatua huduma za kifua kikuu sugu nchini na kuanzisha vituo vidogo vidogo ambavyo vilikuwa na uwezo wa kuanzisha tiba za kifua kikuu sugu, kule kule ambako wagonjwa walikuwa wanagundulika.

Alisema kwa sasa kuna vituo 102 ambavyo vinatoa huduma hizo sawa sawa na hospitali ya magonjwa ambukizi ya Kibong'oto iliyoko Siha, mkoani Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa Dk. Kisonga, wagonjwa wamekuwa wakitumia dawa za kifua kikuu sugu za aina sita tofauti ambazo miongoni mwao kunakuwa na sindano ambayo mgonjwa anachoma siku tano kwa muda wa miezi sita mpaka minane na baada ya hapo anaendelea kutibiwa na dawa za vidonge kwa muda usiopungua miezi 12.



Ofisa Mradi wa kulinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili kutoka shirika lisilo la kiserikali la Action for Justice in Society (AJISO), Tatu Mruttu, akizungumza na wadau mbalimbali wa haki za watoto wakati wa uzinduzi wa mradi wa 'Tuwalinde', unaofadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), mkoani Kilimanjaro juzi. Mradi huo wa miaka miwili utatekelezwa katika kata tatu za Bomang'ombe, KIA na Masama-Rundugai wilayani Hai mkoani humo. **PICHA: JAMES LANKA**

# Aliyedai kubuni Tanzania aomba msaada kwa JPM

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MTANZANIA anayedai alishikiri shindano la kubuni jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964, Jotham Chagwah, amemwandikia barua Rais John Magufuli, akimwomba kutambua mchango wake katika ubunifu wa jina la taifa.

Chagwah ni Mkufunzi mstaafu wa Chuo cha Ualimu Marangu kilichoko Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Kwa sasa mzalendo huyo anaishi katika Mtaa wa Kilototoni ulioko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Himo.

"Mwaka 1964 wakati nikiwa nasoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Tanga, nilishiriki shindano la kubuni jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya Tanganyika na Zanzibar kuungana.

"Wakati shindano hilo likiendelea, serikali iliahidi kutoa zawadi ya Sh. 200 kwa mshindi wa shindano hilo na mimi nilibahatika kuwa miongoni mwa washindi na kutumiwa Sh. 12.50 kwa hundi iliyopitia kwa mkuu wangu wa shule niliyokuwa nasoma," alisema.

Kutokana na ushindi huo, Chagwah amesema amewandikia barua Rais Magufuli kumwomba kutambua mchango wake huo ili apewe heshima yake kama mmoja wa watu wazalendo.

Katika barua yake hiyo, Mtanzania huyo amemweleza historia yote namna alivyoshiriki shindano hilo baada ya Serikali ya Tanganyika na Zanzibar kutoa tangazo la kuwataka wananchi washiriki.

Baadhi ya viongozi wa kisiasa, akiwamo Felista Mtui ambaye ni Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, aliishauri serikali kujenga utamaduni wa kuzitambua juhudi zilizofanywa na wananchi wake, kabla na baada ya uhuru ili kuweka kumbukumbu sahihi kwa faida ya vizazi vijavyo.



Ukurasa 19

Umeme Stieglers: Mlango wa kufikia dira ya maendeleo



Ukurasa 18

Lindi, Mtwara 'kucheele' waamka kulima ufuta

# BUFE

Ijumaa Agosti 23, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Onyo la Marekani laiogopesha Ugiriki kuisaidia meli ya Iran

Ukurasa 15



# Michikichi yapewa kupaumbele, TARI Kahinga uwanja mpya wa maboresho

**Na Ashton Balaigwa**, MOROGORO

TANZANIA inatumia mabilioni ya fedha kila mwaka takribani bilioni 600 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje kwa vile kiwango cha bidhaa hiyo kinachozalishwa nchini hakikidhi mahitaji ya walaji.

Kwa kiasi kikubwa mafuta yanayozalishwa yanatokana na michikichi ambayo pamoja na kuchakatwa mafuta ya kula kama mawese kuna mengine yanayotumiwa viwandani au mafuta ya mise ambayo hupatikana hapa nchini japo kwa kiwango kidogo.

Chikichiki ndilo zao linalotoa mafuta mengi kwenye yale yanapandwa ukilinganisha na mazao mengine kama alizeti, ufuta, pamba, karanga na soya, wanasema watalaamu wa kilimo.

**INAENDELEA UK.16**

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Mradi unaowanasua waliokwama baada ya shule hadi ujasiriamali

Ukurasa 20

BIASHARA

# ‘Kinamama wanapojinasibu tur kiuchumi, ujasiriamali na uwek

Na Beatrice Philemon

MAFUNZO ya ujasiriamali yaliyotolewa kwa kinamama wa vijijini ni moja ya mambo yanayobadilisha jamii za wanawake ambao wanatamba kwa mafanikio.

Wanajinasibu kuwa wanatisha kiuchumi, ujasiriamali na uwekezaji na sasa ni walimu wa kuwafunza wenzao wanaolilia mafanikio yao ili kuondokana na umaskini na utegemezi.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wanawake wa Kijiji cha Luchingu, wilayani Newala, mkoa wa Mtwara , wanaeleza jinsi walivyopata mabadiliko makubwa na wameweza kuanzisha miradi mbalimbali ya biashara ili kujikwamua kiuchumi na kupambana na umasikini.

Hayo yanasemwa hivi karibuni na Katibu wa Kikundi cha kinamama cha Tukazane, Zainab Mohamed anapozungumza na waandishi wa habari na uongozi wa Action Aid Tanzania, waliokwenda kutembelea kikundi hicho kuona mafanikio ya miradi ya maendeleo ambayo imeanzishwa baada ya kupata mafunzo ya ujasiliamali kutoka shirika hilo.

Zainabu anasema kabla ya kupata elimu ya ujasiliamali wanawake wengi katika kijiji cha Luchingu na vijiji vingine wilayani Newala walikuwa hawaruhusiwi kufanya biashara wala kutoa ushauri wowote kwenye mikutano ya kijiji wala kwenda mikutanoni .

Shirika hilo lilitoa mafunzo ya ujasiliamali bure kwa wanawake katika wilaya ya Newala ikiwamo kijiji cha Luchingu kupitia program inayoitwa Local Rights Programmer (LRP) inayotekelezwa katika wilaya ya Newala na Tandahimba tangu mwaka 2002 hadi sasa.

“Wakati wa mafunzo wanawake walifunzwa ubunifu wa bidhaa, jinsi ya kuipenda bidhaa wanazozitengeneza, kutafuta masoko, kutumia vifungashio bora katika bidhaa zao, kujitangaza na kutumia vifungashio bora kwenye bidhaa yako na kutokata tamaa na pia jinsi ya kujiunga kwenye vikundi,” anasema.

### FAIDA

“Mafunzo haya yametusaidia kupiga hatua moja kwenda nyingine kwa sababu tumefanikiwa kuanzisha mradi wa ubanguaji korosho, ufugaji wa kuku wa kienyeji, kutengeneza batiki ili kujiongezea kipato na kuanzisha kikundi cha wanawake kinachoitwa Tukazane.” Anasema Zainabu.

Kikundi cha Tukazane kilianza mwaka 2011 baada ya kushauriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Newala na shirika la Action Aid Tanzania kujiunga katika vikundi kuanzia watu watano na kuendelea ili waweze kupata huduma mbalimbali za mafunzo na mikopo kwa urahisi, anaongeza.



Zainab akionyesha mafanikio makubwa ya uwekezaji ambayo ni nyumba aliyojenga kutokana na mapato ya biashara na ujasiriamali. PICHA

> **“Tunaomba wadau wanaoweza kutusaidia kupata mashine za kisasa kwa ajili ya kubangua korosho watusaidie ili tuweze kuongeza ubora wa bidhaa zetu na kuwa na uzalishaji wa kisasa zaidi.**

Mpaka sasa kikundi hicho kina wanachama nane ambao wanajishughulisha na miradi ya ubanguaji korosho, ufugaji kuku na kutengeneza batiki.

Katika mradi wa ufugaji kuku mpaka sasa wana kuku 50 wa kienyeji na kipato wanachokipata kutoka kwenye kuku wanapeleka kwenye mradi wa batiki.

Kwa upande wa mradi wa korosho, kila mwanachama ana shamba lake, lakini ikifika msimu wa mavuno kila mmoja analeta korosho zake kwenye kikundi na baada ya mauzo ya hizo korosho, tunagawana fedha kulingana na magunia ambayo mwanachama ameleta kwenye kikundi.

Kupitia mradi wa korosho mpaka sasa wanawake wawili wanachama wamenunua mashine za kisasa za kupulizia kwenye mikorosho na hii ni hatua kubwa.

“Tunaishukuru Action Aid Tanzania kwa kutupatia mafunzo ya ujasiriamali kwa sababu mafunzo yametuwezesha kupiga hatua tofauti na miaka ya nyuma kwa sababu hapo awali kabla ya mafunzo wanawake walikuwa hawaruhusiwi kufanya biashara na hivi sasa wanawake wanaweza kufanya biashara,” anasema



Katibu wa kikundi cha Tukazane, Zainab (mwenye baibui jeusi) na wanac njia za asili.

# natisha kezaji’



A ZOTE: BEATRICE PHILEMON



nama wenzake wakibangua korosho kwa

**FUNZA WENGINE**

Musuweta anasema shirika hilo limekuwa mkombozi wao, elimu waliyoipata wanafundisha kina mama wenzao ili nao waendelee mbele na waache utegemezi.

Kwa hivi sasa wanawake wengi wanasafiri katika mikoa mbalimbali ikiwemo Dar es Salaam kutafuta bidhaa za aina mbalimbali kwa ajili ya kuanzisha biashara katika wilaya ya Newala, wengine wameanza kushiriki maonyesho mbalimbali ili kutangaza bidhaa zao, kujifunza kutoka kwa wenzao na kutafuta masoko,” Zainabu anasema.

Aidha, kupitia miradi yao wanayoitekeleza, wanawake wengi katika kijiji cha Luchingu wameanza kuomba kufundishwa na kikundi chao jinsi ya kuanzisha na kusimamia miradi ya kibiashara.

Zainab mwenye miaka 59 na watoto watano ni miongoni mwa wanawake walionufaika na mradi wa mafunzo kutoka Action Aid Tanzania.

“Kupitia mradi wa ubanguaji korosho nimejenga nyumba ya kisasa, kusomesha watoto wangu na kujiongezea kipato,” anasema.

**CHANGAMOTO YA VIFAA**

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa kikundi cha wanawake cha Tukazane, Suwabu Musuweta, anasema ingawa wamejikita katika mradi wa ubanguaji korosho, wanatumia vifaa duni vya asili katika shughuli hizo.

Mbali na hilo bado hawajapata sehemu ya kubangulia korosho, wanakaa chini ya mti na wanatumia vinu kama meza na vigogo katika shughuli hiyo ambayo inachukua muda mrefu kufikia mahitaji wanayoagizwa na wateja.

Anasema katika kila gunia ghafi la korosho wanapata kilo 30 za korosho nyeupe.

“Tunaomba wadau wanaoweza kutusaidia kupata mashine za kisasa kwa ajili ya kubangua korosho watusaidie ili tuweze kuongeza ubora wa bidhaa zetu na kuwa na uzalishaji wa kisasa zaidi,” anasema Musuweta.

Kadhalika , anasema ukipita kila mtaa utakuta wanawake wengi wamejiunga katika vikundi.

Akizungumzia hali ya uchumi kwa wananchi na wanawake katika kijiji cha Luchingu anasema katika suala la kiuchumi hapo awali walikuwa hawajaamka.

Lakini kutokana na elimu waliyoipata hali imebadilika, wanawake wengi wanafanya kazi, wanakwenda Dar es Salaam kuchukua bidhaa na kuja kufungua vibanda vya biashara, nyanya, vitunguu na biashara zingine ndogo ndogo.

“Tumebadilika Action Aid imetupanua mawazo na kutusaidia mafunzo ya ujasiliamali lakini bado tunatumia utalaamu wa asili katika ubanguaji wa korosho, tungependa na sisi tutumie mashine za kisasa,” anasema Mwenyekiti.

“Mimi Mwenyekiti na kikundi chetu tuna ndoto ya kuona chama chetu na wanawake wa Newala tuna kuwa mfano wa kuigwa , tuwe juu kimaendeleo ili wenzetu wajifunze zaidi, sisi tupo tunapambana.” Anaongeza.

Anasema hapo awali wapo akina baba walikuwa wanawabana kina mama wasifanye shughuli yeyote, lakini baada ya kupata mafunzo, wanaume wamebadilika na kuwaruhusu akina mama wafanye kazi.

“Miaka ya nyuma mwanamke alikuwa harusiwi kufanya biashara, mtoto wa kike harusiwi kwenda shuleni, mwanamke haruhusiwi kutoa ushauri wowote kwenye maamuzi, mikutano ya kijiji wala kwenda kwenye mikutano,” anasema.

Vile vile ulikuwa unaenda shamba, unalima, mnauza mazao, na mkipata Sh. milioni tano mwanaume anakwambia anaongeza mke mwingine. Kutokana na dharau hiyo tatizo la talaka lilikuwa kubwa na watoto walikuwa machokoraa na waliokosa elimu.

Anasema baada ya kupata elimu na wanaume kuona wanawake anaweza kukomboa familia, hivi sasa wanaume wameanza kubadilika na kutulia na wanawake.

“Hivi sasa tunatoa maamuzi pamoja, wanaume wapo vizuri na wameelimika, kama wapo ni wale ambao hawajitambui, lakini wale ambao wameona maendeleo ya wanawake wamebadilika na sasa hivi wanakaa pamoja na kupanga bajeti pamoja na mwanamke,” anasema Mwenyekiti.

Anasema ingawa wamejikita katika kilimo cha korosho, changamoto kubwa ni upatikanaji wa pembejeo, au kuchelewa na upatikanaji wa dawa za kupulizia kwenye mikorosho kama vile ‘sculpture’ ya unga inakuwa ngumu kupatikana.

“Kwa mtu mwenye ekari mbili angalau unaweza kutumia Sh. 600,000 gharama za kulipa vibarua, kufagilia shamba na kupuliza dawa mikorosho na kila mkorosho mmoja unapuliziwa kwa Sh.200 wakati kulima shamba bei ni kuanzia Sh. 70,000 kwa heka hadi 80,000.

Kufagilia shamba ekari moja bei inaanzia Sh. 50,000 hadi 60,000,” anasema Musuweta.

Aidha, anasema vile vile mikorosho 50 inatumia petrol lita moja ya mafuta kwa ajili ya kuendesha jenereta inayosukuma dawa kwenye bomba na kilo 50 za sulphur na hii inategemea na ukubwa wa mkorosho.

# Onyo la Marekani laiogopesha Ugiriki kuisaidia meli ya Iran



Meli Adrian Darya 1 ikiondoka Gibraltar baada ya kuachiwa. **PICHA: MTANDAO**

UGIRIKI imekataa kuisaidia meli ya mafuta ya Iran ambayo hivi majuzi ilizuiwa Gibraltar kwa tuhuma ya kusafirisha mafuta kuelekea Syria.

Naibu waziri wa masuala ya kigeni, Miltidias Varvitsiotis, anasema kwamba taifa lake haliko tayari kuisaidia Meli hiyo inayodaiwa kuelekea Syria.

Hatua hiyo inajiri baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, kutishia vikwazo dhidi ya taifa lolote ambalo litaisaidia meli hiyo.

Adrian Darya 1 iliondoka Gibraltar siku ya Jumapili na kusema kwamba inaelekea katika bandari ya Ugiriki ya Kalamata.

Mamlaka katika taifa hilo linalomilikiwa na Uingereza, ziliizuia meli hiyo mwezi Julai. Awali ilijulikana kama Grace 1.

Licha ya ombi la dakika za mwisho la Marekani, Gibraltar iliiachia meli hiyo siku ya Ijumaa na ikaondoka kuelekea Mashariki mwa bahari ya Mediterranean.

Iran imenukuliwa ikisema kwamba iko tayari kutuma wanamaji wake ili kuisindikiza meli hiyo na sasa iko Kaskazini mwa bandari ya Algeria ya Oran.

JE UGIRIKI IMESEMAJE?

Kulingana na vyombo vya habari vya taifa hilo, Varvitsiotis alithibitisha kwamba Marekani imeitaka kutoisaidia meli hiyo. Iran haijawasiliana na serikali ya Ugiriki, alisema.

Hatahivyo, meli hiyo ya Adrian 1 ambayo inabeba mapipa milioni 2 ya mafuta ghafi ni kubwa mno kwa bandari yoyote ya Ugiriki kuiegesha, alisema Varvitsiotis.

Alipoulizwa je, Ugiriki itachukua hatua gani iwapo meli hiyo itaegesha katika maji ya taifa hilo, alijibu iwapo hilo litatokea tutaona la kufanya.

Marekani inaamini Adrian Darya-1 ina uhusiano na Jeshi la Iran la Revolutionary Guard, tawi la jeshi la taifa hilo ambalo limetajwa kuwa kundi la kigaidi na Marekani.

“Tunataka kuwanyima njia za kuendeleza kampeni yao ya ugaidi, tumesema wazi kwamba mtu yeyote atakayeisaidia, yeyote atakayeiruhusu kuegesha katika bandari yake atakuwa katika hatari ya kupokea vikwazo vya Marekani,” alisema Pompeo na kuongeza:

“Marekani itachukua hatua inayoweza kuizuia meli hiyo kuwasili Syria.”

Adrian Darya-1 bado imesema kwamba inaelekea katika bandari ya Kalamata

Samir Madani, mwanzilishi wa tovuti ya masuala ya baharini TankerTrackers.com, ameaimbia BBC kwamba meli hiyo ilikuwa inajaribu kurudi nyumbani kupitia rasi ya Suez Canal.

Italazimika kupakua mapipa milioni moja kwa meli nyingine ambayo itakuwa ikipeperusha bendera ya Iran kwa kuwa meli hiyo imebeba uzani mkubwa, alisema.

Kuelekea Syria pia itakuwa vigumu kwa kuwa imebeba mafuta mengi mno kupakua bila usaidizi katika bandari ya Baniyas. **BBC**

UCHUMI

TANZANIA KUJITOSHELEZA KWA MAFUTA

# Michikichi yapewa kipaumbele, TARI Kahinga uwanja mpya wa maboresho

INAENDELEA UK.16

Hata hivyo, mchikichi pamoja na kuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha mafuta kwa wingi lakini unalimwa kienyeji kwa miaka mingi hasa katika Mkoa wa Kigoma na kusababisha wananchi kutoona umuhimu na faida zake, anasema mtalamu wa kilimo Dk. Filson Kajimbo.

Kutokana na upungufu wa uzalishaji wa mafuta hapa nchini serikali imeziagiza Taasisi ya Kilimo (TARI) kuanza kufufua michikichi inayolimwa kwa wingi mkoani Kigoma kwa kuanza utafiti wa mbegu bora ili zizalishe mafuta, hilo linatokea baada ya kulipa kipaumbele zao hilo na sasa TARI imeanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Michikichi-Kihinga.

Kwa hiyo TARI Kihinga iliyoko Kigoma ndiyo inayobeba jukumu la uzalishaji wa mbegu bora za michikichi, anasema Dk Filson Kagimbo.



Kaimu Mkurugenzi wa TARI Kahinga, Dk Kagimbo (kushoto),akitoa maelezo kuhusu chikichi kwa wakulima waliotembelea banda la TARI wakati wa maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu, **PICHA ZOTE: ASHTON BALAIGWA.**

### KUFUFUA MICHIKICHI

Akizungumza katika mahojiano maalumu na gazeti hili kuhusu utekelezaji wa mkakati huo ,Kaimu Mkurugenzi wa TARI Kihinga, Kagimbo, anasema uzalishaji umeanza kwa mikungu 1,290 inayochavushwa ili kuanza kutoa mbegu za michikichi iliyoboreshwa.

Dokta Kajimbo anasema takribani mbegu 2,000,000 zimeanza kuzalishwa ili kupanda miti hiyo na kupata mafuta baada ya kuchavushwa. Hatua itakayopunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi, kwa mujibu wa maoni yake.

Anasema mbegu hiyo iliyochavushwa itatosha kupanda eneo la hekari 38,000 na kwamba kwa sasa mbegu 63,000 zimeshavunwa na zinazoweza kupandwa kwenye heka 1,260 zilizoko mkoa wa Kigoma maeneo na mingine inayolimwa michikichi.

### UMUHIMU KIPEKEE

Aidha, Kagimbo anasema michikichi ni maarufu kwa mafuta ya kula na yale yanayotumika viwandani na ndilo zao pekee linalotoa mafuta mengi kwa mimea inayopandwa ardhini ukilinganisha na mazao mengine ya mafuta kama karanga , ufuta , pamba na alizeti.

Anasema ukiweka mazao yote yanayotoa mafuta kila zao likawekwa kwenye eneo la heka moja, ni mchikichi pekee inayotoa mafuta mengi kuliko mengine anasema Dk. Kagimbo.

Mtaalamu huyu ambaye pia ni Mratibu wa Kitaifa wa Michikichi anasema mkakati huo utazalisha na kuongeza mafuta huku ukipunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje .

> **"Mafuta ya mawese yanayozalishwa na kuliwa nchini ni asilimia 0.7 hivyo kunahitajika nguvu ya ziada kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo.**

"Mafuta ya mawese yanayozalishwa na kuliwa nchini ni asilimia 0.7 hivyo kunahitajika nguvu ya ziada kwajili ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo", anasema mtaalamu huyo wa kilimo.

Anaongeza kuwa uzalishaji wa zao la mchikichi upo chini na kufikia wastani wa tani 1.6 kwa hekta wakati nchi kama Malaysia wanapata tani nane kwa hekta kiwango ambacho kinapaswa kufikiwa na Tanzania pia.

### MBEGU MPYA

Dokta Kagimba, anataja sababu kubwa ya uzalishaji mdogo kuwa ni pamoja na kutumia mbegu za kienyeji ambazo zimekuwa zikitoa mafuta kidogo kwa kuwa asilimia 90 ya michikichi yote inayolimwa nchini ni ya kienyeji.

Anasema kuwa mbegu za kisasa zilizoanza kuzalishwa za michikichi aina 'Tenera' kwa sasa matumizi yake ni wastani wa asilimia 10 pekee ambazo zimeonyesha uwezo wa kutoa mafuta mengi.

Mtafiti Dk Kagimbo anataja sababu kubwa ya uzalishaji mdogo kuwa ni Tanzania kulima mbegu ya kienyeji ya 'Dura' inayotoa mafuta kidogo tofauti na ile ya Terena.

Anasema asilimia 90 ya michikichi yote inayolimwa Tanzania ni aina ya Dura ambayo ni ya kienyeji. Asilimia 10 ni aina ya Tenera ambayo ni ya kisasa.

"Mbegu ya Tenera ambayo ni ya kisasa inaweza ikatoa mafuta mara tano mpaka 10 zaidi ya ile ya Dura na hivyo tukiongeza uzalishaji wake tutapata mafuta ya kutosha na ziada kupitia michikichi yetu." Anasema mtaalamu huyo.



Dokta Kagimbo (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dk. Geofrey Mkamilo, kuhusu zao hilo linavyooteshwa hadi kuvunwa.

### ARDHI DUNI

Dokta Kagimbo anatoa sababu ya uzalishaji wa michikichi kuwa chini nchini kuwa ni pamoja na udogo wa eneo linalotumika kwa uzalishaji wa zao hilo, kuwa ni udogo wa ardhi inayotumiwa kulima.

Anatoa mfano Kigoma ambako michikichi inalimwa kwa wingi zaidi ya asilimia 80, eneo linalofaa ni hekta 114,000 wakati eneo lililolimwa ni hekta 23,000 kiwango ambacho ni kidogo na hivyo uzalishaji wake kuwa wa chini.

Anaeleza sababu ya tatu inayosababisha uzalishaji wa michikichi kuwa chini kuwa ni umri mkubwa wa miti iliyo mashambani hapo na kwamba kuna zaidi ya asilimia 95 ya michikichi iliyolimwa ina zaidi ya miaka 60.

Anasema wakati mmea huo unatakiwa kuishi si zaidi ya miaka 30 kwa uzalishaji wenye tija , huko Kigoma imekuwa na umri wa karibu mara mbili wa ule unaotakiwa.

"Mti wa mchikichi unao uwezo wa kuishi hata zaidi ya miaka 150 lakini katika umri huo, uzalishaji wake hauna tija hata kidogo na hivyo kutokuwa na faida,"anasema Dk Kagimbo.

Alisema serikali imeamua kufufua kilimo cha michikichi na imeshaanza kuchukua hatua ambayo ni kuongeza zao hilo kwenye orodha ya mazao ya kimkakati ikiwa ni pamoja na serikali kuanzisha Kituo cha Utafiti ch Kihinga TARI ambacho kinaratibu utafiti katika nyanja zote za mnyororo wa thamani wa zao hili.

### TARI ILIVYOJIPANGA

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk Geoffrey Mkamilo, anasema kuwa mpango huo wa uzalishaji wa mbegu hizo umelenga kuisaidia kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 600 zinazotumika kwa mwaka kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje.

"Hilo linatokea wakati uwezo wa kuzalisha mafuta upo. TARI Kihinga itaongeza idadi ya watalaam wa zao hilo na kuwapatia vitendea kazi kama magari na pikipiki kama alivyoagiza Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wakati wa kikao cha wadau wa zao hilo."anasema Dk.Mkamilo.

Anaongeza kuwa serikali imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya mageuzi makubwa kwa ajili ya kuanza kuzalisha kwa wingi miche ya chikichi bora ili kumaliza tatizo la mafuta nchini.

Anasema kwa sasa Tanzania imeweka mkakati wa kufufua kilimo cha michikichi na imeshaanza kuchukua hatua mbalimbali za kufanikisha kazi hiyo kwa zao hilo linachangia kwa haraka uzalishaji mafuta nchini na kufuatia na mazao mengine kama alizeti na karanga.

### MALENGO

Dokta Mkamilo anataja baadhi ya mikakati hiyo kuwa ni pamoja na uzalishaji wa mbegu unaotumia teknolojia ya kisasa ya kuchavusha maua ya mchikichi aina ya Dura ili iweze kuongeza uzalishaji wa mafuta kutoka tani 1.6 kwa hekta ya sasa na kufikia tani nne hadi tano kwa hekta.

Mkakati mwingine ni kuongeza michikichi kwenye orodha ya mazao ya kimkakati, kama ambavyo serikali imetangaza na kwamba TARI Kihinga inafanya na kuratibu utafiti katika nyanja zote za mnyororo wa thamani wa zao hilo. Mkamilo anasema tayari mbegu hizo zimeanza kusambazwa katika taasisi zilizochaguliwa rasmi kwa uzalishaji wa michikichi mkoani Kigoma.

Anazitaja kuwa ni pamoja na Gereza la Kwitanga ambalo limepewa mbegu 30,000 zinazotosha eneo la ekari 600, kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa *JKT) Bulombora, iliyopewa mbegu 19,000 ambazo zinapandwa kwenye ekari 393, na Gereza la Ilagala mbegu 10,000 zinazoweza kupanda kwenye ekari 200.

Mkurugenzi huyo anasema TARI kwa kushirikiana na wazalishaji wa kampuni binafsi wa mbegu wana mkakati wa kuzalisha mbegu milioni 5.0 kwa mwaka.

Aidha, ndani ya miaka mitatu zitakuwa zimezalishwa mbegu milioni 15 za kutosha eneo linalofaa kulima michikichi mkoa wa Kigoma kabla ya kuhamia mikoa mingine inayolima zao hilo ya Mbeya, Morogoro, Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Kagera.

Dokta Mkamilo anasema baada kuwapa wakulima mbegu bora katika eneo lote linalofaa kwa michikichi, likapandwa na yote iliyozeeka ikatolewa na kupandwa ya kisasa, uzalishaji wa mafuta utaongezeka na hivyo uangizaji wa mafuta ya kula kutoka nje utakwisha .

### WADAU UZALISHAJI

Mkuu wa Gereza la Kwitanga lililopo Kigoma, Dominic Kristian, ambaye ametoa shamba kwa ajili ya uchavushaji wa michikichi anasema kuwa tayari wameshaanza kupanda mbegu hizo baada ya kuchavushwa na hekta nyingine zinaendelea lengo ni kupata miche yenye mikungu inayotoa mawese mengi.

Mkuu huyo wa gereza anasema kuwa kwa kushirikiana na wadau watahakikisha wanafikisha malengo waliyopewa na serikali ifikapo mwakani kwa kuwa utayarishaji wa mashamba hayo umekamilika.

### WIZARA YA KILIMO

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, anasema utekelezaji wa mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kupikia hapa nchini unafanyika kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, taasisi za umma, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, sekta binafsi na wakulima.

Anasema mazao yaliyopewa kipaumbele katika mkakati huo ni alizeti, pamba na mchikichi ambayo yamelenga uzalishaji huo wa mafuta kwa kuandaa mkakati madhubuti.

## Biashara katika picha




Machinga wakiwa wametandaza bidhaa zao jirani kabisa na taa za kuongozea magari katika makutano ya Barabara ya Uhuru na Msimbazi, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**



Mchuuzi wa mihogo ya kukaanga akiiandaa tayari kwa kuwauzia wateja wake katika eneo la Msasani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA PICHA: JOHN BADI**



Wauza kashata wakisubiri wateja katika eneo la stendi Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. Kashata ni kitafunwa kinachopendwa zaidi na watoto na vijana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

BIASHARA

# Lindi, Mtwara 'kucheele' waamka kulima ufuta



Wakulima wa ufuta wakifurahia kazi yao, zama hizi zao hilo linaelezwa kuwa na mafanikio na bei ya kuvutia inayoshindana na ya korosho. Hayo ni miongoni mwa mambo yanayowahamasisha wakulima wa Lindi na Mtwara kuanza kulima ufuta. **PICHA: MTANDAO**

**Na Faustine Feliciane,** aliyekuwa Nanyumbu

WAKULIMA wa Lindi na Mtwara pamoja na kwamba ni wazalishaji wakubwa wa korosho huenda wakabadili gia angani baada ya kuona fursa zaidi kwenye kulima ufuta.

Kwa miaka ya karibuni ufuta umekuwa kama mbadala wa korosho katika kuwaongezea kipato wakulima,Ofisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika wa Wilaya ya Nanyumbu, mkoani Mtwara, Maganga Ngashi, akizungumza na Nipashe kwenye mahojiano maalum kwenye kilele cha Maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika Ngongo mkoani Lindi, anasema kwa sasa mkazo wao mkubwa ni kuhakikisha zao la ufuta linakuwa mbadala wa korosho.

Anasimulia kumekuwa na mwamko mkubwa wa kuzalisha ufuta hasa baada ya kuona linashika nafasi ya pili kwa kuwaingizia kipato wananchi wa mikoa hiyo nyuma ya korosho.

"Mwanzoni uzalishaji ulikuwa mdogo sana wengi walijikita zaidi kwenye korosho na mazao mengine ufuta, lilikuwa kama mazao mengine ya kawaida," anasema Ngahi.

> "Kuondokana na wadudu hawa ni lazima mkulima apulizie dawa ya kuua wadudu mara mbili tu, mwanzoni na baada ya mmea kukua na kutoa maua.

Anaongeza : "Kama Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu tulianza kuweka mikakati yakuinua ufuta ili kuwapa fursa wakulima wetu wa kupata mapato mbali na korosho. Tulianza kwa kutoa elimu na kuweka makadirio ya kuzalisha tani1,800 katika msimu wa mwaka 2018/2019, lakini wakulima walienda mbali zaidi ya tukajikuta tumezalisha zaidi ya tani 2,500."

Anasema jambo zuri zaidi ni baada ya kuwapo kwa soko kubwa la zao hilo ambalo pia limekuwa na bei ya kuridhisha inayowafanya wakulima kuona thamani yake.

"Ufuta unauzwa kati ya Sh. 2,800 na 3,000 kwa kilo, bei ni tofauti kubwa na miaka ya nyuma, ukiangalia bei yake inakimbizana kwa karibu na korosho ambayo ni 3, 500," anasema Ngashi.

Ofisa huyo anaeleza kuwa katika msimu huo wa mwaka 2018/2019, ufuta umechangia asilimia 30 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Nanyumbu.

"Mikakati ambayo tumeiweka kwa sasa ni kuhakikisha tunazidisha uzalishaji wa ufuta, katika msimu ujao wa 2019/2020 tunataka kuzalisha tani 3,000 ili kuongeza mapato yetu ya ndani," anaongeza Ngashi.

Ufuta umekuwa ukilimwa katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia kupanda kwake mpaka kufikia kuvunwa shambani.

Wakulima wanaanza kupanda mwezi Desemba na kuvuna kati ya mwishoni mwa mwezi Machi mpaka Aprili.

Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika amewahamasisha wananchi wa mkoa wa Mtwara hususani Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kuongeza uzalishaji wa zao hilo kama kaya ili kuweza kujiongezea kipato zaidi.

"Niwaambie wakulima wenzangu, ufuta kwa sasa ni zao lenye tija kubwa sana, halina shida ya soko hivyo kama kaya itatumia hii fursa kwa kuzalisha kwa wingi zao ni wazi wataongeza kwa kiasi kikubwa mapato yao," anasema Ngashi.

KUONGEZEKA UZALISHAJI

Mmoja wa wakulima wa zao la ufuta wa eneo la Mangaka, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, Edmund Mbala, anaweka wazi sababu za kuongezeka zaidi kwa uzalishaji wa ufuta kuwa ni pamoja na utumiaji wa mbegu bora na ulimaji kisasa.

"Huko nyuma wakulima walikuwa wakilima kimazoea, tulikuwa tunatumia mbegu za asili, lakini sasa tuna mbegu za kisasa zinazazalishwa kwenye vyuo mbalimbali ambazo zinatoa matokeo bora," anaeleza Mbala.

Anasema wakulima wengi wadogo hawakuwa na uwezo wa kupata mbegu bora, lakini sasa upatikanaji ni mkubwa ndiyo maana wanaona uzalishaji wa ufuta umekuwa ukipanda kila msimu," anaongeza.

Alisema Chuo cha Utafiti na Kilimo cha Naliendele cha mkoani Mtwara kimechangia katika upatikanaji wa mbegu bora za ufuta.

"Tuna mbegu ya Mangaka 1 ambayo tunazalisha sisi wenyewe baada ya kupata mafunzo kutoka Chuo cha Naliendele, hii imechangia sana kupata mazao mengi, mbegu hii ikitumiwa kama inavyoelekeza inampa nafasi kubwa mkulima kupata ufuta mwingi," anasema Mbala.

Anasema mbegu hiyo ya Mangaka 1 kama inatumiwa vizuri ina uwezo wa kutoa magunia matano na zaidi katika kila ekta moja ya shamba la ufuta.

Anasema wanaendelea kupambana na changamoto ya wadudu waharibifu wa zao hilo ambao wamekuwa wakila maua ya ufuta kabla ya kuchanua.

"Kuondokana na wadudu hawa ni lazima mkulima apulizie dawa ya kuua wadudu mara mbili tu, mwanzoni na baada ya mmea kukua na kutoa maua," anakumbusha Mbala.

**KUHUSU TIJA**

Faida kubwa wanayoipata kwa sasa wakulima wa ufuta imeelezwa kuwa imechangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumo mpya wa uuzwaji wa zao hilo wa stakabadhi ghalani.

Mkurugenzi Mtendaji (DED) wa Halmashauri ya Nanyumbu, Hamis Dambaya, anasema mfumo huo umewasaidia wakulima katika mauzo yao na umeondoa changamoto ya mauzo.

'Miaka ya nyuma soko lilikuwa changamoto kubwa sana, lakini mfumo huu mpya umesaidia wakulima, wanachukulia kama fursa ya kuzalisha kwa wingi ufuta," anasema Dambaya.

Anawaambia kuwa halmashauri itaendelea kushirikiana na wakulima katika kusaidia namna bora ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kwamba tofauti na korosho, ufuta hauna gharama kubwa za uzalishaji ikilinganishwa na korosho.

BIASHARA

# Umeme Stieglers: Mlango wa kufikia dira ya maendeleo

**Na Reubeni Lumbagala,**

DODOMA



Moja ya vituo vya kufua umeme nchini ambavyo vimejengwa miaka ya karibuni kupunguza uhaba wa nishati mkoani Katavi. **PICHA: MTANDAO**

DIRA ya maendeleo ya Tanzania inaelekeza kuifanya kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Ili kutekeleza dira hii, mkazo umewekwa katika ujenzi wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo, kukuza sekta ya kilimo na uwepo wa nishati ya umeme wa uhakika ili kuwezesha kuendesha shughuli za viwandani.

Moja ya miundomsingi ya maendeleo ni nishati ya na katika kutimiza azma ya kuifikisha Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati nguvu ya umeme ni msingi mkubwa.

Ongezeko la viwanda hapa nchini ni dhahiri linaongeza mahitaji ya nishati hiyo ili kukidhi mahitaji mapya ya uzalishaji viwandani.

Safari ya ujenzi wa viwanda inaendelea ambapo wawekezaji wa ndani na n je ya nchi wanaohamasishwa kuja kuwekeza Tanzania katika nyanja mbalimbali kama viwanda vya kusindika samaki na mazao mengine ya baharini, kilimo, ufugaji, elimu na afya.

Uwekezaji una faida nyingi zikiwamo kukuza mitaji ya wawekezaji hasa wa ndani, kutoa ajira, kuongeza mapato ya taifa na kukuza uchumi kwa ujumla.

Juhudi za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati haziwezi kufanikiwa ikiwa nishati ya umeme wa uhakika itakosekana.

Kutokana na ukweli huu, ndiyo maana serikali ya awamu ya tano ilipokuja na mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere au mwanzoni 'Stiegler's Gorge' uliopo kwenye bonde la Mto Rufiji katikati ya mikoa ya Pwani na sehemu nyingine Morogoro kila mpenda maendeleo aliunga mkono.

Mradi huo una uwezo wa kuzalisha umeme wa Megawati 2,115 ambazo zitaongeza umeme unaopatikana nchini kufikia takribani megawati 4,000.

Kukamilika na kuanza kutumika mradi huo wa umeme kutatoa nafasi ya kukidhi mahitaji ya nishati ya umeme wa kutumika viwandani, katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali pamoja na matumizi ya majumbani.

Megawati 2,115 ni umeme mwingi ambao unazidi kuipaisha Tanzania kwa kuwa na kiwango kikubwa cha umeme nchini.

Hivyo basi, kukamilika kwa mradi huu kunatoa nafasi kwa viwanda vingi kupata umeme wa uhakika na wa gharama nafuu.

Viwanda vikipata umeme wa uhakika na wa gharama nafuu bidhaa zinazozalishwa viwandani zinashuka bei na kuuzwa kwa gharama nafuu na hivyo wananchi kumudu kuzinunua bidhaa zinazozalishwa viwandani.

> **"Wawekezaji watavutiwa kuwekeza Tanzania kutokana na uhakika wa kuuziwa umeme kwa gharama nafuu kutokana na uzalishani wa Megawati 2115 kutoka Mto Rufiji.**

Kukatika kwa umeme kumekuwa kikwazo cha uzalishaji wa uhakika wa bidhaa mbalimbali viwandani na pia utoaji huduma hivyo mradi wa umeme wa Julius Nyerere unakuwa tiba ya kukatikakatika shughuli za uzalishaji viwandani.

Wamiliki na wawekezaji wa viwanda wanapotumia umeme mbadala kama wa jenereta katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji huduma, huingia katika hasara kutokana na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya kuendeshea jenereta hizo na kusababisha ongezeko la bei ya kile wanachozalisha.

Kutokana na mwarobaini wa ujenzi wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere, tatizo la upungufu wa umeme na kuongezeka bei ya bidhaa mara kwa mara, kutapungua kwa asilimia kubwa.

Wawekezaji waliokuwa na hofu ya kuwekeza katika viwanda kutokana na changamoto ya nishati ya umeme wa uhakika, hawatakuwa na hofu hiyo tena mradi pindi mradi huu utakapokamilika.

Kwahiyo, wawekezaji watakuwa na uhakika wa kukuza mitaji yao kwani watakuwa na uhakika wa kuzalisha bidhaa zao pasipo kutumia mitaji yao kwa nishati mbadala.

Wawekezaji watavutiwa kuwekeza Tanzania kutokana na uhakika wa kuuziwa umeme kwa gharama nafuu kutokana na uzalishaji wa megawati 2,115 kutoka Mto Rufiji.

Upatikanaji wa umeme wa uhakika utachochea shughuli za viwandani kufanyika kwa saa 24. Hakutakuwa na sababu ya viwanda kufanya kazi saa chache ama kufungwa kwa kukosa umeme wa uhakika na wenye kutosheleza mahitaji ya kufanya kazi mfululizo.

Katika mchango wa viwanda kuchagiza ukuaji wa uchumi, wamiliki wa viwanda watalazimika kuongeza idadi ya wafanyakazi ili wakidhi mahitaji ya uzalishaji unaoweza kuhitaji watu kufanya kazi saa 24.

Wakulima wataongeza uzalishaji ili kulisha mahitaji ya viwanda kwa kutoa malighafi muhimu zinazohitajika katika uzalishaji. Vilevile, serikali itapata mapato kupitia kodi zitakazolipwa na wamiliki wa viwanda na wafanyakazi wake.

Uzalishaji wa megawati 2,115 utatoa nafasi kwa serikali kuuza nishati hiyo katika nchi za jirani zikiwamo za Afrika Kusini na Mashariki zenye mahitaji ya umeme kwa ajili ya kupunguza upungufu.

Fedha zitakazopatikana kutokana na mauzo ya nishati ya umeme zitatumika katika ujenzi wa miradi mbalimbali vikiwamo viwanda vyingine. Pia fedha hizo zitasaidia kuinua sekta nyingine muhimu kama kilimo, miundombinu, elimu, afya, maji, uvuvi na ufugaji ambazo ni sekta nyeti katika kuendeleza maendeleo ya viwanda hapa nchini.

Muhimu ni mkandarasi wa mradi huu kufanya kazi kwa mujibu wa makubaliano ili mradi uweze kukamilika kwa wakati na hatimaye nchi ianze kunufaika na matunda yake hasa sekta ya viwanda. Mradi wa umeme wa Julius Nyerere ambao ni tiba mbadala wa mahitaji ya nishati ya umeme kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii unafungua milango ya kuifanya Tanzania kuwa taifa la nishati ya uhakika barani Afrika.

***Maoni: (+255) 764 666349***

UCHUMI

# Wataalamu wanavyovutana mkwamo uchumi Marekani



Mfanyakazi wa Marekani akiwa kazini kwenye moja ya viwanda nchini humo. Pamoja na kuwa na teknolojia na utaalamu mwingi upatikanaji ajira ni tatizo linalotikisa uchumi. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

MJADALA mkali unaendelea nchini Marekani kuhusu hali ya uchumi wa nchi hiyo, ambayo imekuwa kama homa inapanda wanahofia kuwa uchumi unaelekea mkwamo au hitilafu kali ya kukua kwake.

Aidha, takwimu katika soko la fedha na matokeo ya vipindi tofauti (mwezi au miezi mitatu) katika sekta tofauti kama ajira, faida ya jumla ya kampuni kubwa, thamani ya hisa soko la mitaji kuanza tena kuonyesha kuwa kasi ya kukua kwa sekta tofauti inavutia, lakini katika mafanikio hayo takwimu hasi zinaibuka tena na kuleta mvutano.

Moja ya sababu za kuhofia kuwa uchumi unaingia katika kipindi cha mkwamo au kukwama kwa uzalishaji wawekezaji wakihofia faida, au soko ni kupungua kwa uhitaji wa dhamana za serikali katika soko la fedha kwa kiwango ambacho ni chini ya dhamana ya miaka miwili.

Ni kielelezo kinachotumika na wapinzani kwani uhitaji unapopungua chini ya kiwango hicho mkwamo wa uzalishaji unafuata, lakini baadhi ya wataalamu wanasema si nyenzo ya kutegemewa. Wanasisitiza uchumi wa Marekani ni imara.

Yuko mwanaharakati ambaye amewahi kuwa Naibu Waziri wa Fedha nchini humo, Profesa Paul Craig Roberts ambaye ni mchangiaji katika mitandao na vyanzo kadhaa vya habari kimataifa, ambaye anasisitiza kuwa uchumi wa Marekani tayari umeingia katika mkwamo dhaifu wa uzalishaji. Tatizo la kile alichosema hata hivyo ni kuwa Marekani haijawahi kuzinduka kikamilifu kutoka mkwamo wa 2008 na mnyauko wa soko la hisa uliofuata, jambo ambalo wataalamu walio wengi hawalikubali.

> **Hali hiyo ilisababisha 'mnyauko' wa pointi 800 za thamani katika soko la hisa, na takwimu mpya kuhusu ajira miezi mitatu iliyopita zikafufua soko.**

Anapinga kwa nguvu 'majigambo'ya Rais Donald Trump kuwa uchumi wa Marekani ni bora duniani tena kwa mbali.

Anahoji pia ukusanyaji wa takwimu za kutokuwa na kazi, akisema kuwa zinalenga wanaotafuta kazi kwa wakati uliopo na siyo waliokata tamaa, kwani ambao hawajatafuta kazi kwa wiki nne mfululizo wanaondolewa katika idadi hiyo.

Ni kuwaingiza katika takwimu za wasio na kazi, na si za watafutaji ajira. Wachangiaji wengine katika mjadala huo wanasisitiza kuwa ipo hatari ya mkwamo katika siku za usoni lakini hawana uhakika kama mkwamo huo umeshafikiwa, ila kuna hitilafu kwani mkwamo ambao unajadiliwa unagusa Marekani na haielekei kuwa kitovu chake ni Marekani.

Baadhi ya wachumi wanazungumzia mkwamo wa uchumi wa Marekani pamoja na uchumi wa dunia kwa jumla, hali ambayo kimsingi inaambatana na kupungua kasi kwa uchumi wa China, wakati uchumi wa Marekani ulipungua kasi kidogo kiasi.Kimahesabu uchumi wa China unakua kwa kasi kuliko Marekani kwani ni mchanga zaidi, lakini katika hali halisi kuna mkwamo wa kina kutokana na kupandishiwa ushuru wa forodha au kuwekewa vikwazo na Marekani.

Wasimamizi wa uchumi katika utawala wa Trump hawapuuzii uwezekano wa mkwamo laini kuwa mkali zaidi siku za usoni, huku wataalamu wanakinzana ni hatua gani zinafaa kuchukuliwa. Wale wa itikadi ya kiliberali yaani wapenda maendeleo ambao si wahafidhina wanataka vikwazo na ushuru zaidi kwa bidhaa za China viondolewe, wakati Trump anasisitiza kuwa Marekani imeshinda vita ya uchumi na China, sasa inasonga mbele. Trump anakumbushia kuwa ni China ndiyo inahaha kufikia mwafaka, siyo Marekani. Wataalamu wanakiri kuwa katika mvutano wa uchumi kati na nchi hizo mbili ni Marekani iliyoshika mpini, lakini 'waliberali' wanasisitiza kuwa uchumi wa Marekani umepata pigo katika maeneo mengi, licha ya utawala wa Trump kukataa kuwa hali si shwari, ukaongeza misaada kwa wakulima walioathirika.

Rais Trump mapema mwaka huu ametangaza kuwa serikali yake itaweka kiasi cha dola bilioni 16 kusaidia ukanda wa kilimo nchini humo ule unaozalisha soya. Kwa sehemu isiyo ndogo ya uzalishaji kwa jumla walikuwa wanatemea soko la China. Hata hivyo inatazamiwa kuwa msaada huo ni wa mpito kwani kilimo cha Marekani ni cha mashamba makubwa sana, hivyo ni suala la kujipanga upya kuangalia nini kinafaa zaidi kulingana na uwezekano uliopo wa soko la China baada ya China kupandisha ushuru, na penginepo kuhamia kwingine kununua zao hilo.

Wakulima hao wanaweza kulima majani ya kulisha mifugo wakutumia wakati wa kipupwe.

Baadhi ya wataalamu, hasa wale wanaotambuliwa kuwa ni 'wahafidhina' wanasisitiza kuwa uchumi wa Marekani una vianzio vingi vyenye hali nzuri, hivyo ni kuongeza chumvi kuvumisha hofu kuwa mkwamo unakaribia.

Wanatoa kielelezo kuwa uchumi ulikua kwa asilimia 2.1 katika takwimu za mwisho wa robo mwaka, na hata katika takwimu hizo za soko la fedha zilizosababisha mjadala, wanunua hisa katika soko la New York ni kama vile walipuuza taarifa hizo na katikati ya wiki (iliyopita) mauzo ya hisa yalikuwa juu kwa zaidi ya asilimia moja kila sekta. Ni baada ya kuyumba kiasi fulani wiki mbili hivi zilizotangulia.

Wakati huo huo Rais Trump anatangaza azma ya kutaka kupunguza kodi kwa kampuni kwa idadi ya waajiriwa, ili kuongeza kasi ya ajira. Mapema mwezi uliopita, wakati wasiwasi kuhusu uchumi kuzorota ukifikia kilele, takwimu za miezi mitatu zikaonyesha kasi ya ajira viwandani na huduma tofauti imepanda hivyo kuvuruga kinachosemwa na wakinzani wa utawala wa Trump kuhusu uchumi.

Hofu ya mkwamo wa uchumi Marekani ilileta balaa katika soko la hisa Australia ambako ongezeko la thamani la takriban miezi miwili lilifutika hisa za dola za Marekani bilioni 60 'zilipoungua' hasa kutokana na wasiwasi huo.

Mzunguko wa taarifa za uchumi na jinsi zinavyopokelewa na vyombo vya habari ulionekana kwa kiasi fulani kuchangia kukua kwa wasiwasi huo, kwa mfano 'mnyauko' wa hisa soko la mitaji Australia ulifuata kushuka ghafla kwa thamani ya hisa soko la New York (nje ya vipengele vinavyochangia vya wasiwasi kuhusu uchumi wa Australia).

Mshtuko huo katika soko la hisa New York ulitokana na kupungua kwa uhitaji - na hivyo kiwango cha faida tarajiwa kilichopatikana - soko la Marekani, hali iliotafsiriwa kuwa inaashiria mkwamo wa kina wa uchumi.

Hali hiyo ilisababisha 'mnyauko' wa pointi 800 za thamani katika soko la hisa, na takwimu mpya kuhusu ajira miezi mitatu iliyopita zikafufua soko.

Labda cha kufurahisha kwa baadhi ya nchi za Afrika hasa zinazochimba madini kama dhahabu ni kuwa mikwamo ya hapa na pale katika thamani ya hisa za viwanda huwa inavuta mitaji au ununuzi wa hisa katika kampuni za nishati na madini, hivyo hisa za kampuni za dhahabu kupanda chati.

Hivyo wakati taarifa za mkwamo wa uchumi kwa kiwango fulani nchini Marekani, na kwa nguvu zaidi katika nchi kadhaa za Asia zinazotegmea zaidi soko la China, Afrika inaonekana kupata afueni kutokana na hitaji la hisa za madini kuwa kubwa zaidi kuliko viwanda na huduma tofauti.

Ni ishara kuwa madini yanaweza kuwa nyenzo halisi ya Afrika kuelekea uchumi wa viwanda, ikifikia makubaliano ya soko la pamoja ndani ya Afrika, mfumo unaoambatana na ushirikiano wa karibu zaidi na Umoja wa Ulaya, au China.

# Waomba mabati kujenga zahanati

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WANANCHI wa Kijiji cha Isyonje, Kata ya Isongole wilayani Rungwe wameiomba serikali kuwasaidia mabati kwa ajili ya kuezeka zahanati ya kijiji hicho, ili kunusuru mbao walizoweka juu ya jengo la zahanati hiyo kuharibika.

Ombi hilo limetolewa na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Isongole, Charles Salekwa, mbele ya Mbunge wa Jimbo la Rungwe, Sauli Henry, wakati akiwakabidhi msaada wa mabati 120 kwa ajili ya kuezeka sehemu ya jengo la zahanati hiyo.

Alisema jengo la zahanati ya kijiji hicho limejengwa kwa nguvu ya wananchi hadi kufikia hatua ya kupaua na sasa uwezo wa wananchi hao kuchangishana umepungua kutokana na hali duni ya uchumi walionayo, hivyo wanaiomba serikali kuwasaidia.

"Tulianza kujenga jengo la zahanati yetu kwa nguvu za wananchi na tumejitahidi mpaka tumepata mbao za kupaua, changamoto yetu ni ukosefu wa mabati ambayo kama tusiposaidiwa na serikali huwenda hata mbao tulizozipandisha juu ya jengo letu zikaharibika," alisema Saklekwa.

Alisema mbali na zahanati hiyo, wananchi wa Kijiji cha Isongole pia wanaendelea na ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa kwenye shule yao ya msingi ili kuwezesha wanafunzi wanaopaswa kuanza shule mwakani kupata mahali pa kusomea.

"Michango ya maendeleo kwa wananchi ni mingi kwani mpaka hivi sasa tunaendelea na ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa kwenye shule yetu, hivyo tunaomba tunapofikia hatua ya kupaua serikali itusaidie," alisema Salekwa.

Mbunge wa Rungwe, Sauli Amon, alisema ofisi yake itaendelea kushirikiana na wananchi kutatua changamoto zinazowakabili ili kuhakikisha maendeleo yanasonga mbele.

Hata hivyo, alisema changomoto ya uhaba wa mabati ataifikisha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ili ifanyiwe kazi, lakini wakati wakisubiri msaada wa serikali ameamua kuwapatia mabati 120 ili yasaidie kuezeka zahanati hiyo.

# Wanne mbaroni tuhuma za meno ya tembo 13

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali ambazo ni vipande 13 vya meno ya tembo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa hao walikamatwa kwa nyakati mbili tofauti.

Alisema katika tukio la kwanza waliwakamata watuhumiwa wawili Zungu Paulo 'Tinya' (45) na Baraka Lazaro 'Timotheo' (40) wote wakazi wa Kijiji cha Lupa wilayani Chunya ambao walikutwa na vipande vitatu vya meno ya tembo bila kibali.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa Agosti 19, mwaka huu, saa 2:00 usiku katika Kijiji cha Lupa wakiwa wamehifadhi pembe hizo kwenye mfuko wa sandarusi na kuzunguka navyo wakitafuta wateja mitaani.

Kamanda Matei aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Igelele Daniel (42) na Nyirenda John 'Daimon' (32) wote wakazi wa Kijiji cha Isangawana ambao walikutwa na vipande 10 vya meno ya tembo bila kibali.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa na Jeshi la Polisi Agosti 19, mwaka huu, majira ya saa 2:15 usiku katika nyumba ya kulala wageni iliyopo katika Kata ya Itewe wilayani Chunya.

"Thamani halisi ya nyara hizo bado haijafahamika, lakini tumebaini kuwa watuhumiwa hao wote ni wawindaji haramu na taratibu za kisheria zinaendelea kufanyika ili wafikishwe mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria," alisema Matei.

Alisema jeshi hilo linaendelea na msako katika maeneo mbalimbali mkoani humo kwa ajili ya kupambana na matukio ya uhalifu kuhakikisha mkoa huo, unakuwa salama.

Katika hatua nyingine, Matei alisema watu wawili wamefariki katika matukio mawili tofauti ya ajali akiwamo askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) MT.90399 CPL Fred Grayson, ambaye alifariki dunia baada ya gari yake kugongana uso kwa uso na lori.

Alisema ajali hiyo ilitokea juzi usiku katika eneo la ZZK Mji Mdogo wa Mbalizi, ambapo askari huyo ambaye alikuwa anaendesha gari namba za usajili T. 219 CSU akitokea katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe kuelekea Mbeya Mjini aligongana na lori namba T.838 APZ.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni marehemu ambaye alikuwa anafanya kazi katika Kikosi cha 44KJ kilichopo Mbalizi kutaka kulipita gari lililokuwa mbele yake bila kuchukua tahadhari na ndipo akakutana uso kwa uso na lori hilo.

Hata hivyo alisema dereva wa lori hilo lililokuwa linatokea Mbeya Mjini kuelekea Tunduma alikimbia na kutokomea kusikojulikana, huku akilitelekeza gari katika eneo la tukio.




Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, SACP Ulrich Matei, akionyesha kwa waandishi wa habari jijini humo jana, baadhi ya vipande vya meno ya tembo, ambavyo watuhumiwa wanne walikamatwa navyo wilayani Chunya. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Sababu idadi ya wasiojua kusoma, kuandika kupungua

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

IDADI ya wanafunzi wasiojua kusoma wala kuandika imepungua mwaka mmoja uliopita kutokana na serikali kuongeza mkazo katika kuhakikisha walimu wanatekeleza majukumu yao ipasavyo.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Emmanuel Kishimbo, aliyasema hayo alipokuwa akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo.

Alisema changamoto ya wanafunzi kutokujua kusoma na kuandika katika halmashauri hiyo, ilikuwa kubwa katika miaka michache iliyopita, lakini baada ya halmashauri kujiwekea mikakati ya kuhakikisha walimu wanatimiza vema wajibu wao, idadi ya wanafunzi wasiojua kusoma wala kuandika imeanza kupungua kwa kasi.

"Wanafunzi wasiojua kusoma wala kuandika kuanzia darasa la awali hadi darasa la saba imepungua kwa asilimia 89.5 mwaka mmoja uliopita kutokana na jitihada za Idara ya Elimu kuhahakikisha walimu wote wanatimiza wajibu wao wa kufundika," alisema Kishimbo.

Hata hivyo Kishimo alisama pamoja na mafanikio hayo Wilaya ya Mbarali bado inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa walimu 381 kuanzia darasa la awali hadi darasa la saba, upungufu wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu.

Alisema pia ipo changamoto ya baadhi ya wanafunzi kutohitimu masomo katika ngazi ya darasa la saba kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utoro na mimba za utotoni.

Alisema ili kukabiliana na changamoto hizo, Idara ya Elimu itaendelea kuhamasisha wananchi kujenga vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu sambamba na kutoa taarifa za upungufu wa watumishi kwenye mamlaka husika ili hatua zichukuliwe.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alisema katika mwaka ujao wa fedha halmashauri yake imejipanga kuboresha sekta ya elimu ikiwamo kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu.

Alisema halmashauri yake ina mpango wa kuongeza vyumba vya madarasa kwa kuhamasisha wananchi kujenga maboma ya kutosha na halmashauri kuyakamilisha ili yatumike kutatua tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Francis Mtega, aliwataka watendaji wa halmashauri hiyo, kuongeza bidii ili kuhakikisha changamoto ambazo zimejitokeza kwenye mwaka wa fedha uliomalizika zipatiwe ufumbuzi mara moja mwaka huu.





## Wapewa elimu ufugaji kuku

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WANANCHI wameshauriwa kuanzisha miradi ya ufugaji kuku, ili kujikwamua kiuchumi kutokana na kuwa na faida nyingi.

Meneja Masoko wa AKM Giltters Ltd ya kusambaza na kuzalisha vifaranga vya kuku aina ya Kuroila F1, Dofrian John, alisema hayo jana alipozungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu kwa wafugaji kuku na mawakala wa kusambaza vifaranga kutoka Kanda ya Kati, yaliyofanyika jijini hapa.

John alisema kama wananchi watafanya uwekezaji kwenye miradi hiyo wataweza kuongeza vipato vya familia na kufanya uwekezaji kwenye maeneo mengine.

"Tunalalamika hakuna ajira lakini watu wanashinda vijiweni, tufuge kuku ni rahisi si lazima uwe na shamba kubwa kufanya ufugaji huo, unaweza kuanza na hata chumba kimoja kufuga kuku," alisema.

Aidha, alisema zaidi ya watu 160,000 na mawakala 420 wa ufugaji kuku aina ya Kuroila F1 inayosambazwa na kampuni hiyo na wamenufaika ufugaji huo kwa kuongeza uchumi.

Aliitaja mikoa iliyopata mafunzo hayo kuwa ni Tabora, Kigoma, Singida, Dodoma, Kigoma na Katavi.

John alisema kampuni hiyo ina uwezo wa kuzalisha vifaranga 100,000 kwa siku na uhitaji wa vifaranga katika soko ni mkubwa kiasi kwamba wameona watoe elimu ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo ni endelevu na yalianza mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Njombe, Mbeya, Iringa, Songwe, Rukwa na Ruvuama.

Kwa mujibu wa meneja huyo baada ya Kanda ya Kati, mafunzo hayo yataendelea kwa Kanda ya Ziwa yenye mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita, Mara na Kagera.

Aliitaja kanda nyingine kuwa ni Kaskazini yenye Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga na watamalizia na Kanda ya Pwani yenye Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Morogoro, Mtwara na Zanzibar.

# Mpango wa IPOSA kuandikisha vijana 10,000

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameitaka mikoa minane nchini ambayo iko katika majaribio ya kutekeleza mpango wa elimu changamani kwa vijana walio nje ya shule (Iposa) kuhakikisha hadi Agosti 30, mwaka huu, iwe imeandikisha vijana 10,000.

Aidha, amewataka wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha hadi Desemba, mwaka huu, walimu wote waliosomea elimu maalum wanahamishwa na kupelekwa katika shule hizo au shule jumuishi.

Jafo alisema hayo juzi katika kikao cha ofisa elimu wa mikoa, elimu ya watu wazima na wa elimu maalum wa halmashauri nchini kinachofanyika jijini hapa.

Alisema kwa sasa tayari wameshaandikisha vijana 8,010 hivyo wahakikishe wanafikia lengo lililowekwa katika wakati ulipangwa.

Waziri huyo alisema Machi, mwaka huu, serikali ilizindua mpango wa Iposa kwa majaribio katika vituo 72 kwenye mikoa minane ambayo ni Kigoma, Tabora, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe.

Jafo alisema matarajio ya mpango huo ni kuandikisha vijana 10,000 ambao watasoma kwa kipindi cha miezi 18 kukamilisha mzunguko wa mafunzo.

"Hadi Julai 15, mwaka huu, tayari vijana wapatao 8,010 walishaandikishwa, hivyo tunatarajia hadi Agosti 30 matarajio yawe yamefikiwa," alisema Jafo.

Pia Jafo aliwataka wakurugenzi kutenga fedha kwenye kifungu cha OC kwa ajili ya shughuli za elimu ya watu wazima na elimu maalum na kusisitiza kuwa kuanzia bajeti ijayo, halmashauri ziainishe fedha hizo ilivyo kwenye fedha za asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Jafo alisema mwaka 2018 serikali ilibainisha watoto wenye mahitaji maalum wa umri kati ya miaka minne hadi sita katika kata 2,723 sawa na asilimia 68.8 ya kata zote nchini. Watoto 16,463 walibainika kuwa na mahitaji maalum kwa viwango tofauti ya uhitaji maalum au ulemavu.

Kuhusu kuhamishwa walimu hao, aliagiza uhamisho huo ufanyike huku ukihakikisha wahusika wanalipwa gharama za uhamisho bila ya kulimbikiza madeni.

Kuhusu hali ya uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Jafo alisema unaendelea kuongezeka kwa ngazi zote, ambapo mwaka 2016 wanafunzi walioandikishwa elimu ya awali walikuwa 2,389, huku 2019 wakiandikishwa wanafunzi 3,490 sawa na ongezeko la asilimia 46.1.

Aidha, alisema upande wa elimu ya msingi 2016 waliandikishwa wanafunzi 37,055 na mwaka 2019 waliandikishwa wanafunzi 49,655 sawa na ongezeko la asilimia 34, huku elimu ya sekondari mwaka 2016 waliandikishwa wanafunzi 6,167 na mwaka 2019 waliandikishwa wanafunzi 10,751 sawa na asilimia 74.6 na kusisitiza ni ongezeko kubwa.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wakulima Tanzania (TASO), Luten mstaafu Shabani Muyombo (kushoto), akizungumza wakati wa kufungua kikao cha Kamati Kuu ya Jumiya hiyo, kilichofanyika jana, jijini Dodoma na kumwomba Waziri wa Kilimo na Chakula, Japhet Hasunga, kuwarudishia mali zao baada ya kurudishiwa usajili wao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Waziri ataka wajasiriamali ngozi kutambuliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeliagiza Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kusaidia wajasiriamali wanaohitimu mafunzo kupata vyeti vya utambuzi.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alisema hayo jana wakati wa ziara ya kufuatilia utendaji kazi wa Sido jijini Dodoma.

Alisema ni vyema mafunzo yanayotolewa na shirika hilo yafanyike kwa ushirikiano na DIT ili wahitimu wapate vyeti vya utambuzi ambavyo vitawasaidia kujulikana na taasisi zingine wanapokwenda kuomba ajira.

Alisema lengo lao ni kuona vijana wanapata ujuzi wa kina kinadharia na kuwakuza katika utengenezaji wa bidhaa za ngozi hadi hatua ya mwisho.

"Unaweza kuwa na ujuzi lakini huna cheti cha utambuzi. Kwa hiyo shirikianeni na DIT ambao wanatambulika ili kuanza utaratibu wa wahitimu wa Sido kupata vyeti vya utambuzi," alisema.

Aliitaka Sido kufanya mikakati ya kuzungumza na DIT kuona namna ya kushirikiana kwenye jambo hilo ili kuleta tija kwa washiriki wa mafunzo mbalimbali yanayotolewa.

"Siku hizi vijana wana mtindo wa kuulizana ujuzi umepata chuo gani kwa hiyo akiona una cheti cha DIT anakuelewa haraka," alisema Manyanya.

Alibainisha kuwa vyeti hivyo vitawasaidia kupata kazi mbalimbali kwenye kampuni au taasisi zinazohitaji bidhaa za ngozi.

Aidha, aliipongeza Sido Dodoma kutokana na utendaji mzuri walioonyesha husussani katika ujenzi wa kituo cha ngozi ambacho hutumika kwa ajili ya kufundishia wajasiriamali.

Naye Meneja wa Sido Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, alisema eneo hilo linatumika kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wa bidhaa za ngozi na pia kuna majengo matatu ya mpya ambayo yanatarajiwa kutumika kwa ajili ya wajasiriamali wa bidhaa mbalimbali.



HABARI ZANZIBAR

# Rais Shein aipa jukumu Wizara ya Ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, ameutaka uongozi wa Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati kuvitumia vyombo vya habari kuyatangaza mafanikio iliyoyapata ili wananchi wapate kuyajua.

Dk. Shein alitoa agizo hilo alipokutana na uongozi wa wizara hiyo, wakati ilipowasilisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Julai 2018 hadi Juni 2019 na Mpango Kazi wa Utekelezaji kwa mwaka 2019/2020.

Alisema serikali ni ya wananchi na ipo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi, hivyo ni vyema wakapewa taarifa zote kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali na hasa zile zinazogusa maisha yao ya kila siku.

Dk. Shein pia aliupongeza uongozi wa wizara hiyo kwa kuwasilisha vyema mpango kazi wao na kueleza kufarajika kwake kutokana na matumizi katika wizara za serikali kwa kutambua kuwa tatizo hivi sasa sio fedha bali ni matumizi.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina fedha za kutosha kukidhi mahitaji ya bajeti za wizara zake kutokana na makusanyo mazuri yanayofanywa na taasisi husika zinazokusanya mapato zikiwamo Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Dk. Shein alieleza kuwa serikali inajitahidi kutekeleza wajibu wake katika kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza mambo yake ikiwamo miradi ya maendeleo jambo ambalo limeleta faraja katika kutekeleza mipango ya nchi.

"Yapo mafanikio mengi yamepatikana katika miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya wizara hii ikiwa ni pamoja na mambo yote manne na hivi karibuni limeingia la tano la mafuta na gesi asilia hivyo nina imani kwamba mafanikio makubwa yatapatikana sasa ni vyema tukayatangaza, tukawaambia wananchi wetu ili wayajue," alisema Dk. Shein.

Naye Waziri wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, Salama Aboud Talib, alisema wizara hiyo inaendeleza juhudi na mikakati ya serikali ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora za maji, nishati iliyo salama na endelevu, makazi bora pamoja na matumizi mazuri ya ardhi.

Alisema wizara yake kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), imeendelea kusimamia shughuli za programu za uhaulishaji na upanuzi wa shughuli za maji mijini na usambazaji maji vijijini.

Alisema kupitia mradi huo imefanikiwa kulaza mabomba kwa masafa ya kilomita 87.1 katika maeneo ya Bumbwisudi, Kizimbani, Kianga, Welezo, Mikunguni, Mwembemakumbi, Makadara, Mwembeladu, Rahaleo, Miembeni, Mkunazini na maeneo ya Mji Mkongwe.

Alisema wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA), imeendeleza juhudi za kuimarisha mazingira bora ya utendaji wa kazi kwa kutekeleza shughuli za ujenzi wa jengo la ofisi Maisara na hadi kufikia Juni 2019, umekamilika kwa asilimia 60.

Pia wizara hiyo pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zilikamilisha majadiliano na Kampuni ya RAKGAS kwa kitalu cha Pemba-Zanzibar na hatimaye Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia, ilitia saini mkataba wa kwanza wa mgawanyo wa uzalishaji wa mafuta na gesi asilia Oktoba 28, 2018.

Mkataba huo kwa maelezo ya waziri huyo, unajumuisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kampuni ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar na Kampuni ya RAKGAS kutoka Ras al Khaimah.

"Kazi za utafiti wa nishati ya mafuta na gesi zinaendelea kupitia kampuni ya RAKGAS na taarifa zote kuhusu kuwapo kwa nishati ya mafuta na gesi tutapewa taarifa zake kikamilifu baada ya kukamilika kwa kazi za utafiti," alisema.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kulia), akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti na mpango kazi wa wizara yake kwa mwezi wa Julai 2018 hadi Juni 2019, wakati Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), alipozungumza na uongozi wa wizara hiyo, Ikulu juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Castico awatahadharisha waomba mikopo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, amewataka wajasiriamali wanaoomba mikopo katika mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kuitumia mikopo hiyo kwa kufanya matumizi yaliyomo katika mipango ya biashara.

Akizindua mafunzo ya wajasiriamali waliopata mikopo, alisema ili kuepuka kufa kwa biashara ni vyema kufanya matumizi kwa mujibu wa mipango ya biashara iliyowekwa.

"Ombi langu kwenu ni kuhakikisha kuwa mnatumia ipasavyo fedha za mkopo kwa kufanya matumizi yaliyomo katika mipango ya biashara yenu, kwa kuwa tunaambiwa na wataalamu kuwa asilimia 90 ya biashara zinzokufa hutokana na wajasiriamali kufanya matumizi kinyume na maelekezo ya mipango yao ya biashara," alisema.

Vile vile, alieleza kuwa kitu cha msingi katika biashara ni kutathmini biashara kila baada ya kipindi maalum, kwa kuwa kufanya hivyo kutakuwa na uelewa kwa kiasi gani biashara imefikia malengo yaliyokusudiwa.

"Mnapotathmini maendeleo ya biashara zenu mnakuwa mmepata wasaa wa kupima utekelezaji wa malengo yenu ya biashara na kujua wapi mmefikia, kipi mmeweza, wapi mmeteleza na nini mfanye ili kuimarisha biashara zenu," alisema.

Alisema, shughuli za ujasiriamali ni sehemu muhimu ya kutengeneza ajira kwa wananchi, hivyo ni muhimu kuwa na biashara imara zinazotoa huduma bora kiushindani na ndio maana kumekuwa kukitolewa mafunzo mbalimbali ili kufikia malengo.

Alisema Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi una taratibu na kanuni zake ili kupata mikopo hivyo ni lazima kila mjasiriamali anayetaka mkopo azifuate kwa kuwa hakuna njia ya mkato.

Alizitaja taratibu hizo kuwa ni pamoja na kupitia kwa sheha wa eneo husika, kukaguliwa na maofisa mikopo, kufanyiwa tathmini na kamati ya mikopo na kupitishwa na bodi ya mfuko.

Naye Mkurugenzi wa Mfuko wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Suleiman Ali Haji, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwaandaa wajasiriamali kwa kuwajengea uwezo utakaowawezesha kufanya shughuli zao za kibiashara na uzalishaji kwa ufanisi zaidi baada ya kupatiwa mtaji.

Alisema, mfuko huo unatoa mikopo nafuu na isiyo na riba kwa wajasiriamali, anachotakiwa ni kuchangia pesa kidogo kabla ya kupata mkopo.

# Wizara ya Elimu yaendelea kupitia mitaala

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kupitia Taasisi ya Elimu, inaendelea kupitia mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi ili kuhakikisha Zanzibar inakuwa na elimu bora.

Akizungumza wakati akifungua warsha ya kupitia mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wadau wa Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Suleiman Yahya Ame, alisema kuandaa mtaala ni muhimu kwa kuwa unasaidia kupata viwango bora vya elimu kwa wanafunzi.

Aliwataka kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kupata mtaala bora wa elimu pamoja na kuangalia mitazamo tofauti ili kupunguza tatizo la masomo mengi katika ngazi ya maandalizi na msingi.

Aliwashauri wadau hao kuwa na tahadhari wakati wanapopunguza masomo kwa kuepuka kutoa somo lililokuwa na umuhimu na kuwataka wakati wa kuipitia ripoti kutoa michango mizuri ili kupata mtaala ulio bora kwa taifa.

Mkuu wa Divisheni ya Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi, Abdallah Mussa, alisema ripoti hiyo imeandaliwa kwa kushirikiana na taasisi hiyo pamoja na Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais Ikulu na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Idara maalum na vikosi vya SMZ.

Alisema katika mtaala huo baadhi ya maoni yaliyotolewa yameeleza kuwa mtaala ni mrefu na hivyo ripoti hiyo itatumika vyema kufafanua ulio bora.

# Wasusi wapewa mikopo bila dhamana, elimu ujasiriamali

**Na Enock Charles**

WASUSI wa nywele Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wamepata fursa ya kukuza mitaji yao kwa kupewa mikopo isiyo na dhamana pamoja na elimu ya ujasiriamali.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa semina maalum ya wasusi iliyoitwa 'Ususi ni Ajira', juzi jijini humo, ikiratibiwa na Kampuni ya KopaFasta inayotoa mikopo hiyo, Katibu Tawala kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Judith Elius, aliyemwakilisha mkuu wa wilaya hiyo akiwa mgeni rasmi, alisema hatua hiyo inaakisi kuunga mkono juhudi za serikali katika kuwakwamua kiuchumi wananchi na kuipeleka Tanzania katika uchumi wa kati.

Aidha, Elius aliwataka wasusi kuchangamkia fursa hiyo na kutambua kuwa 'ususi ni ajira', na kwamba mikopo inayoambatana na elimu ni suluhu ya changamoto iliyokuwa inawakabili wengi wao wasiokopesheka.

"Wasusi wanapaswa kuwa na mwitikio chanya katika fursa hii ya mikopo na elimu ya ujasiriamali. Na kwa kuwa tumeshirikishwa kwa nia njema, sisi kama serikali tutahakikisha kuwa kila mwenye uhitaji katika kundi hili anapata," alisema Bi. Elias.

Alizitaka kampuni nyingine kuiga mfano wa kampuni hiyo ambayo masharti yake ya kutoa mkopo ni mwombaji kuwa na kitambulisho cha taifa pamoja na sehemu ya kufanyia kazi yake ya usus.

Meneja wa kampuni hiyo, Patrick Kang'ombe, alisema kuwa lengo la kutoa mikopo bila kuwa na dhamana ni kuwawezesha Watanzania wengi wasio na mali, ambao walikuwa wanachukuliwa kuwa hawakopesheki, lakini wana mtaji wa vipaji vya kipekee.

"Kuna wasusi ambao wamekuwa wakisukia majumbani au hata chini ya miti, ambapo mvua ikinyesha hawawezi kufanya kazi. Ni lazima tuwaboreshee mazingira yao, wakuze mitaji na kuchangia pato la Taifa," alisema Kang'ombe.

Alisema kupitia KopaFasta, mbali na wasusi, wameshayafikia makundi mengine ya wasanii kama wachoraji na wachonga vinyago ambao dhamana yao kuu ni uaminifu na utambulisho wao. Aliongeza kuwa makundi haya yamekuwa hayakopesheki kupitia mfumo wa kibenki uliopo kutokana na wengi wao kushindwa kukidhi vigezo vya kuwa na dhamana ya mali.

Rais wa Shirikisho la Sanaa za Ufundi Tanzania (TAFCA), Adrian Nyangamalle, alisema sekta ya sanaa na burudani ni muhimu kwa uchumi wa Taifa, kwani takwimu iliyotolewa bungeni wakati wa uwasilishaji wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilionyesha kuwa hii ndiyo sekta iliyokuwa kwa kasi zaidi ikiwa ni asilimia 13.7, yaani zaidi ya sekta ya ujenzi.

Katika semina hiyo iliyolenga wasusi 500, wawezeshaji kuhusu elimu ya ujasiriamali na saikolojia Chris Mauki, Charles Nduku na Meneja wa Chama cha Urembo na Vipodozi (TCA), Judith Charles walitoa mada.

Wakizungumza baada ya semina hiyo, wasusi hao walieleza kuwa wamefaidika na mafunzo waliyoyapata pamoja na fursa ya mikopo.

"Sasa tumepata fursa ya kutatua changamoto ya mitaji iliyokuwa inatukabili kwa kuwa hatukuwa tunakopesheka kwa kukosa dhamana ya mali, lakini pia tunashukuru Kampuni ya KopaFasta kwa kutupatia elimu ya jinsi ya kutumia mikopo tunayopewa ili tukuze mitaji na kujikwamua kiuchumi," alisema Hilda Adam, mmoja wa washiriki na mnufaika wa mkopo huo.




Sehemu ya Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Suka, jijini Dar es Salaam, likiwa na mwonekano mzuri kutokana na ujenzi unaoendelea wa upanuzi wa barabara hiyo, kuwa njia sita. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TTB yaweka nguvu kutangaza India, China

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB), imesema imejipanga kuongeza kasi ya kutangaza vivutio vya utalii katika nchi mbalimbali duniani hususan kwa kuwekeza nguvu zaidi kwa sasa katika masoko kwenye nchi za India na China.

Imesema imewekeza nguvu kubwa katika kutumia mawakala kutoka nchi ambazo wamelenga kutangaza vivutio hivyo ambao watakuwa wanasambaza taarifa za vivutio mbalimbali vya Tanzania.

Pia imesema katika tamasha la utalii linalotarajia kufanyika Oktoba 18 hadi 20 mwaka huu, wamejipanga kuongeza nguvu ya kutangaza vivutio mbalimbali vilivyopo katika nchi kwa ajili ya kuendelea kuongeza zaidi idadi ya watalii.

Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Devotha Mdachi, alisema nchi 60 zitashiriki katika tamasha hilo na kwamba maandalizi ya kupokea ugeni huo yamekamilika ambayo yanafanywa kwa kushirikiana na TTB na Balozi katika nchi husika.

"Mpaka sasa tumepokea uthibitisho kutoka ofisi za ubalozi toka nchi mbalimbali zikiwamo Ubalozi wa Sweden, Malaysia, China, Korea ya Kusini, Japan, Canada, Afrika Kusini, Oman, India, Uingereza, Brazil," alisema Mdachi.

Mdachi alitaja maeneo ambayo wamejipanga kuboresha zaidi kwa ajili ya kuwapeleka watalii watakaoshiriki katika tamasha hilo ni hifadhi ya Serengeti, Udzungwa, Mikumi, fukwe za Tanga, mapango ya Amboni, Mlima Kilimanjaro, miradi ya utalii wa utamaduni.

# Waziri Jafo aitaja NMB kwa mafanikio serikalini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imeitaja benki ya NMB kuwa miongoni mwa taasisi zilizofanikisha makusanyo ya fedha kwa mwaka 2018/19, kwa kuwa benki hiyo haina tofauti na Wizara ya Tamisemi kwa kufika maeneo yote nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Selemani Jafo, wakati akizungumza na walimu zaidi ya 300 kutoka halmashauri za wilaya mkoani Dodoma katika 'Siku ya Mwalimu' ambao walikutanishwa na benki ya NMB.

Waziri Jafo alisema uamuzi wa benki hiyo kwenda nchi nzima na kufungua matawi, mawakala pamoja na kuongeza ATM, ulisaidia kwa watu kuzifikia kwa urahisi huduma za kibenki pamoja na halmashauri kuitumia kwa makusanyo yake.

Hivi karibuni Jafo alitangaza mapato ya serikali kutoka katika halmashauri yakipanda kutoka asilimia 73 ya mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 81 mwaka 2018, juzi kwenye mapato katika mamlaka ya serikali za mitaa tumekusanya takriban Sh. bilioni 664 sawa na asilimia 91 kiasi ambacho hakijawahi kufikiwa. Ninyi NMB mmetusaidia kwa hili," alisema Waziri Jafo.

Alisema benki hiyo ni miongoni mwa taasisi zinazofanya vizuri hapa nchini ikiwa na wateja zaidi ya 3.5 milioni pamoja na matawi 229 ambayo ni zaidi ya halmashauri zilizopo ingawa aliwataka waongeze wateja na kuagiza kitengo cha utafiti kufanya kazi yake vizuri.

Kuhusu mikopo, alisema kuna kilio kutoka kwa watumishi kuhusu riba kubwa ya mikopo kwenye benki zote nchini kwani wanatoza kiwango ambacho si rafiki kwa wafanyakazi jambo linalosababisha malalamiko na wengine kujutia uamuzi wa kukopa.

"Naomba suala la riba mliangalie, haiwezekani riba ya mfanyakazi ikawa sawa na anayefanya biashara, ndiyo maana mnasababisha walimu kuingia madeni kwenye Saccoss nyingine hadi wanaacha kadi zao huko, mwisho wa siku wengine wanataka kujinyonga, tafakarini ikibidi mfike hata kwenye single digit," alisema Jafo.

Katika hatua nyingine, aliwataka walimu kutumia mishahara yao kwa utaratibu na kuacha maisha ya kuiga kwani ndiyo yanayowapelekea kwenye madeni makubwa.

Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Solo Mlozi, alisema benki hiyo imejipanga kuwafikia Watanzania mahali walipo kwa kutumia mawakala wake na kuendelea kuboresha huduma zao kwa kadri iwezekanavyo.

# Museveni, Kagame wasaini kumaliza 'bifu'

**LUANDA,** Angola

MARAIS Yoweri Museveni wa Uganda na Paul Kagame wa Rwanda wamesaini makubaliano ya amani katika Mji Mkuu wa Angola, Luanda kumaliza uhasama uliopo kati ya mataifa hayo jirani.

Hatua hiyo imeleta afuani na furaha kubwa kwa raia wa nchi hizo, husussani wafanyabiashara.

Wakuu hao wa nchi walifikia makubaliano hayo katika mkutano wa pili huko Luanda mbele ya marais wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Angola na rais wa Congo Brazaville waliokuwa wapatanishi katika mgogoro huo.

Joto la kisiasa limekuwapo tangu mwanzoni mwa mwaka huu na limeathiri maisha ya watu kijamii na kiuchumi katika mataifa hayo jirani.

**Ni madai yasiyo na msingi. Lakini haya yote yanaonyesha ushirikiano wa dhati uliyopo baina ya serikali ya Uganda na kundi la RNC.**

Maofisa nchini Rwanda wameishutumu Uganda kwa kuwafunga na kuwatesa kinyume cha sheria raia wake nchini Uganda, wakati Uganda nayo inaishutumu Rwanda kutekeleza ujasusi katika ardhi yake.

Baada ya kuingia makubalinao hayo, Rais Kagame aliwaeleza waandishi wa habari kuwa: "Tutashughulikia matatizo haya yote".

Makubaliano hayo yalifikiwa baada ya jitihada zilizoidhinishwa na Angola kwa usaidizi wa DR Congo.

Shirika la Habari nchini Angola, Angop liliripoti kuwa viongozi hao wamekubaliana kutilia mkazo kutatua mzozo wowote baina ya mataifa yao kwa njia amani.

Machi mwaka huu katika hotuba yake kwenye mkutano wa kitaifa, Rais wa Rwanda Paul Kagame alieleza kuwa chimbuko la mgogoro baina ya nchi yake na nchi ya Uganda ni la tangu miaka 20 iliyopita nchi ya Uganda ikitaka kuangusha utawala wake.

Rais Kagame alisema mgogoro huo ulishika kasi hivi karibuni kufuatia wananchi wa Rwanda wanaoingia nchini Uganda au kufanyia kazi nchini humo kushikwa na kuzuiliwa sehemu ambazo hazijulikani na kufanyiwa vitendo vya mateso.

Rais Kagame amekuwa akiushutumu utawala wa Uganda kutoa nafasi ya ushirikiano kwa kundi la Rwanda National Congress linaloongozwa na Mkuu wa zamani wa majeshi ya Rwanda jenerali Kayumba Nyamwasa.

"RNC wanafanya kazi kwa ushirikiano na vyombo vya usalama vya Uganda. Kilicho wazi ni kwamba wanachokifanya ni kunyanyasa Wanyarwanda ambao hawataki kuungana nao huku wakiwasingizia kwamba wametumwa na utawala wa Kigali kuhujumu usalama wa Uganda na kuwa wanyarwanda wa upinzani," alisema Rais Kagame na kuongeza.

"Ni madai yasiyo na msingi. Lakini haya yote yanaonyesha ushirikiano wa dhati uliyopo baina ya serikali ya Uganda na kundi la RNC".

Uganda imekuwa ikiishutumu Rwanda kuwatuma majasusi na kufanyia vitendo vya ujasusi kwenye ardhi yake, shutuma ambazo Rwanda imekanusha.

Rais Kagame amesisitiza kwamba mara kadhaa mwenyewe aliwasilisha malalamiko hayo kwa mwenzake Yoweri Museveni na kwamba hakuonyesha utashi wowote wa kuyatatua.

Katika ishara nyingine ya kuonekana ya kingia doa kwa uhusiano baina ya nchi hizo jirani, Mei mwaka huu Uganda na Rwanda zilishutumiana kwa mauaji na utekaji nyara wa raia wa kutoka mataifa hayo mawili.

Kutokana na uhasama huu, Rwanda imeamua kufunga mpaka wake na Uganda wa Gatuna kwa usafiri wa bidhaa. **BBC**



Rais wa Uganda, Yoweri Museveni (kushoto), akipeana mkono na mwenzake wa Rwanda, Paul Kagame wakati wa makubaliano ya kuondoa uhasama kati yao yaliyosaini Angola. **PICHA: REUTERS**

## Johnson aenda kukutana na Macron

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, anatarajia kuzuru Ufaransa ikiwa ni siku moja baada ya Kansela wa Ujerumani Angela Merkel kumpa matumaini ya kufikia muafaka kuhusu mchakato wa Uingereza kuondoka katika Umoja wa Ulaya(EU).

Katika mkutano wake na Merkel uliofanyika juzi, viongozi hao walisema wanataka kuepusha Brexit bila makubaliano, ingawa wanatofautiana juu ya namna ya kufanikisha suala hilo.

Lakini Johnson huenda akakumbana na hadhira ngumu zaidi mjini Paris kuliko ilivyokuwa Berlin.

Juzi, Rais Macron alitupilia mbali mapendekezo ya Johnson kuutaka EU kufungua tena majadiliano kuhusu mpaka wa Ireland, akisema kanda hiyo imeweka wazi wakati wote kwamba haitakubali hilo, aliwaambia waandishi habari mjini Paris kwamba mapendekezo ya Uingereza kujadili upya vipengele vya mkataba ni suala lisilokuwapo.

Leo viongozi hao watatu wa Ulaya wanatarajiwa kukutana na Rais wa Marekani, Donald Trump, muungaji mkono mkubwa wa Brexit na Johnson, pamoja na viongozi wa Canada, Italia na Japan kwenye mkutano wa kilele wa mataifa saba yalioendelea zaidi duniani G7, katika mji wa Biarritz nchini Ufaransa.

Mazungumzo hayo yanakuja baada ya Merkel kumueleza Johnson kwamba makubaliano yanaweza kufikiwa ndani ya siku 30, ikiwa suluhisho litapatikana kuhusu suala gumu la mpaka wa Ireland.

"Kuna masuala mawili ambayo yote ni muhimu: Moja ni, Uingereza inataka kuondoka EU. Lingine ni kwamba makubaliano ya Good Friday lazima yazingatiwe. Hii halitoki Uingereza pekee, bali pia mwanachama wa EU Ireland," alisema Merkel. **DW**

## Spika aongoza bunge amempakata mtoto

**WELLINGTON,** New Zealand

SPIKA wa Bunge New Zealand, Trevor Mallard, ameonekana akimpakata mtoto wa mmoja wa wabunge akiongoza mjadala katika bunge hilo la wawakilishi.

Mallard (pichani) aliweka picha akiwa amempakata mtoto wa kiume wa mbunge T mati Coffey katika mtandao wake wa kijamii waTwitter.

Coffey, ambaye ni mbunge wa Labour wa eneo la Waiariki, alitangaza kuzaliwa kwa mtoto wake, T t nekai Smith-Coffey, Julai, mwaka huu.

Siku ya Jumatano Coffey alihudhuria vikao vya bunge na mwanawe kwa mara ya kwanza baada ya kurejea kazini kutoka likizo ya uzazi.

Wakati wa kikao hicho Spika Mallard alichukua jukumu la kumpakata mtoto pamoja na jukumu la spika.



Picha hiyo ya Coffey akiwa amembeba mtoto bungeni iliwekwa na mbunge wa chama cha Green Gareth Hughes kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter.

"Inapendeza sana kuwa na mtoto bungeni, hii ni kwa kweli ni nzuri sana," Hughes aliandika.

Akizungumza tukio hilo Coffey alisema "Napata usaidizi kutoka kwa wafanyakazi wenzangu wote bungeni".

Coffey ni mbunge wa kwanza kumpeleka mtoto wake bungeni, na kufuata mfano wa wanasiasa wengine duniani.

Lib Dem kiongozi wa Jo Swinson, ambaye alihudhuria vikao vya bunge na mtoto wake mwaka 2018, na Seneta wa Australia Larissa Waters, ambaye alimnyonyesha mwanawe bungeni mwaka 2017.

September mwaka jana Waziri mkuu wa New Zealand, Jacinda Ardern aliandikisha historia kwa kuandamana na mtoto wake wakati akitoa hotuba yake ya kwanza katika mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN) mjini New York Marekani. **BBC**

# Waziri Mpina avunja rasmi Bodi ya Maziwa

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amevunja Bodi ya Maziwa nchini kutokana na kutoridhishwa na utendaji wake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa wizara hiyo, Rehema Mbulalina, bodi hiyo imevunjwa kutokana na utendaji usioridhisha.

"Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kwa mamlaka aliyonayo kisheria chini ya Sheria ya Bodi ya Maziwa Na. 8 ya Mwaka 2004, kifungu cha 8 na 9(1), ameivunja Bodi ya Wakurugenzi ya Maziwa Tanzania.

"Hii ni kutokana na kutoridhishwa na utendaji wa bodi. Imevunjwa kuanzia Agosti 22, 2019," ilieleza katika taarifa hiyo ya wizara.

Juni Mosi, mwaka huu, wakati wa maadhimisho ya 22 ya kilele cha Wiki ya Maziwa Duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Arusha, Mpina alisema Tanzania licha ya kuwa na mifugo mingi na kushika nafasi ya pili barani Afrika kwa wingi wa mifugo, uzalishaji wa maziwa nchini ni duni.

Katika maadhimisho hayo, Mpina alisema uzalishaji wa maziwa nchini haulingani na uzalishaji wa baadhi ya nchi jirani licha ya kuwa na maeneo mazuri ya malisho tofauti na nchi hizo.

Mpina alizitolea mfano Kenya ambayo inazalisha maziwa lita bilioni 5.6 na Uganda lita bilioni 2.7, huku Tanzania ikizalisha lita bilioni 2.2 kwa mwaka licha ya kuwa na maeneo mazuri ya malisho.

Alisema serikali inaendelea kuhakikisha uzalishaji na usindikaji wa maziwa unaongezeka na kudhibiti mipaka yote ambayo ilikuwa inapitisha maziwa kutoka nje bila kukaguliwa.

Mpina alitoa maelekezo kwa Bodi ya Maziwa kwamba ifikapo Julai 30, mwaka huu, ihakikishe mwananchi yeyote atakayehitaji mtamba, asikose na ikiwezekana iagize mitamba kutoka nje ya nchi.

Waziri huyo pia aliitaka bodi hiyo kujadili bei halisi ya maziwa nchini.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza wakati wa kufungua mkutano wa walimu uliondaliwa na Benki ya NMB, jijini Dodoma, jana. Habari Uk. 24. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Magufuli ateta na mabalozi 43 Ikulu

**Na Mwandishi Wetu**

MABALOZI wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani wampongeza Rais Dk. John Magufuli kwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inajengwa kwa fedha za Watanzania.

Mabalozi hao 43 ambao wapo nchini tangu Agosti 13, wametoa pongezi hizo jana walipokutana na kuzungumza na Rais Magufuli Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Walitoa pongezi hizo baada ya kutembelea mradi wa ujenzi wa Bwawa la Nyerere litakalozalisha megawati 2,115 katika Mto Rufiji, mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (standard gauge railway) unaoanzia Dar es Salaam hadi Morogoro, jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, mradi wa ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya barabara ya Morogoro na Sam Nujoma (Ubungo Interchange), mradi wa upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, mradi wa usambazaji wa gesi (Taifa Gas), mradi wa udhibiti wa mawasiliano Tanzania na mradi wa ujenzi wa daraja la Tanzanite (New Selander Bridge) katika Bahari ya Hindi.

Kwa upande wa Zanzibar, mabalozi hao wametembelea mradi wa ujenzi wa jengo la biashara na makazi (shopping mall) eneo la Michenzani, mradi wa ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Sheikh Abeid Amani Karume, mradi wa ujenzi wa nyumba za kisasa wa Fumba Wilaya ya Magharibi, mradi wa ujenzi wa barabara ya Kaskazini - Bububu - Mkokotoni na mradi wa ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi katika eneo la Manga Pwani.

Mabalozi hao wameeleza kuwa utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na juhudi nyingine kubwa zinazofanywa na serikali katika nyanja mbalimbali za huduma za jamii zimeleta heshima kwa nchi na machoni mwa Jumuiya ya Kimataifa, na kwamba zimedhihirisha kufikiwa kwa malengo ya Tanzania kuingia katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Pia wampongeza kwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kipindi cha mwaka mmoja na wameahidi kuongoza vyema katika mikutano ya mabalozi wa SADC katika nchi wanazowakilisha kwa kuzingatia mwelekeo ambao Rais Magufuli ameutoa katika Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika Agosti 17 na 18.

Akizungumza baada ya kuwasilikiza mabalozi hao, Rais Magufuli aliwapongeza kwa kazi wanazozifanya katika nchi wanazoiwakilisha Tanzania na amewataka waendelee kutekeleza majukumu yao kizalendo na kwa kutanguliza maslahi ya Tanzania.

Pamoja na kueleza kuhusu hali ya uchumi wa nchi, juhudi za kuwapelekea maendeleo Watanzania na juhudi za kujenga uwezo wa kujitegemea, Rais Magufuli aliwataka mabalozi hao kutafuta wawekezaji watakaowekeza katika miradi yenye manufaa hapa nchini.

"Nataka Mabalozi mtuletee miradi ya maendeleo, ifike mahali Balozi ujiulize kwa kuwa kwangu Balozi nimepeleka nini nyumbani? Nimewezesha kujengwa kiwanda? Kujengwa barabara? Kujenga daraja au jengo fulani?" Alisema.

Aliwasisitiza mabalozi hao kuhakikisha wanasimamia na kufuatilia kwa karibu masuala wanayoamini yana manufaa kwa nchi ikiwamo uwekezaji na kwamba wasikubali kukwamishwa na viongozi ama wizara yoyote.

Kuhusu changamoto mbalimbali walizomueleza, Rais Magufuli ametoa wito kwa mabalozi hao kuzishughulikia pale wamapoona wana uwezo na ameitaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kufanyia kazi taarifa wanazopelekewa na mabalozi hao kwa wakati.

# Wauza nyama mbovu buchani waonywa

**Na Boniface Gideon,** TANGA

SERIKALI imetoa onyo kali kwa wafanyabiashara wa nyama watakaobainika kuuza bidhaa hiyo isiyo na viwango.

Onyo hilo limetolewa na Mratibu wa Usalama wa Chakula Halmashauri ya Jiji la Tanga, Alice Maungu, wakati akizungumza na Nipashe, kufuatia kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa wateja kwamba baadhi ya wafanyabiashara huchanganya nyama zilizoharibika hasa nyakati za jioni.

Alice alisema, wafanyabiashara hao wanatumia ujanja huo kwa kutaka kupata faida kubwa.

"Ni kweli tumekuwa tukiendesha operesheni ya kukagua nyama kwenye bucha zote zilizopo katika Jiji la Tanga na tunawakamata na kuziteketeza nyama," alisema.

Alisema operesheni ya kukamata wafanyabiashara wanaouza nyama zisizo na viwango ni endelevu na inafanyika kwa kushtukiza kwenye maeneo yote ya Jiji la Tanga, alisema.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuzingatia sheria na miongozo ya biashara zao ili kuwalinda wananchi na biashara zao pia.

Katika hatua nyingine, alipiga marufuku wamiliki wa bucha kutumia magogo kukatia nyama na kuwataka wafanyabiashara wafuate sheria kwa kutumia mashine maalumu zakukatia.

Alisema matumizi ya magogo ni hatari kwa afya ya mtumiaji kwa kuwa yanahifadhi vijidudu (bakteria) ambavyo vinaweza kusababisha magonjwa hatari kwa binadamu.

Aliwataka waananchi kuwa makini wanaponunua nyama.

Nao Baadhi ya wananchi akiwamo Ashura Mohamed na Zaina Abdalah, walikiri kununua nyama aina ya utumbo nyakati tofauti ukiwa umeharibika na kuwarudishia wahusika.

"Mimi wiki mbili zilizopita nilinunua nyama aina ya utumbo soko la Mgandini muuzaji alinichanganyia na niliyooza nilimrudishia mwenyewe kwa kuwa nilikua sijui pa kuipeleka," alisema Zaina.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**

Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.



NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie

E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**Thomas Komba** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0595-0070** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2001 katika shule ya Sekondari Ruvuma.

Yeyote atakar kiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/TAB/RB/57042/2019**

## KUPOTEA KWA CHETI



Rehema Augustin Ibrahim anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4484/0057 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Tanner.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo **chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: SOM/RB/201/2019**

## KUPOTEA KWA KADI

**DANIEL ALON NGUVILA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA TVS KING YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 343 AQF.

CHASSIS NAMBA MD6M14PK1F4A20204. ENGINE NAMBA OK4AF4161731.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU,

TAARIFA YA POLISI:

**MBE/RB/233631/2019.**

215385702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ally Ramadhani Kasanura** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa T 613 BBU aina ya TOYOTA MARK II, yenye chasis namba JZX 906597598.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:

**OB/RB/4581/2016**

215384702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MCA/84**
**MAHAKAMA YA MWANZO MAKANG'WA**
**WILAYA YA CHAMWINO DODOMA**
**MIRATHI NA.03 YA 2019.**

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MAKANG'WA WILAYA YA CHAMWINO - DODOMA.

Ombi la GODFREY ELIAS KIRA kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu JOHN ELIAS KIRA.

Mtu yeyote mwenye pingamizi na mirathi hapo juu, ,Tanzania bara na visiwani unatakiwa ulete pingamizi hilo Mahakama ya mwanzo Makang'wa kabla mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu ndani ya miezi mitatu.

Tangazo hili limetolewa Mahakama ya mwanzo Makang'wa Chamwino – Dodoma. tarehe 22/08/2019.



215385502

## KUPOTEA KWA CHETI



**Geofrey Juma** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye ndex namba 118 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1991 katika shule ya Sekondari Shirati, vheti cha Ualimu chenye index namba EA023615 kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Tarime mwaka 1994.

**Yeyote atakaevion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: KRG/RB/81/07**

115384302

**JAHMURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo TANGA MJINI
Usimamizi wa Mirathi NAMBA 19 123/2019
Ombi la John RIchrd Semkuya kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi marehemu Richard Semkuya Nyange


Kwa: Yeyote Anayehusika

……………………………………….

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 19/08/2019



215384402


Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

NEWSPAPER

CLASSFIED ADVERTISEMENT

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.

E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# OZIL AANZA MAZOEZI KUIVAA LIVERPOOL, SPURS




**LONDON,** England

MESUT Ozil amerudi kwenye mazoezi na timu ya Arsenal tayari kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu ya England zinazokuja dhidi ya Liverpool na Tottenham.

Kiungo huyo bado hajacheza mchezo wowote kwenye ligi hiyo msimu huu, baaada ya kuwa mhanga wa jaribio la kutekwa na gari na genge moja la wahuni akiwa pamoja na mchezaji mwenzake, Sead Kolasinac mwezi uliopita.

Arsenal ilisema kwamba wachezaji hao hawakuwapo kwenye mchezo wao wa ufunguzi wa ligi dhidi ya Newcastle kwa ajili ya "ulinzi zaidi", huku Ozil aliukosa mchezo wa ushindi wa Jumamosi dhidi ya Burnley kwa sababu ya kuwa mgonjwa.

Hata hivyo, mchezajii huyo wa zamani wa Ujerumani alipigwa picha akiwa mazoezini na wachezaji wenzake Jumatano, na kutoa ishara kwamba atakuwapo kwenye mechi zinazokuja dhidi ya bingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool na wapinzani wao wa jiji moja la London, Tottenham.

Chanzo kimoja kiliidokeza ESPN FC mapema mwezi huu kwamba, wawakilishi wa Ozil wanafanya mazungumzo na Klabu ya D.C. United ya Marekani kuona uwezekano wa kuhamia kwenye ligi hiyo maarufu kama MLS.

Taarifa hizo zilisema kwamba, kuna uwezekano mkubwa Ozil akaondoka klabuni hapo kipindi cha dirisha dogo la Januari.

## Tajiri namba 1 Uingereza ainunua Nice

**LONDON,** England

SIR Jim Ratcliffe, ambaye ni tajiri namba moja nchini Uingereza amepewa mamlaka ya mwisho ya kumaliza kuinunua Klabu ya nchini Ufaransa ya Nice.


Mamlaka ya ushindani wa masoko ya nchini Ufaransa imemuwashia taa ya kijani tajiri huyo Jumatano na sasa amepewa ruhusa ya kuendelea na mpango wake huo.

Ratcliffe, mwanzilishi na Afisa mtendaji mkuu wa kampuni ya kubwa ya kemikali ya Ineos, sasa atalipa euro milioni 100 kwa wamiliki Chien Lee na Alex Zheng ili kuwa bosi mpya wa klabu hiyo.

Uhamishaji wa fedha kwa njia ya benki utafanyika mwishoni mwa wiki hii na mfanyabiashara huyo, ambaye utajiri wake ni wa thamani euro bilioni 21.

Atahudhuria kwa mara ya kwanza kwenye mchezo wa Nice dhidi ya Marseille katika Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Jumatano ya Agosti 28 mwaka huu akiwa kama ndiye mmiliki mpya.

Nice kwa sasa ni moja ya klabu ghali zaidi katika historia ya soka la Ufaransa, ikiwa na gharama ya zaidi ya euro milioni 79 ambazo zilitumika na matajiri wa Qatar kuinunua Paris Saint-Germain mwaka 2011.





## Juventus wataka kipute Serie A kianze mapema

**ROME,** Italia

LIGI Kuu ya Italia, Serie A, inatakiwa kuanza mapema zaidi ili kukuza soko la bara la Asia pamoja na kuimarisha mapato ya klabu, Ofisa Mtendaji wa Juventus, Giorgio Ricci amesema.

Ligi kubwa tano za Ulaya zilifurahia rekodi ya mapato mazuri zaidi msimu wa 2017-18, kwa pamoja zikiingiza kiasi cha bilioni 15.6, lakini Serie A ilikuwa nyuma ya EPL, Bundesliga na La Liga.

"Tunatakiwa kutafuta uwiano mzuri kati ya nyumbani na kimataifa," alisema Ricci akiiambia BBC Sport.

"Sio tu suala la muda wa matangazo, ni suala ya haki ya kugawawa na nani anaonyesha mechi.

"Kwa kesi hiyo tofauti kati ya Ligi Kuu ya England na Serie A ni kubwa. Hii ni habari ya zamani tunatakiwa kubadilika na kupigania ligi kuweza kupata mapato makubwa zaidi."

Aidha, Juve imesema kwamba, kuanza kwa ligi ya Italia majira ya jioni kunapunguza kuwavutia watazamaji kutoka barani Asia.

Mkataba wa sasa wa haki za matangazo ya televisheni kwa Serie A unamalizika mwaka 2021 kwa bara la Asia.

Msimu mpya wa Ligi Kuu ya Serie A unaanza Jumamosi kwa mabingwa Juve

## HABARI MICHEZO

# Spurs yatakiwa kumuuza Eriksen

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham ni lazima imuuze Christian Eriksen sasa kama ataendelea kugoma kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa golikipa wa zamani wa Spurs, Paul Robinson.

Mkataba wa sasa wa Eriksen unatarajia kumalizika mwishoni mwa msimu huu na mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka klabuni hapo akibainisha mwanzoni mwa msimu huu kwamba "anataka kujaribu kufanya kitu kipya".

Robinson anaona kwamba, Eriksen tayari ameshaamua kutosaini mkataba mpya na amewashauri Spurs kumuuza kiungo huyo kama hataki kuongeza mkataba na klabu hiyo.

"Nitashangaa kama wanaendelea kubakia naye, kutokana na ukweli kwamba hajasaini mkataba mpya ambao amepewa ofa," alisema Robinson wakati akihojiwa na Sky Sports.

"Ameshapiga kelele ya kutaka changamoto mpya. Amekuwa klabuni hapa kwa miaka sita na ukweli kwamba hajasaini mkataba mpya na yupo kwenye mwaka wake wa mwisho.

"Nafikiri ataleta tatizo kwa timu hasa kwa wachezaji wanaomzunguka. Nafikiri ni wakati muafaka angeachwa aondoke tu."





# RONALDO: THAMANI YANGU NI BIL. 763.5/-

**LISBON,** Ureno

CRISTIANO Ronaldo amesema kwamba, ada ya uhamisho kwenye mpira wa miguu "imepaa" zaidi na kwamba mchezaji wa aina yake kwa soko la sasa angeuzwa euro milioni 300 sawa na Sh.bilioni 763.5 za Tanzania.

Juventus walitumia euro milioni 112 wakati walipomsajili nahodha huyo wa Ureno kutoka Real Madrid mwaka 2018.

Ni wachezaji watano tu Neymar, Kylian Mbappe, Joao Felix, Antoine Griezmann na Philippe Coutinho ndio wamegharimu ada kubwa zaidi.

Wawili kati yao waliotumia fedha hizo nyingi si makinda na Ronaldo mwenye umri wa miaka 34, sasa anaona kwamba kiwango hicho kimeongezeka mno kwa wachezaji chipukuzi ambao hawajaweza kuthibitisha ubora wao.

"Leo hii mtazamo wa biashara ya mpira wa miguu ni tofauti kabisa," alisema nyota huyo katika mahojiano na televisheni ya Ureno ya TVI.

"Nikichukulia mfano wa kesi ya Joao Felix. Leo hii kila mchezaji ana thamani ya euro milioni 100, bila hata kuthibitisha ubora wake. Kuna fedha nyingi kwenye mpira wa miguu.

"Mabeki wa kati na magolikipa wana thamani ya euro milioni 70 hadi euro milioni 80.

"Sikubaliani na hilo, lakini hii ndio duniani tunayoishi. Soko lipo hivyo, tunatakiwa kuheshimu hilo."

Ronaldo aliwekza rekodi ya ada ya uhamisho kubwa zaidi wakati Madrid walipotoa euro milioni 94 kumnunua kutoka Manchester United mwaka 2009.

Alipoulizwa ni kiasi gani kingetumika kumnunua kama angekuwa na umri wa miaka 25 kwa sasa, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, alijibu: "Ni ngumu kufanya mahesabu.

# *Zappacosta ajiunga kwa mkopo AS Roma*

**LONDON,** England

DAVID Zappacosta amekamilisha uhamisho wa kujiunga na Klabu ya AS Roma ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A kwa mkopo.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Italia, alifika Roma Jumanne kukamilisha mpango huo.

Zappacosta alijiunga na Chelsea kwa mkataba wa miaka minne akitokea Torino kwa pauni milioni 23 mwaka 2017.

Lakini amefanikiwa kucheza mechi 22 za Ligi Kuu, katika msimu wake wa kwanza alicheza mara nne tu mnamo 2018-19. Hakuonekana katika timu ya Chelsea msimu huu.

Na msimu huu ameonekana hana nafasi katika kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Frank Lampard na hivyo ameamua kutimka.

Beki wenzake David Luiz na Gary Cahill tayari wameondoka hapo Stamford Bridge msimu huu wa kipindi cha majira ya joto.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LUKAKU AICHANA UTD SHAMBULIO LA POGBA

●●● Ni kawaida yao kutafuta mtu wa kumshambulia, alitafutwa mmoja wetu mimi, Paul ama Alexis...

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku ameishukia Manchester United kwa kushindwa kutimiza wajibu wake ipasavyo wa kumlinda yeye dhidi ya vyombo vya habari na kudai kwamba yeye, Paul Pogba na Alexis Sanchez wameendelea kufanywa mbuzi wa kafara.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, Lukaku alijiunga na Inter kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la Ligi Kuu England kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 75, ikiwa ni miaka miwili tu kupita tangu aliponunuliwa kwa dau kama hilo hapo Old Trafford akitokea Everton.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 26, alikosolewa sana wakati akichezea United akiwa chini ya kocha Jose Mourinho na nafasi yake katika kikosi cha kwanza ilichukuliwa na Marcus Rashford baada ya Ole Gunnar Solskjaer kuanza kuinoa United.

**Lukaku anahisi palikuwa na mueleke0 usiofaa kuhusu kiwango chake kama ilivyo kwa Pogba na Sanchez, ambaye amekuwa akipigiwa upatu wa kujiunga naye hapo Inter.**

"Lazima wapate mtu," Lukaku aliiambia LightHarted Podcast, ilionekana ilirekodiwa kabla ya yeye kujiunga na Inter. "Ni Pogba, ni mimi ama ni Alexis. Ilikuwa ni kati yetu watatu wakati wote. "Walitafuta mmoja wetu kumlaumu. Niliinua mkono wangu juu, kama, mwaka huu sidhani ni mimi pekee niliyecheza vibaya. Watu wengi walicheza vibaya, lakini walihitaji kutafuta mtu wao wa kumkosoa.

"Kama walitaka kuelekeza lawama kwangu, unajua nini, f*** ndiyo, fanya unachotaka kufanya kwangu.

"Nadhani timu ina uwezo mkubwa sana wa kufanya mambo kadhaa mazuri. Kuna vipaji vingi. Lakini si vipaji tu; lazima ujenge timu. "

Lukaku pia aligusia suala la maoni kwamba hakufaa katika staili ya uchezaji ya Solskjaer aliyoihitaji.

"Watu wengi hawakudhani ningeweza kuwa sehemu ya mfumo huo," alisema. "Hiyo ni hisia yangu kutoka kwa mazungumzo ambayo ninayo. Najua tu.

"Kwangu mimi, kitu kinachonifanya kucheka sana: ni namna gani mambo yanavyoharibika ni s*** yanaenda vibaya kwa timu yangu, lakini wakati ninaichezea timu ya taifa, ni vizuri? Na ni mwenye furaha."

## ZISIKUPITE

### SANCHO AANDALIWA DAU UTD

MANCHESTER United imemuweka winga wa Borussia Dortmund, Muingereza, Jadon Sancho, 19, ambaye pia anawindwa na Manchester City, kuwa windo lao la kwanza katika dirisha la usajili la Januari na inaandaa ofa ya pauni milioni 100. ***(Sun)***

### BARCA YAKWAMA KWA NEYMAR

BARCELONA imetoa ofa ya kwanza ya mkopo, na pauni milioni 137 kwa kipengele cha kumnunua Mbrazil Neymar, 27, zilizokataliwa na Paris St-Germain, wakati huu mabingwa hao wa Ligue 1 wakihitaji pauni milioni 229 kumwachia. ***(Marca)***

### HAVERTZ AVUTIA VIGOGO EPL

LIVERPOOL, Manchester City, Manchester United, Arsenal na Chelsea ni miongoni mwa klabu kubwa za Ulaya zinazovutiwa kumsajili mshambuliaji wa Bayer Leverkusen, Mjerumani Kai Havertz, 20, ambaye anathaminishwa na pauni milioni 91. ***(Sport1 - in German)***

### DE GEA KUISUBIRISHA UNITED

KIPA wa Manchester United na Hispania David de Gea, 28, bado hajamwaga wino katika mkataba mpya utakaomfanya kulipwa pauni milioni 350,000 kwa wiki na anaweza kuisubirisha klabu hiyo hadi Januari. ***(Sun)***

### LOVREN AIVUTIA LEVERKUSEN

BEKI asiyekubalika Liverpool kwa sasa, Mcroatia Dejan Lovren, 30, anaivutia Bayer Leverkusen ya Ujerumani baada ya kushindwa kukamilisha uhamisho wake wa kujiunga na Roma. ***(Bild - in German)***

### WANYAMA ANUKIA CLUB BRUGES

TOTTENHAM ipo katika mazungumzo ya kumuuza kiungo Mkenya Victor Wanyama, 28, kwa Club Bruges kwa dau la pauni milioni 11. ***(Telegraph)***

### BATSHUAYI KUKOMAA CHELSEA

STRAIKA wa Ubelgiji, Michy Batshuayi, 25, anataka kubaki na kupigania namba Chelsea, lakini atatazama upepo utakavyokwenda Januari. ***(Standard)***

### BENTEKE KUFUNGWA PALACE

CRYSTAL Palace ipo katika hatua za mwisho kukamilisha mchakato wa kumuongeza mkataba straika Mbelgiji Christian Benteke, 28, na beki wa kati Muingereza James Tomkins, 30. ***(Mail)***

### BOATENG AWEKWA SOKONI

BAYERN Munich imefungua milango ya kumuuza beki Mjerumani Jerome Boateng, 30, kwa pauni milioni 22. ***(Mail via Marca)***

### ALMADA APIGIWA HESABU CITY

MANCHESTER City inamfuatilia kwa karibu kiungo wa Velez Sarsfield, Muargentina Thiago Almada, 18, ambaye bado hajaongeza mkataba na klabu hiyo. ***(A Bola, via Manchester Evening News)***

### KLOPP KUMZUIA KANE

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, anataka kumchezesha kiungo Muingereza Herbie Kane, 20, katika Kombe la Carabao, ili kuhitimisha matumaini ya Portsmouth, Sunderland na Coventry ya kumsajili mchezaji huyo kwa mkopo. ***(Portsmouth News)***

# TANZANIA U-15: NI KUFA AU KUPONA VS RWANDA

**Na Somoe Ng'itu,** ASMARA

WACHEZAJI wa timu ya soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 15 wa Tanzania (U-15), ambao wanatarajia kuwakabili chipukizi wenzao kutoka Rwanda katika mechi ya tatu ya Kundi B itakayochezwa kwenye Uwanja wa Asmara nchini Eritrea, wamesema watahakikisha wanafanya kweli leo.

**Tanzania yenye pointi tatu katika mashindano hayo ya Afrika Mashariki na Kati iko kwenye nafasi ya tatu katika kundi hilo linaloongozwa na Rwanda ikifuatiwa na Uganda zenye pointi sita kila moja, huku Ethiopia yenye pointi moja ikishika nafasi ya nne na Sudan Kusini ambao hawana pointi wakiburuza mkia.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania, Maalim Saleh, alisema wachezaji wake wataendelea kupambana katika mechi hiyo, huku wakiwa wamewafanyia "upelelezi" wapinzani wao Rwanda katika mechi zao zilizopita.

Saleh alisema wanafahamu ili waweze kusonga mbele katika mashindano haya, wanatakiwa kushinda mechi ya leo na ile ya mwisho ya hatua ya makundi itakayochezwa keshokutwa Jumapili dhidi ya Ethiopia.

"Tunaendelea kuimarika katika kila idara, pia wachezaji wameanza kufuata kile tunachowaambia, tunajua Rwanda si timu nyepesi, nao pia watakuja wakiwa wamejipanga kusaka ushindi, kwa upande wangu naamini tutapambana ili kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo ya kesho (leo)," alisema Saleh.

Mshambuliaji wa timu hiyo, Rabin Sanga, alisema mashindano haya ni magumu, lakini bado wanaamini Tanzania ina nafasi ya kushinda kombe la michuano hii inayochezwa kwa mara ya kwanza kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

"Bado nafasi na imani ya kusonga mbele tunayo, tunajua Rwanda pia wamejipanga, hatutawahofia, tutacheza kufa au kupona ili kupata ushindi," alisema Sanga, ambaye alifunga mabao mawili katika ushindi wa 6-0 walioupata juzi dhidi ya Sudan Kusini.

Mechi nyingine ya mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Uganda dhidi ya Sudan Kusini.

Michuano hiyo itaendelea tena kesho kwa mechi za Kundi A, ambapo Burundi itaikabili Sudan na Eritrea itawakaribisha Somalia wakati Tanzania itamaliza hatua ya makundi kwa kuvaana na Ethiopia hapo Jumapili.



Kocha Msaidizi wa KMC, Mrage Kabange, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana namna walivyojiandaa kuelekea mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Kigali ya Rwanda utakaopigwa Uwanja wa Taifa leo. Kushoto ni Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Cliford Ndimbo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Lipuli FC yaanika silaha zake Ligi Kuu

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

LIPULI imeanika jeshi lake litakaloiwakilisha katika michuano ya Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho la Soka nchini (FA Cup) kwa msimu mpya wa 2019/20 wakati huu ikijiandaa kufungua dimba la kinyang'anyiro hicho Jumapili.

Miamba hiyo inayotumia Uwanja wa Samora mjini Iringa, keshokutwa Jumapili itaikaribisha Mtibwa Sugar katika mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Bara msimu huu na kuelekea mchezo huo, mdau wa maendeleo ya michezo mkoani Iringa, Fadhili Fabian Ngajilo amewaasa viongozi wa Lipuli FC kuepuka migogoro, majungu na fitna ili kusonga mbele.

Ngajilo alisema hayo mapema wiki hii alipota msaada wa mipira kumi kwa timu hiyo wakati wa Siku Maalum ya Timu ya Lipuli FC kutambulisha kikosi chake kipya iliyofanyika Uwanja wa Samora mjini Iringa.

Alisema mpira hiyo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 1.6 na yenye ubora wa Shirikisho la Soka Duniani (Fifa) imetengenezwa nchini China kwa ajili ya kuwezesha timu hiyo kuondokana na changamoto ya vifaa vya michezo.

Timu zingine zilizopewa mipira ni Kihesa FC (mipira miwili), Veteran FC (miwili), Mtwivilla FC (mitatu) na Iringa United (miwili) na kufanya jumla ya mipira 17 ilitolewa na mdau hiyo.

Wakati huohuo, timu ya Lipuli FC ilitambulisha kikosi chake kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania 2019/20 ambacho kinaundwa na makipa; Agathony Ng'ingo na Shabani Mussa.

Walinzi ni Godfrey Kameta, David Mussa, Mussa Lyango kutoka Vital'O ya Burundi, Emmanuel Sekule, Philipo Mwayobya, Emmanuel Kichiba, Hamad Waziri, Novalty Lufunga, Derrick Karulika (DR Congo) na Steven Mganga.

Viungo ni Fredy Tangalu, Josephat Ntamak (Vital'O), Jimmyshoji Mwasondole, Ally Lyungu (Lipuli U-20). Patrick Voctor (Nigeria), Mwinyi Elias na Paul Materas.

Washambuliaji ni Issa Rashid, Daruwesh Saliboko, Paul Nonga, Joshua Ibrahimu (Kenya), Kenneth Masumbuko, Rashid Karihe, Shehuu Magaji (Nigeria) na Albert Kisake.

## Azam: Wahabeshi hawatoki Chamazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC wameendelea kushikilia msimamo wao kuwa wanachokitaka ni sapoti tu ya mashabiki, na kwamba suala la ushindi kwao katika Uwanja wa Chamazi ni kawaida.

Azam FC inahitaji ushindi kuanzia bao 2-0 ili kuweza kusonga mbele dhidi ya Fasil Kenema ya Ethiopia kwenye mechi hiyo ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya ile ya awali kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini.



Katika mechi hiyo itakayopigwa majira saa 10:00 alasiri kwenye Uwanja wa Chamazi, Azam imesema haijawahi kupoteza uwanjani hapo ikiwa katika majukumu ya mechi za kimataifa na imepania kuendeleza rekodi hiyo kesho.

Kauli hiyo, aliitoa Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffary Maganga (pichani) na huku akisisitiza maandalizi yamekamilika kwa asilimia 80 na kilichobaki ni wachezaji kutekeleza wajibu wao uwanjani.

"Kocha Etienne Ndayiragije amekuwa na programu maalumu kuelekea mchezo huo, lengo ni kupata matokeo chanya, tunaomba mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani na kila atakayeingia atapata na 'Ice cream ya ukwaju' bure mlango," alisema.

## Simba yaipasua kichwa JKT TZ

**Na Shufaa Lyimo**

HUKU ikiendelea kujifua kuelekea mechi yao ya ufunguzi ya Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20, timu ya JKT Tanzania imesema pamoja na kujipanga vizuri, wataivaa Simba kwa tahadhari kubwa Alhamisi ijayo kutokana na kutambua ubora wa wapinzani wao hao.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdallah Bakhresa alisema, kikosi chake kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya msimu huo hususan mechi hiyo ya dhidi ya Simba.

"Timu yangu inaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya msimu ujao ambao utakuwa na ushindani mkubwa, mechi yetu ya kwanza tutakutana na Simba, ninaiheshimu timu hiyo, hivyo tutacheza kwa tahadhari, alisema Bakhresa.

Alisema anashukuru hali za wachezaji wake wote zipo vizuri na hana majeruhi yoyote kwa sasa.

# Michezo

Ijumaa Agosti 23, 2019

Nipashe




Lukaku aichana Utd shambulio la Pogba UKURASA 30



Wachezaji wa Simba; Kutoka kushoto ni Meddie Kagere, Shomari Kapombe na Sharaf Eldin Shaiboub wakiwa mazoezini kuelekea mechi dhidi ya UD Songo. **PICHA: SIMBA**

# Simba hii ukiumia umepoteza namba

●●● Ajibu, Manula, Da Silva warejea, ni vita nani aanze dhidi ya UD Songo Jumapili, mtihani kwa Aussems...

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI kamili la kikosi cha Simba linamekamilika kuelekea mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo itakayopigwa keshokuwa Jumapili Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam baada ya wachezaji watatu waliokuwa majeruhi kurejea kujifua na wenzao.

**Simba iliwapoteza wachezaji wake watatu; kipa Aishi Manula, mshambuliaji Ibrahim Ajibu, na mshambuliaji Mbrazil Wilker Henrique da Silva waliokuwa majeruhi, lakini sasa wamerejea kikosini kujifua na wenzao.**

Wakati wachezaji hao wakirejea, Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu amesema kwamba chumba cha majeruhi amebaki nahodha John Bocco, ambaye aliumia wakati wakishinda 4-2 na kutwaa Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC wiki iliyopita.

"Ajibu, Manula na Wilker da Silva wamereja na wanajifua na wenzao, kilichobaki sasa ni uamuzi wa Kocha Mkuu Patrick Aussems, kuamua atampanga nani kuelekea mechi yetu ya marudiano Jumapili," alisema Rweyemamu.

Hata hivyo, licha ya nyota hao kurejea kutokana na ubora wa kila mchezaji anayepata nafasi kuonyesha uwezo mkubwa, Aussems atalazimika kuchanga karata yake vizuri ya nani aanze katika kikosi hicho.

Kipa Beno Kakolanya, ameonyesha ubora wa hali ya juu tangu alipoanza kuidakia timu hiyo dhidi ya Power Dyanamos kwenye mechi ya Simba Day na kuiongoza kushinda 3-1, kisha wakatoka sare tasa dhidi ya UD Songo ugenini kabla ya kuiongoza kushinda 4-2 dhidi ya Azam FC kwenye Ngao ya Jamii.

Ni wazi, Manula anaweza kusubiri kwa muda kabla ya kumshawishi Aussems hasa ukizingatia anahitaji kujiweka fiti zaidi kutokana na kutokea chumba cha majeruhi, lakini pia Ajibu na Da Silva wana kazi ya kufanya katika nafasi zao.

Ajibu na Da Silva wanapaswa kuonyesha ubora wa hali ya juu wakati huu Bocco akiwa majeruhi, kwani tayari hakuna kati yao anayeweza kumweka benchi kwa sasa, Sharaf Eldin Shaiboub ama Clatous Chama au hata Hassan Dilunga 'HD'.

Upana wa kikosi cha Simba umeanza kuonekana mapema hususan idara ya kiungo mshambuliaji kutokana na uwezo mkubwa unaoonyeshwa na wachezaji wa nafasi hizo.

Simba keshokutwa itahitaji ushindi wa aina yoyote ili kuweza kusonga mbele katika mchuano hiyo ambayo msimu uliopita iliishia robo fainali kufuatia kutolewa na TP Mazembe ya DR Congo kwa jumla ya mabao 4-1.

Kama Simba itasonga mbele ama UD Songo, itakuna na mshindi kati ya FC Platinum ya Zimbabwe na Nyasa Bullets ya Malawi ambayo kesho itakuwa ugenini ikisaka matokeo baada ya mechi ya awali kulazimishwa sare tasa nyumbani.

## Niyonzima, Kaseja walianzisha mapema

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI nahodha wa Klabu ya KMC FC, Juma Kaseja, akiwataka wachezaji wenzake kushirikiana vizuri uwanjani katika mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Kigali ya Rwanda, mchezaji wa zamani wa Yanga na Simba, Haruna Niyonzima amesema wamefuata matokeo na si vinginevyo.

Timu hizo zitarudiana leo Uwanja wa Taifa saa tisa alasiri baada ya kutoka sare tasa wiki mbili zilizopita mjini Kigali, Rwanda na mshindi wa mchezo huo atakutana na mshindi wa jumla kati ya Masters Security Services ya Malawi na Proline FC ya Uganda anapotokea Kocha Mkuu wa KMC FC, Jackson Mayanja.

Na Niyonzima amesema wanaiheshimu KMC kwa kuwa wanajua ni timu nzuri inayocheza soka la kuvutia, lakini wamefuata matokeo jijini Dar es Salaam baada ya kutoka sare tasa mchezo wa awali nyumbani.

"Tunajua ni timu nzuri na ina wachezaji wazuri, utakuwa ni mchezo mgumu, lakini tunachotaka ni kupata matokeo na kusonga mbele katika michuano hii," alisema Niyonzima.

Lakini Kipa Kaseja alisema jana kuwa kwa upande wake atacheza kufa au kupona kuhakikisha anaipa ushindi timu yake, jambo ambalo amewaomba wachezaji wenzake kubeba morali huo ili kuweza kuipeperusha vema bendera ya nchi.

"Kesho (leo) ni kufa au kupona, AS Kigali hawatoki, watajuta kutufahamu tunataka ushindi wa mabao mengi mapema," alisema Kaseja huku akieleza kwa sasa yupo fiti baada ya kuugua hivi karibuni.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002